

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Nane – Tarehe 11 Februari, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaweza kukaa.  
Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU**

**SPIKA:** Kiapo cha Uaminifu

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

Waheshimiwa Wabunge, wafuatao waliapa Kiapo  
cha Uaminifu

1. Mhe. Ameir Abdalla Ameir
2. Mhe. Bakar Hamad Bakar
3. Mhe. Bahati Khamis Kombo
4. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
5. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyoona  
kwenye *Order Paper* tumekuwa na zoezi la Kiapo cha  
Uaminifu baada ya jana kupokea Waraka kutoka kwa Spika  
wa Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid

kwamba wenzetu hawa Waheshimiwa ambao tumewaapisha hivi punde ndiyo wamechaguliwa kutoka katika Baraza la Wawakilishi kama Katiba yetu inavyotaka.

Waheshimiwa Wabunge, Katiba yetu inasema Wajumbe watano wa Baraza la Wawakilishi watajiunga na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, takwa hilo la Katiba limekwishatekelezwa, sasa nafasi zilizobaki ni zile tu za Mheshimiwa Rais kuzijaziliza kadri atakavyoona inafaa. Sasa Bunge linazidi kukamilika katika kuliunda kwake kwa maana ya wajumbe. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Muuliza swali la kwanza atakuwa Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Jimbo la Kawe.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha kumi zinazozungumzwa sana Barani Afrika. Ni lugha ya pili kwa kuzungumzwa na watu wengi Barani Afrika na pia ni kati ya lugha kumi zinazozungumzwa sana duniani. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Kiswahili kinakuwa bidhaa hasa wakati wa kuchangia diplomasia ya uchumi na kuwa fursa ya ajira kwa Watanzania? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye leo ametupa uhai wa kukutana hapa na kuendelea na shughuli zetu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, pili, niungane nawe kuwakaribisha Waheshimiwa Wabunge wenzetu kutoka Baraza la

Wawakilishi kuungana nasi kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Karibuni sana, tutawapa ushirikiano wa hali ya juu na kwa kweli mtasaidia sana kuchangia yale muhimu na kuishauri Serikali na sisi Serikali tupo tayari kupokea ushauri wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kujibu swali la Mheshimiwa Baba Askofu Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kiswahili sasa kimepata nafasi kubwa ya kuzungumzwa kwenye mataifa mengi duniani na wala siyo kuzungumzwa tu pia hata matumizi yake yameongezeka. Tumeanza kuona nchi mbalimbali kubwa duniani zikiandaa vipindi vya Kiswahili kwenye redio na kwenye magazeti yao. Hii ni ishara kwamba Kiswahili chetu sasa kinakua duniani kote.

Mheshimiwa Spika, nini Serikali inafanya kuimarisha diplomasia ya kiuchumi na kutengeneza fursa hata kwa Watanzania ambao ndiyo wenye Kiswahili? Kiswahili hiki hapa nchini kinazungumzwa na makabila yetu karibu yote na ndiyo lugha ambayo inatuunganisha Watanzania. Tumeanza kusambaza Kiswahili hiki kwenye ukanda wetu wa Afrika Mashariki, tumeona nchi zote za Afrika Mashariki zinazungumza lugha hii. Wote ni mashahidi tumeona jitihada ambazo zimefanywa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kusambaza Kiswahili kwenye Nchi za Ukanda wa Kusini (*SADC*) pale ambapo amekutana na Marais mbalimbali kuwahamasisha na sasa tumeona Kiswahili kimeanza kufundishwa kwenye nchi zao, kwa hiyo, Kiswahili kinazidi kupanuka.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, Kiswahili nacho kinaenda mbali zaidi, utaona Ujerumani, Marekani, Uingereza na Mataifa mengine makubwa yanaendelea kutumia Kiswahili. Sisi kama Serikali tumeweza kuwasiliana kupitia Balozi zetu, kila Balozi tumeiagiza kwenye nchi ambazo Balozi yupo kuanzisha kituo cha kujifunzia Kiswahili. Malengo yetu ni kupanua matumizi ya lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapowafikishia Mabalizi na kufungua vituo na kuwafanya wananchi wa nchi husika kujifunza Kiswahili hapo sasa tumeingiza kwenye diplomasia ya Kiswahili. Kwa kuwa sasa Kiswahili kinapendwa duniani kote na kinazungumzwa na nchi nyingi sisi Watanzania sasa tuna fursa ya kuwa walimu wazuri kwenye nchi hizo kwenye vituo vyetu vya kufundisha Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapokwenda kuwa walimu kwenye nchi hizo tayari tunafungua fursa za kiuchumi kwa kuajiri Watanzania kwenda kufanya kazi kwenye nchi hizo. Watanzania wakishapata ajira tunajua kodi kidogo inarudi nchini na tunaboresha uchumi wetu wa ndani. Kwa hiyo, tutatumia diplomasia hii kukuza uchumi wa ndani na hasa kwa kutoa fursa ya Watanzania kuajiriwa kwenye maeneo hayo kuendeleza kuboresha Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Swali linalofuata linatoka kwa Mheshimiwa Neema Kishiki Lugangira, uliza swali lako, kifupi tafadhali.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Spika, swali langu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kubwa la masoko ya mazao yetu hata kama tunazalisha kwa ubora wa juu. Je, Serikali iko tayari kupeleka wataalam wake nje ya nchi na hasa kwenye nchi ambazo zimefanikiwa ili kujifunza namna bora ya usimamizi wa masoko yetu? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lugangira, Mbunge wa Mkoa wa Kagera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kutafuta masoko kwenye mazao yetu lakini pia Mheshimiwa Mbunge anataka kujua

mpango wa Serikali wa kuwapeleka wataalam wetu nje ya nchi kujifunza kutafuta masoko. Sina uhakika sana kama alikuwa anataka kusisitiza kuwepo kwa masoko au suala ni kupeleka wataalam kujifunza masoko. Hata hivyo, Serikali yetu inatambua na inao mkakati ambao sasa tunaendelea nao wa kuzalisha mazao mengi ya chakula na biashara. Kwenye mazao yote ya biashara tumeendelea kuboresha kupata masoko ya ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuwapatia nafasi nzuri wakulima wetu kuuza mazao yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia inapoingia kwenye utaalum wa kutafuta masoko muhimu zaidi ni kujua kama mazao tunayozalisha tuna masoko huko nje? Tunachokifanya sasa kila zao kupitia Balozi hizi nazo tunazitumia kutangaza mazao tuliyonayo ndani ya nchi ili tuweze kuyauza kwenye nchi wanazotumia mazao hayo. Zoezi hili linaendelea na tunapata wateja wengi kuja kununua mazao yetu na hali hiyo imesababisha masoko yetu kuimarika.

Mheshimiwa Spika, muhimu kwetu sisi ni kutafuta mfumo mzuri unaowezesha mazao haya kujulikana na kuyauza na tupate bei nzuri. Kama ambavyo sasa ndani ya nchi tumeweka Mfumo wa Stakabali Ghalani ambao unakusanya mazao pamoja na kuwaalika wanunuzi kila mmoja anatamka atanunua zao hilo kwa shilingi ngapi kwa kilo, yule mwenye bei ya juu ndiye ambaye tunampa fursa ya kununua. Kwa hiyo, huo ni mfumo wa uuzaji wa mazao yetu ambao tumeuandaa na tutapata bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Serikali tunao mpango wa kutafuta masoko kwenye nchi ambazo zinazohitaji mazao hayo. Juzi hapa nilikuwa na Wabunge wa Mkoa wa Rukwa wakiomba Serikali iwasaidie kutafuta masoko ya mazao yanayolimwa Mkoani Rukwa kwa nchi za Zambia, Rwanda na Burundi. Kwa hiyo, kazi ambayo Serikali inafanya sasa ni kuwasiliana na nchi ambazo ni walaji wa mazao haya ili kuhakikishia kuwa mazao haya yanapolimwa na kuvunwa tunayapeleka kwenye nchi husika. Hiyo ni njia pia ya kupata soko zuri la mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali kwa sasa tunaendelea kujenga masoko ya kimkakati, masoko ya kikanda, ambayo tunayajenga pembezoni mwa nchi yetu ili kukaribisha ndugu zetu walioko jirani kuja kununua. Miezi mitatu iliyopita nilikuwa Mkoani Kilimanjaro, nimekwenda pale Horohoro, tunajenga soko kubwa sana ambalo pia wananchi wa maeneo hayo wakizalisha mazao yatawekwa hapo, wa nchi jirani wote watakuja hapo. Kwa hiyo tunawapunguzia ugumu wa kuingia mpaka huku ndani kutafuta mazao hayo badala yake tunawa-*allocate* kwenye masoko yale.

Mheshimiwa Spika, mwezi mmoja uliopita pia nilikuwa Mkoani Kigoma kule Kagunga. Tumejenga soko zuri sana. Kwa hiyo tunawakaribisha ndugu zetu wa Burundi na Rwanda kuja kununua pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunajenga soko lingine kubwa sana Mkoani Kagera pale Nyakanazi. Lengo letu wale wote kutoka Kongo, Rwanda watakuja pale Nyakanazi kwenye soko letu lile la zaidi ya bilioni 3.5 ili wapate bidhaa. Kwa hiyo muhimu kwetu sisi ni kuweka mkakati wa namna gani mazao yetu yaliyoboreshwa yaweze kupata thamani kubwa kwa lengo la kumfanya mkulima aweze kupata tija kwa kazi ya kilimo anayoifanya. Kwa hiyo Serikali inaendelea na maboresho haya, Waheshimiwa Wabunge kama mna mawazo mengine ya kuboresha masoko, tunawakaribisha ili Serikali iweze kuimarisha upatikanaji wa mazao haya na iweze kuuza mazao haya kwa bei nzuri sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao kutoka CHADEMA. Hayupo; Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali lifuatalo:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali iliona umuhimu wa kuwafikishia wananchi kule vijijini umeme kwa gharama nafuu, kwa hivyo wakaweka utaratibu wa kuunganishia nyumba umeme kwa Sh.27,000 tu. Je, Serikali haioni umuhimu

kwa kuzingatia kwamba maji ni uhai na ni hitaji kubwa sana kwa kila mtu hapa duniani, kuhakikisha kwamba wanaweka utaratibu kama huu wa kuweka gharama ya kumuunganishia mtu maji?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sasa hivi kule *MUWASA* na *RUWASA* natumaini na mamlaka nyingine za maji zitatoza 350,000 mpaka 600,000 kumuunganishia mtu maji. Sasa je, mtu ataweza kweli kuvuta maji kupeleka nyumbani? Kwa hiyo watu wameamua kuanza kunywa maji ya mfereji ambapo hiyo haisaidii...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa swali lako limeeleweka.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu; gharama za maji.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu wa gharama za maji kupitia Sera yetu iliyoko pale Wizara ya Maji. Utaratibu huu tumeanzisha taasisi zitakazotoa huduma za maji sasa hivi tumezepeleka mpaka wilayani tunaita *RUWASA*, taasisi ambazo zinashughulikia maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upatikanaji wa maji kupitia mahali ambako kuna vyanzo, naweza kukiri kwamba tunaweza kuwa tuna ugumu kidogo wa upatikanaji wa maji kwa ujumla wake, lakini pamoja na ugumu huo wa upatikanaji wa maji kwenye baadhi ya maeneo kwa kutokuwa na vyanzo, bado tumeweka viwango vya kawaida ili wananchi waweze kupata huduma. Malengo yetu ni kila mwananchi mpaka kwenye ngazi za vitongoji aweze kupata maji. Kwa sasa sera yetu inafika vijijini.

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa inafanywa ya zile *RUWASA* kuainisha vyanzo na gharama ya kuanzisha miradi hiyo. lakini pia na Wizara ya Maji nayo kuwekeza kwenye mamlaka hizo ili kupata maji ya kutosha mpaka kwenye ngazi za vijiji.

Mheshimiwa Spika, natambua yako malalamiko ya bei ambayo pia hata wakati tulipokuwa kwenye ziara tumeona baadhi ya maeneo bei zinatofautiana kutoka eneo moja mpaka eneo lingine. Wizara ya Maji inaendelea na utaratibu wa kuona, je, tunaweza kuwa na kiwango kimoja nchi nzima kama vile ambavyo tumefanya kwenye *REA* kulipa Sh.27,000 ili mtu apate kuvutiwa maji?

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo itakapokamilika, Wizara ya Maji itakuja hapa itatuambia sasa uvutaji wa maji kutoka kwenye chanzo au mahali ambapo unaweza kuunganisha kuleta nyumbani ni kiasi gani. Tutakapokuwa na maji mengi tutatamani sana kila mmoja avute bomba apeleke nyumbani kwake, lakini kwa sasa kwa kiwango hiki cha maji tunajenga vituo ili wananchi wote waweze kwenda hapo kwa ajili ya kupata maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala litakapokamilika na kiwango cha maji kikipatikana kwa wingi sasa tutakuja kuweka viwango vya kila mmoja kuvuta maji kupeleka nyumbani kwake. Huo ndiyo mkakati wa Serikali kwa sasa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Khatib Said Haji wa *ACT* Wazalendo, Mbunge wa Jimbo la Konde.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, miongoni mwa ahadi zilizopo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi na kupitia kauli za Mheshimiwa Rais, ni juu ya uboreshwaji wa maslahi ya wafanyakazi Tanzania. Wafanyakazi wa Tanzania wameendelea kuwa wavumilivu, wastahimilivu na wakijenga matumaini juu ya ahadi hii muhimu sana kwa maisha yao:-



Je, Serikali inatoa kauli gani, ni lini wafanyakazi wa Tanzania watapandishiwa mishahara yao na kuboreshewa maslahi yao? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khatib, Mbunge kutoka Pemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo dhamira na inaendelea na dhamira hiyo ya kuboresha maslahi ya watumishi wa umma. Tunalo eneo la mishahara, upandishaji wa madaraja na maeneo mengine pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani ilijifunza kwamba wakati wote tunapotangaza hadharani kupandishwa kwa mishahara kumekuwa kunatengeneza gharama kubwa kwenye masoko yetu na kusababisha ugumu wa maisha ya watu wengine. Unajua tunao wafanyakazi, lakini tuna wakulima, wafugaji, wavuvi; hayo ni makundi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa eneo la wafanyakazi peke yake ukitangaza hadharani kwamba tumepandisha mishahara kwenye masoko yetu, vituo vya mabasi na huduma nyingine zote zinapanda lakini wanapandisha hii kwa sababu ya maslahi ya kundi moja tu, tukiwa tuna makundi mengine hatuna *forum* za kupandisha maslahi yao. Kwa hiyo tumeona kwenye eneo hili tutumie njia ambayo si lazima twende hadharani, lakini tunaboresha maslahi ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maslahi ya wafanyakazi hayapo kwenye mishahara tu; kwa kuwapandisha daraja, tunawapandisha, kupunguza kiwango cha kodi nacho pia na namna mbalimbali za kumfanya mtumishi aweze kuboreshewa maslahi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wafanyakazi wengi wanasubiri kusikia kupanda kwa mishahara, lakini ukifanya hilo tayari unatengeneza ugumu wa maisha kwa sababu ya kupanda kwa vitu mbalimbali. Bado Serikali inaendelea kutafuta njia nzuri ya kuongeza maslahi ya mtumishi ambayo pia mengine yanakuwa zaidi hata ya mshahara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amesema mara kadhaa kupitia sherehe za wafanyakazi kwamba kupandisha mshahara kwa Sh.20,000 au Sh.30,000 haina tija, lakini mara nyingi ukiamua kupunguza kodi ambayo mfanyakazi analipa kutoka kwenye *double digit* kuja kwenye *single digit*, hilo ongezeko linaweza kuwa kubwa zaidi kuliko hata hili la kupandisha mshahara kwa Sh.10,000 na kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado Mheshimiwa Rais ameendelea kuahidi na Serikali hii imeendelea kuahidi kuboresha maslahi ya watumishi wa umma. Bado Serikali ipo na imeingia madarakani, tunatambua mchango mzuri sana unaotolewa na watumishi wa umma na Serikali yao inatambua na ndiyo Serikali sasa inapata mafanikio kwa sababu ya mchango wao mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe wito kwa watumishi wa umma, wasikate tamaa wakidhani kutangaza mshahara hadharani ndiyo kunaweza kutatua matatizo. Muhimu zaidi kupitia Mabaraza ya Wafanyakazi ambayo tunakaa nayo mara kwa mara kujadiliana namna nzuri ya kuongeza maslahi, tunaendelea kukaa na zile taasisi/jumuiya za wafanyakazi kuweza kutafuta njia nzuri ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Kwa hiyo wafanyakazi wetu waendeleo kufanya kazi, tuendeleo kuiamini Serikali na tuendeleo kutumia vyombo vyetu kwa maana ya jumuiya zetu za wafanyakazi ili kuendelea kuzungumza maeneo ambayo tunahitaji kuyafanyia kazi, kwa lengo la kuleta maslahi kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mathayo David Mathayo, Mbunge wa Same Magharibi.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutokana na sera nzuri za Chama Cha Mapinduzi katika elimu, hususan elimu bila malipo na kutokana na kuongezeka kwa shule za sekondari za kata, *enrollment* ya wanafunzi imekuwa ni kubwa sana; na hii imesababisha kuonekana kwamba kuna upungufu mkubwa sana wa idadi ya Walimu katika halmashauri zetu. Wakati huohuo wapo zaidi ya Walimu 6,000 ambao ama wanastaafu au wengine wachache kufariki dunia, lakini Utumishi inachelewa kutoa vibali vya kuwaajiri Walimu wale:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba kasi ya ongezeko la wanafunzi inakwenda na uwiano sawa na kasi ya ongezeko la walimu? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumeanza kuona faida ya maazimio na maamuzi ya Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli ya elimu ya msingi ambayo inaanza kuanzia chekechea mpaka kidato cha nne kwenda kusoma bila malipo yoyote na kuwa na ongezeko kubwa la vijana ambao sasa wanakwenda kusajiliwa darasa la kwanza, lakini pia hata kidato cha kwanza kwenda cha nne.

Mheshimiwa Spika, manufaa haya yanatokana na utaratibu wa awali ambao ulikuwa umezalisha michango mingi sana kwenye shule na kukwaza Watanzania kupeleka watoto wao shuleni. Sasa baada ya kuanzisha elimu bure

tumeona pia hata wale watoto wanaotoka kwenye familia zisizokuwa na uwezo wanakwenda sasa shule kupata elimu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kutoka elimu ya msingi mpaka sekondari yote hii tunaita elimu msingi ambayo mtoto ni lazima asome na amalize kidato cha nne na akipata ufaulu anaendelea kidato cha tano kwenye elimu ya juu ya sekondari. Hili pia limefanya kuwe na hitaji la ongezeko la walimu, miundombinu nayo lazima iongezwe na Serikali kote huko inafanya jitihada za kuongeza miundombinu kwa kuhakikisha kwamba kila tunaposajili wanafunzi darasa la kwanza wote waingie madarasani na wakae kwenye madawati.

Mheshimiwa Spika, wanapomaliza darasa la saba wanafaulu kuingia kidato cha kwanza tunahakikisha kwamba tunakuwa na miundombinu ya kutosha ili kidato cha kwanza wanapoanza shule waanze wakiwa darasani na kuendelea mpaka elimu ya kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, wote mnatambua tulitoa maagizo kwa wakurugenzi kuhakikisha kwamba wanafunzi wote waliofaulu mwaka huu wote waingie darasani na waanze kusoma. Ifikapo tarehe 28, Mwezi huu wa Februari, kila halmashauri ihakikishe imeshakamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa, vyoo na nyumba za Walimu ili wanafunzi wanapoingia waweze kuanza masomo yao.

Mheshimiwa Spika, sasa ongezeko hili pia linataka mahitaji ya ongezeko la Walimu na Serikali inaendelea kuwaajiri. Hapa juzi kulikuwa na ajira za Walimu 13,000. Awamu ya kwanza tumepeleka Walimu 8,000, wiki mbili zilizopita tumeshasambaza Walimu 5,000 na bado tunaangalia tunapata ripoti za upungufu wa Walimu kwenye maeneo gani. Bado vibali vya ajira vitatoka na tutaendelea kuajiri kadri tunavyokuwa na uwezo wa kuajiri lakini na mahitaji pia ya elimu. Lengo ni Walimu hawa wawe na vipindi vichache, wawe na urahisi wa maandalizi ya masomo yao na waweze kufundisha na kusimamia vizuri ili kumsaidia mtoto

kupata uelewa wa taaluma anayoipata kila siku mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali yake bado inaajiri na itaendelea kuajiri kuhakikisha kwamba kila shule inakuwa na Walimu wa kutosha kwa masomo yetu yaliyopo kwenye upande wa shule za msingi na sekondari vilevile. Lengo ni kuhakikisha kwamba, wanafunzi wetu wanapokwenda shuleni wakirudi jioni wawe wameshapata taaluma ya vipindi vyote ambavyo vimepangwa, tena kwa uelewa mpana kwa sababu Mwalimu anakuwa na nafasi nzuri ya kuweza kujiandaa. Huo ndiyo mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba ajira zinaendelea vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunafahamu kabisa shughuli ya usafirishaji ni moja kati ya sekta zinazotoa ajira nyingi kwa vijana, hasa bodaboda. Pia kumekuwa na tabia hii ya askari wetu wa Jeshi la Polisi kuwakimbiza vijana wetu wa bodaboda pale wanapovunja sheria za barabarani, hali inayosababisha ajali na vifo kwa bodaboda pamoja na abiria:-

Je, ni lini Serikali itatoa tamko kwa Jeshi la Polisi kuhusu namna nzuri ya udhibiti wa sheria hizi badala ya mfumo huu wa kuwakimbiza ili kupunguza idadi ya ajali na vifo kwa bodaboda na abiria? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvia, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bodaboda ni miongoni mwa vyombo vya usafiri vinavyotumia moto, kwa maana ya

mtambo ambao unatumia moto katika kuendesha chombo hicho. Vyombo vyote vya moto vimewekewa kwenye sheria katika uendeshaji wake. Kwanza kila dereva lazima awe na leseni; lakini pili, chombo hicho lazima kiwe na bima. Kwa chombo kama bodaboda dereva anatakiwa kuwa amevaa *helmet* ili aweze kuendesha. Hayo ni matakwu ya kisheria na wasimamizi wa sheria ni hawa makamanda wetu wa Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, sasa nimemsikia Mheshimiwa Mbunge akisema wanawakimbiza, sina uhakika sana na hilo la kukimbiza, lakini yapo matukio kwa kamanda mmoja mmoja, inategemea na mazingira hayo yaliyowafikisha katika kukimbizana, lakini hakuna utaratibu wa kuwakimbiza madereva hata pale ambapo wanatenda makosa. Tumeweka utaratibu wa makamanda kufanya ukaguzi na ili ufanye ukaguzi wanatoa alama ya kumsimamisha yule dereva ili ajiridhishe kama vigezo vyote hivi ameweza kuvifikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua watu wanaposimamishwa na makamanda wetu wengine wanapita. Sasa wanapopita hawa wanakuwa na mawasiliano na anapopita anajua anavunja sheria, kwa hiyo utakuta mtu anaongeza moto anakimbia akidhani anakimbizwa kumbe anakimbia mwenyewe halafu anapata ajali. Sasa hilo nalo pia halikubaliki sana kama imetokea mmoja akaamua kumkimbiza dereva, lakini muhimu zaidi tunahitaji madereva wote wanaoendesha vyombo vya moto kuzingatia sheria ambazo ziko na sisi Wabunge tumezitengeneza hapa na wasimamizi wetu ni hao askari polisi ambao ni trafiki.

Mheshimiwa Spika, muhimu zaidi tuendelee kutoa wito kwa waendesha bodaboda kuzingatia sheria. Serikali imeridhia bodaboda hii iwe chombo cha usafirishaji na ni fursa kwa vijana wetu kutumia kama sehemu ya mradi, kama biashara kusafirisha abiria hapa na pale; wazingatie sheria hizi ili wafanye kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumeweka utaratibu mzuri sana ambao hauhitaji vijana hawa wawe wanakurupushwa huko maeneo mbalimbali. Halmashauri zetu tumezipa maelekezo kuwakutanisha hawa vijana, kuwaandalia mazingira mazuri, kuwapa elimu na Jeshi la Polisi liko kulekule kwenye wilaya na lenyewe lihusike katika kuwapa elimu na kuona namna nzuri ya kuwahudumia ili wafanye kazi hiyo ya kusafirisha abiria na waendeleo kupata mitaji yao.

Nimeona katika halmashauri mbalimbali kupitia Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi, wakiita vikao vya madereva bodaboda kuwaanzishia umoja wao, kuwaelimisha namna ya kuendesha biashara zao ili kuondokana na hayo malalamiko yanayojitokeza ya askari kukimbizwa. Hata hivyo, pale ambapo inatokea polisi anamkimbiza bodaboda, huo siyo utaratibu, badala yake ni muhimu kuendelea kutoa elimu. Tunatoa agizo kwa maaskari wetu kuendelea kutoa elimu kwa vijana wetu wanaofanya biashara ya bodaboda na wote wako kwenye maeneo hayo ili tuwe na uelewa wa pamoja katika kutekeleza sheria hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi likitimiza wajibu wake wa kutoa elimu na kusimamia sheria, lakini hawa kwa sababu ni wengi na wengi wanaanza kujifunza na wanaingia kwenye biashara, wakipata hiyo elimu nao wazingatie haya ili kupunguza hizo ajali. Nadhani tukifanya hilo tutafika mahali pazuri pa kila mmoja kufanya kazi yake kwa weledi mkubwa; Jeshi la Polisi lifanye kazi yake, bodaboda afanye kazi yake, kila mmoja atimize wajibu wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Esther Matiko, uliza swali lako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, natambua Serikali ina mamlaka ya kutoa ardhi kutoka kwa wananchi kwa ajili ya matumizi mbadala kama vile ya uwekezaji au matumizi

mbalimbali kwa taasisi za umma na binafsi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, Sheria Na.4 Kifungu cha 3(i) na (g) kinatamka bayana kwamba pale mtwaaji anapochukua ardhi kutoka kwa wananchi lazima ahakikishe amefanya uthamini wa haki na ukamilifu, lakini zaidi ahakikishe analipa fidia kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na haya mazoea ya kufanya uthamini lakini inachukua muda mrefu sana kulipa fidia katika maeneo haya ambayo Watanzania wamechukuliwa ardhi zao, ili waweze kwenda sehemu zingine na kuweza kuanzisha makazi na kufanya shughuli za kijamii na uchumi:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujua, ni nini hatua ya Serikali kuhakikisha kwamba pale tathmini inapofanyika basi hawa wananchi wanalipwa fidia zao kwa wakati ili waweze kwenda kuendelea na shughuli za kiuchumi?  
*(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhali.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Mkoa wa Mara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunayo Sheria ya Ardhi na imetoa maelekezo kwa watumiaji wote. Kwa sera ya Serikali yetu nchini, ardhi ni mali ya Serikali na ni tofauti sana na maeneo mengine na kila mtumiaji wa ardhi hii ni lazima apate kibali, sisi tunaita hati, ile hati ni kibali cha matumizi ya ardhi ambacho kinaeleza umepewa ardhi hiyo kwa ajili ya nini? Mfano, kujenga nyumba; kiwanda au shamba, kile ni kibali cha Serikali kwa mtumiaji. Huo ndiyo utaratibu ambao tunao na ndiyo maana tunasisitiza kila aliyejenga nyumba, mwenye shamba, anataka kufanya biashara ya kiwanda, lazima apate hati, yaani apate kibali kutoka Serikalini.



Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ardhi hii ni ya Serikali, inaweza kuwa na mahitaji ya uendelezaji kwenye eneo ambalo tayari watu wapo, wanafanya kazi zao za kilimo yaani wanaendelea na maisha yao ya kawaida. Pale ambapo tunahitaji ardhi hiyo na hapo pana watu wanafanya shughuli zao, ili kuwatoa tunafanya uthamini. Katika zoezi la uthamini ni lazima uende kujua eneo hilo la ukubwa huo ambako mwananchi huyo yupo; kama alipanda mazao; mazao yote yamewekwa bei maalum ya uthamini; lakini pia kama amejenga nyumba, inafanyiwa uthamini na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali inapotaka kufanya jambo hilo, au yeyote anapotaka kutumia eneo hilo ambalo mwananchi yupo, suala la uthamini limezungumzwa pia na limesisitizwa na hili lazima lizingatiwe kwamba mtu anapotolewa eneo moja kupelekwa eneo lingine kwa lengo la kutumia eneo hilo iwe ni kwa uwekezaji au kufanya kazi nyingine, ni lazima uthamini uwepo. Najua yapo matatizo kadhaa katika maeneo mbalimbali, wengine huchukua ardhi bila fidia, wakati mwingine kunaweza kuwa na makubaliano, wakati mwingine wananchi wenyewe wanaamua kutoa ardhi ili shughuli muhimu ifanywe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge kama analo eneo ambalo kuna malalamiko na yanahitaji wananchi wa eneo hilo kupata haki yao stahiki, bado una fursa ya kuonana na viongozi wa eneo hilo waanze utaratibu wa kwenda kufanya uthaminishaji ili wananchi wote waweze kulipwa fidia yao kulingana na ukubwa wa ardhi na thamani ya mali zilizopo.

Kwa hiyo, hili limesisitizwa na linasimamiwa maeneo yote ili kila mmoja apate haki yake kulingana na ukubwa wa eneo lililoachwa kwa ajili ya shughuli hiyo mpya. Huo ndiyo utaratibu tulionao ndani ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunakushukuru sana kwa leo kwa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana sana sana. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mheshimiwa PM. Leo tulikuwa na wauliza maswali 16, lakini tumeweza kuwapata saba. Kwa hiyo, siyo neno, wengine *next time*. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali ya kawaida, swali la kwanza linaulizwa kuelekea Ofisi ya Mheshimiwa Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; na litaulizwa na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini.

Na. 103

**Hitaji la Vituo Vya Afya Newala**

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Newala ina Kata 22 na Vijiji 107, lakini ina Vituo vya Afya vitatu tu, kati ya 22 vinavyohitajika.

Je, Serikali haioni haja ya kujenga Vituo vipya vya Afya katika Halmashauri ya Newala ili kuboresha huduma za Afya kwa wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) kwa kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Kuanzia mwaka 2015 hadi Septemba 2020, Serikali imejenga Zahanati 1,198; imejenga na kukarabati Vituo vya Afya 487 na imejenga Hospitali za Halmashauri 102.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 na 2019/2020, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Newala kiasi cha Shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri na Shilingi milioni 400 kwa ajili kufanya ukarabati wa Kituo cha Afya Kitangari. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni moja (1) kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri na Shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma matatu ya Zahanati katika Halmashauri ya Wilaya ya Newala.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa awamu kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Nimekuona Mwuliza swali, Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda Njwayo. *(Kicheko)*

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Jimbo la Newala Vijijini linakabiliwa na uhaba mkubwa wa upatikanaji wa dawa kwa wananchi wake. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na suala hili? Uhaba ule unachangia kwa kiasi kikubwa sana wananchi kushindwa kujiunga na mpango wa CHF iliyoboreshwa kwa sababu wamekatishwa tamaa na mpango wa awali, wakienda vituoni hawapati dawa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Jimbo la Newala Vijijini linakabilishwa na uhaba mkubwa pia wa watumishi, hali ambayo inazorotesha utoaji wa huduma za afya kwa

wananchi. Ni lini Serikali itapeleka watumishi wa afya katika Jimbo la Newala Vijijini ili wananchi wale wapate huduma inayostahili kama wananchi wengine? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Naibu Waziri, Mheshimiwa Festo Dugange, tafadhali; uhaba wa watumishi na dawa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imeweka kipaumbele kuhakikisha vituo vyetu vya huduma kote nchini vinakuwa na dawa za kutosha. Ndiyo maana katika kipindi cha miaka mitano, bajeti ya dawa ya Serikali imeongezeka kutoka shilingi bilioni 31 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 271 mwaka 2020. Hii ni jitihada kubwa sana ya Serikali kuhakikisha wananchi wanapata dawa za kutosha vituoni.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuisitiza, kwanza kuhakikisha Halmashauri zinasimamia ipasavyo mapato ya uchangiaji wa huduma za afya katika vituo vyetu. Nasi Waheshimiwa Wabunge ni sehemu ya Madiwani katika Halmashauri zetu, kumekuwa na changamoto ya usimamizi wa makusanyo ya fedha za uchangiaji ili ziweze kuongeza mapato ya vituo na kuboresha dawa katika vituo vyetu. Serikali itaendelea kusimamia kwa karibu na kuboresha upatikanaji wa dawa nchini kote lakini katika Halmashauri ya Newala Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na uhaba wa watumishi, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele cha hali ya juu sana katika kuboresha upatikanaji wa watumishi katika vituo vyetu. Mipango iliyopo ni pamoja na kuendelea kuajiri na ushahidi unaonekana. Katika kipindi cha miaka mitano, zaidi ya watumishi 14,000 na mwaka jana madaktari 1,000 wameajiriwa katika vituo vyetu mbalimbali. Zoezi hili la kuajiri

watumishi wa afya ni endelevu na Serikali itaendelea kuajiri ili kuboresha huduma za afya katika nchi yetu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, naomba tuendelee na swali linalofuata la Mheshimiwa Grace Victor Tendega.

Na. 104

### **Serikali Kujenga Majengo ya Kusubiria Kujifungua Katika Vituo Vya Afya**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Akina mama wajawazito wamekuwa wakitozwa fedha kuanzia shilingi 50,000/= hadi 70,000/= wasipojifungulia katika Vituo vya Afya hasa katika Jimbo la Kalenga; huku vituo hivyo vikiwa mbali na maeneo wanayoishi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga maeneo ya kusubiri kujifungua katika Vituo vya Afya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, majengo ya wajawazito kujisubiria yanalenga kupunguza umbali kwa wajawazito kufika kwenye vituo vya huduma za afya pindi wanapokaribia kujifungua. Lengo likiwa ni kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga vinavyosababishwa na umbali kutoka katika vituo vya kutolea huduma.

Meshimiwa Spika, katika kutatua changamoto hii, Serikali imeendelea kujenga vituo vya huduma za afya kote nchini na kujenga Hospitali za Halmashauri 102, Vituo vya Afya 487 na Zahanati 1,198 katika kipindi cha Novemba, 2015 hadi Septemba, 2020. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 33.5 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali za Halmashauri 67; shilingi bilioni 33.5 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali 67 za Halmashauri na shilingi bilioni 27 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mpya za Halmashauri. Kiasi cha shilingi bilioni 27.5 pia kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha maboma ya Zahanati 555.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango wa ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya nchini kote, umepunguza umbali kwa wananchi kuvifikia vituo vya huduma za afya na hivyo viashiria vya huduma na vifo vya wajawazito vimepungua kutoka 11,000 mwaka 2015 hadi 3,000 mwaka 2020. Serikali itaendelea kujenga na ukarabati miundombinu ya huduma za afya kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni ahadi ya muda mrefu ya ujenzi wa sehemu za kujisubiria akina mama hasa wajawazito. Tumesema katika sera kwamba tutakuwa na Vituo vya Afya katika kila Kata na Zahanati katika kila kijiji; lakini katika Jimbo la Kalenga hii imekuwa ni changamoto kubwa sana. Akina mama wakijifungulia njiani wanatozwa Sh.50,000/= mpaka Sh.70,000/=. Ni lini Serikali itajenga majengo ya kujisubiria katika Jimbo hili la Kalenga? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, nini kauli ya Serikali kuhusu hizo tozo ambazo zinatozwa kwa akina mama ambao pia ni walipa kodi katika nchi hii na Serikali ndiyo yenye changamoto ya kutojenga hivyo Vituo vya Afya? (*Maikofi*)

**SPIKA:** Kule Kongwa haya maeneo ambayo akina mama wanasubiria yanaitwa Chigonela. Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Dkt. Dugange, Naibu Waziri wa TAMISEMI, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Grace Tendega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunahitaji kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga kwa kuboresha miundombinu ya huduma za afya. Ni kweli kwamba miradi ya ujenzi wa majengo ya kujisubiria kwa maana ya *maternity waiting homes*, imekuwa ni kipaumbele cha Serikali. Hata hivyo, majengo hayo yanajengwa ili kupunguza umbali wa wajawazito kufika kwenye Vituo vya Huduma za Afya. Kwa hiyo, ili ujenge majengo haya ni lazima uwe na Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Spika, sasa kupanga ni kuchagua. Ndiyo maana Serikali imepanga kwanza kujenga kwa wingi Vituo vya Afya ili viwe karibu zaidi na makazi ya wananchi na tuweze sasa, yale maeneo ambayo yana umbali mkubwa, kuweka mpango wa pili wa kuanza kujenga majengo ya kujisubiria wajawazito. Haitakuwa na tija sana ukiwekeza kujenga majengo ya kujisubiria wananchi sehemu ambayo ina umbali mkubwa sana kutoka kwenye vituo vya huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kipaumbele namba moja ni lazima uwe na kituo, ndiyo maana yale majengo yanajengwa karibu na kituo. Ndiyo maana katika miaka hii mitano tumejenga vituo vingi na tunaendelea na ujenzi wa vituo hivyo ili kusogeza huduma kwa wananchi, hatimaye tutakuja kujenga sasa majengo ya kusubiria wajawazito. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kipaumbele hicho bado kipo, lakini tunaboresha kwanza vituo na baadaye tutakenda kwenye awamu wa ujenzi wa majengo ya kujisubiria.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kauli ya Serikali kuhusu tozo, Serikali haijatoa maelekezo yoyote kwa watendaji na watoa huduma kutoza faini kwa wajawazito wanaojifungulia majumbani.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa watendaji katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ni wajibu wa watumishi katika vituo vya huduma kutoa elimu na kuhamasisha wajawazito kuona umuhimu wa kujifungulia katika vituo vya huduma badala ya kuwalipisha faini wakijifungulia nje ya vituo vya huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali itaendelea kusimamia jambo hilo. Naomba nitoe wito kwa watendaji wote kuzingatia jukumu lao la kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kujifungua katika vituo vya huduma.

**SPIKA:** Sasa hili swali niwape Wabunge wanaume au Wabunge wanawake?

**WABUNGE FULANI:** Wanawake. Haya *TWPG*, twende Tabora. (*Kicheko*)

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hospitali nyingi zinatoza wanawake wajawazito wanapokwenda kujifungua. Hospitali ya Kitete ni moja kati ya Hospitali ambazo zinatoka akina mama; anapojifungua mtoto wa kiumbe analipa Sh.50,000 na anapojifungua mtoto wa kike, analipa Sh.40,000. Je, Serikali imeweka tozo hii kwa ajili ya nini? (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, jambo hili lilitusumbua sana kwenye kampeni, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, naomba swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma za afya nchini unatolewa kwa mujibu wa sheria, sera na miongozo ikiwemo utoaji wa huduma za afya kwa wajawazito wakati wa kujifungua. Serikali imeelekeza bayana kwamba huduma za wajawazito na watoto wa chini ya umri wa miaka mitano zinatolewa bila malipo yoyote na Serikali inaendelea kusimamia utekelezaji wa sera na miongozo hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba baadhi ya maeneo, kwa baadhi ya watumishi wasio waaminifu, kwa namna moja ama nyingine wamekuwa wanatekeleza kinyume na sera na mwongozo huo. Kazi ya Serikali ni pamoja na kupokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niyachukue mawazo ya Mheshimiwa Mbunge na niwahikikishie kwamba tutaenda kuyafanyia kazi ili kuondokana na changamoto hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tuendeleo Waheshimiwa, tatizo hili ni kubwa sana hasa kwenye hospitali za Mikoa. Kule Tabora lilimsumbua sana Mheshimiwa Mwakasaka hili jambo. *(Kicheko/Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Abubakar Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero.

Na. 105

### **Kuongeza Uwekezaji wa Kiwanda cha Sukari Kilombero**

**MHE. ABUBAKAR D. ASENKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaongeza uwekezaji wa Kiwanda cha Sukari Kilombero ili kunusuru miwa ambayo haijavunwa kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaona kuna umuhimu wa kuongeza uzalishaji wa sukari nchini ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa sukari ambao umekuwa ukijitokeza mara kwa mara. Kwa msingi huo, hoja ya kuongeza uwekezaji katika Kiwanda cha Sukari cha Kilombero ni ya msingi sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imekuwa ikisimamia utendaji kazi wa Kiwanda hiki cha Sukari cha Kilombero kwa ukaribu kama inavyosimamia kampuni nyingine ambazo Serikali ina hisa chache kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370. Serikali pamoja na Mbia Mwenza (*Kilombero Holding Limited*) imekuwa kwenye majadiliano ya kina kuhusu kuongeza uzalishaji wa kiwanda hiki kwa kufanya upanuzi wa kiwanda ambapo imekubaliana kupitia gharama za upanuzi wa kiwanda, kufanya upembuzi yakinifu na namna ya ugharamiaji wa mradi. Mara baada ya zoezi hili kukamilika uwekezaji katika kiwanda hiki utafanyika haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa wewe ni miongoni mwa watu waliofika Jimboni kwetu na kuona namna ambavyo tunalima miwa kwa bidii kwa kufuata kauli ya Mheshimiwa Rais ya nchi kujitegemea katika suala zima la sukari; na kwa kuwa hao wenye viwanda ndio waliopewa vibali vya kuingiza sukari inayopungua katika nchi yetu, je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka mwekezaji mwingine wa kiwanda ili kuondoa *monopolism* ya kiwanda ambacho kipo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri na Mawaziri husika katika sekta hii ya kilimo na viwanda na biashara, watakuwa tayari kuambatana nami baada ya Bunge hili, kwenda kuwasikiliza wananchi hasa wakulima wa miwa Jimboni kwangu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abubakari, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, Serikali inaona umuhimu wa kuongeza uwekezaji wa viwanda vya sukari nchini hasa katika Kiwanda cha Kilombero ili kuongeza uzalishaji wa sukari nchini. Kwa upande wa Kiwanda cha Sukari cha Kilombero, Serikali na mbia mwenza, iko katika majadiliano ya kupanua kiwanda hiki na hatimaye kuongeza uzalishaji wa sukari ili miwa yote inayolimwa iweze kutumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, napenda kumwahidi Mheshimiwa Abubakari kwamba niko tayari kuongozana naye pamoja na wataalam wangu kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kujionea hali halisi ya uzalishaji katika kiwanda hicho, pale tutakapopata nafasi mara baada ya mkutano huu wa Bunge kuahirishwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Waziri, majibu ya nyongeza, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuongezea majibu kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba Serikali iko kwenye mazungumzo na wawekezaji kadhaa angalau watatu ambao wana nia ya kuwekeza katika kujenga viwanda vipya vya sukari. Naamini kwa mazungumzo hayo, tukiwapata tutapunguza sana tatizo la sukari na nia ya Serikali ni kuona kwamba katika mwaka

mmoja ujao tunajitosheleza kwa mahitaji ya sukari hapa nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba, wiki ijayo baada ya Bunge hili mimi na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tuna ziara katika Mkoa wa Morogoro na tutajitahidi tufike pia jimboni kwa Mheshimiwa ili kuweza kuona changamoto. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri na mimi nasisitiza mwende huko. Tulikuwa huko kwenye kampeni tunayajua mengi. Ni siasa kubwa na wananchi wanahangaika sana. Mtu analima miwa, hana mahali pa kuuza inakuwa ni usumbufu, kwa kweli kipatikane kiwanda kingine. Itasaidia. (Makofi)

Tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Na. 106

### **Uzalishaji wa Madini ya Niobium Wilaya ya Mbeya**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, ni lini uzalishaji wa madini ya *niobium* utaanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Profesa Shukurani Manya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa uchimbaji wa madini ya *niobium* katika Wilaya ya Mbeya unahusisha leseni tatu za uchimbaji wa kati na eneo hili lina jumla ya kilometa za mraba

22.1. Mradi huu unatarajiwa kuwa na uhai wa miaka 30 na unamilikiwa na Kampuni ya *Panda Hill Tanzania*, ambayo ni kwa ubia wa 50:50 na kampuni za *Cradle Resources Limited* na *Tremont Investments*. Mradi huu utahusisha uchimbaji wa madini ya *niobium* ambayo yataongezwa thamani nchini kwa kuchanganywa na madini ya chuma ili kuwa na mchanganyiko wa madini ya *FerroNiobium*, zao hili ndilo lenye soko katika nchi za Ulaya, Asia na Amerika ya Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, Mwekezaji aliwasilisha Wizarani maombi ya misamaha ya kodi katika uwekezaji wake. Mwekezaji alielekezwa na Wizara kufuata matakwa ya Sheria ya Madini ambayo ndiyo inayotumiwa na wawekezaji wengine wote katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa mwekezaji kukamilisha taratibu za kumwezesha kuanza utekelezaji wa mradi ikiwepo pia kupata ridhaa ya maandishi kutoka kwa wamiliki wa maeneo katika leseni zake kama ilivyo Sheria ya Madini. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Njenza, swali la nyongeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nashukuru vile vile kwa majibu ya Serikali ambayo yanaleta matumaini sasa kwa matumizi ya chuma na matumizi ya *niobium* na kuwepo kwa kiwanda cha *FerroNiobium* hapa hapa kwetu nchini. Swali la kwanza, je, sasa kwa vile haya madini inaonesha kuwa ni madini ya viwandani ambayo yatachanganywa pamoja na chuma na ikiwezekena pamoja na *aluminium*, ni lini sasa Serikali itahakikisha kuwa uzalishaji wa chuma ikiwemo machimbo ya Liganga na Mchuchuma yataanza mara moja ili yaweze kutengenezwa *FerroNiobium* hapa hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa sababu haya madini yanatengeneza *FerroNiobium*, je, viwanda vya *FerroNiobium* vinaangukia kwenye Sheria za Uwekezaji za EPZ? Nashukuru.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Profesa Shukurani Manya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nipende kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba madini ya *Niobium* yatachanganywa pamoja na madini ya chuma ili kutengeneza muunganiko huu wa *FerroNiobium* na ni kweli kwamba Serikali kwa sasa iko katika mazungumzo rasmi na mwekezaji anayewekeza katika Mradi wa Liganga ili hatimaye tuweze kuanza mradi huo kwa sababu umechelewa sana. Kwa hiyo napenda kuamini kwamba maongezi haya yatakapokuwa yamekamilika baina ya mwekezaji wa Liganga na suala likiwa hasa katika mikataba, basi mtanzuko huo utakapokuwa umeondoka tunapenda kuamini kwamba itakuwa ni fursa ya kuendeleza mradi wa *Niobium* ambayo itachanganywa na chuma chetu cha Liganga.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, ni kweli kwamba madini mengine yana matumizi katika viwanda na pia ndiyo iliyokuwa ni *sticking point* katika mazungumzo yetu na mwekezaji. Sasa ukiangalia madini ya *Niobium* katika *periodic table* ni *transition metals*, kwa hiyo tunapaswa tuyatambue kwamba ni madini ya metali na ukiyabadilisha yakaonekana kwamba kwa vile yana matumizi katika viwanda tozo inayotozwa ya *royalty* madini ya viwanda ni asilimia tatu, madini ya metali ni asilimia sita.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hapa napo tulikuwa na mkinzano na mwekezaji kwamba matumizi ya baadaye yasisababishie tukaanza kuonesha kwamba hayako katika *group* la metali, kwa sababu hata dhahabu nayo pamoja na kwamba ni metali inaweza ikapata matumizi katika viwanda. Kwa hiyo tukaona kwamba hebu tuendeleo kuuangalia upande wa kwamba madini ya *niobium* ni madini ya metali, *royalty* yake ibakie kuwa asilimia sita hata kama

baada ya hapo itakuja kuchanganywa na kuwa *FerroNiobium*. Kwa hiyo hayo ni maongezi ambayo tumeongea na mwekezaji na tunaamini kwamba tutafikia muafaka. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. *Engineer* Hhayuma.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, lakini naomba uniwie radhi. Nilikuwa nimelenga swali namba 103.

**SPIKA:** Nakushukuru sana. Tunaendelea na swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki.

Na. 107

### **Kufanya Utafiti wa Madini – Manyoni Mashariki**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti ili kubaini uwepo wa aina mbalimbali za madini katika Jimbo la Manyoni Mashariki hususan Kata za Sasilo, Makuru, Kintinku na Solya?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, bado tuko Wizara ya Madini, Mheshimiwa Profesa Shukurani Manya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Taasisi yetu ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*Geological Survey of Tanzania - GST*) kwa nyakati tofauti imefanya utafiti wa awali, nisisitize tu utafiti wa awali katika maeneo mbalimbali nchini

Tanzania zikiwemo Kata za Makuru, Solya, Kintinku na Sasilo ambako ndiko Mheshimiwa Mbunge anatoka.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya tafiti za awali zilizofanyika katika maeneo hayo zinaonesha kuwa kuna viashiria vya uwepo wa madini kama ifuatavyo:-

(a) Katika Kata ya Makuru – kuna dhahabu kidogo pamoja na ulanga (*nickel*);

(b) Katika Kata ya Solya – Kuna urani, *thorium* na madini ya ujenzi;

(c) Katika Kata ya Kintinku – kuna Urani; na

(d) Katika Kata ya Sasilo – kwa utafiti uliofanyika hakukuonekana kwamba kuna viashiria vya uwepo wa madini.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha uchimbaji kufanyika, mara nyingi sana tafiti za kina zinahitajika ili kujiridhisha na kiwango cha mashapo iwapo yanaweza kuchimbwa kwa faida au la.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Madini. Nina maswali mawili ya nyongeza. Wewe mwenyewe unatambua kwamba Sekta ya Madini ina mchango mkubwa sana kwenye kukuza ajira kipato na Pato la Taifa. Swali la kwanza, je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuja na utafiti wa kina ili tuweze kuibua taarifa za kijiolojia zitakayoaidia Serikali kuwekeza kwenye mambo ya madini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa tayari Naibu Waziri amesema kuna Taarifa za awali kwenye baadhi ya maeneo ikiwemo Kata ya Makuru, katika Kijiji cha Londoni



ambako tayari wachimbaji wa madini wadogo wadogo wanachimba. Sasa, je Serikali imejipanga vipi kuwawezesha wananchi katika maeneo ambayo kuna taarifa za awali ili waweze kujikita kwenye uchimbaji wa madini, tukuze ajira na kipato cha nchi? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Profesa Manya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nipende kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Jimbo la Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba utafiti wa kina ndilo jawabu la hatimate kuwawezesha uchimbaji kufanyika. Sasa mojawapo ya mabadiliko ya Sheria ya Madini ambayo yanaonesha tumaini na huko mbele ni pamoja na kuziwezesha Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Madini kwa rasilimali ili ziweze kufanya majukumu yake ipasavyo. Ni katika mtindo huo huo kwamba Taasisi ya Utafiti wa Jiolojia ya Madini - *GST* imepokea vifaa rasilimali kama wiki mbili zilizopita tulipata magari sita kwa ajili ya kuwawezesha kufanya ugani.

Mheshimiwa Spika, pia *STAMICO* wamewezeshwa na wao wenyewe kwa pato lao la ndani wamepata mitambo mitatu ya *drilling*. Sasa hizo ni hatua za kuimarisha Taasisi ili hatimaye ziweze kufanya kazi ya utafiti wa kina na hatimaye kuwasaidia wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu swali lake la pili linauliza ni lini watawezesha; ni katika mtindo huo wa kwamba tutakapokuwa tumeendelea zaidi kuimarisha taasisi zetu kwa uwezo wa kifedha kama ambavyo Serikali imeanza kufanya tunapenda kuamini kwamba tunaelekea mahali ambapo Taasisi ya Jiolojia inaweza ikashirikiana na *STAMICO* na hatimaye wakawa wanafanya utafiti wa kina mahali fulani na kwa utafiti huo sasa wakapewa wachimbaji wadogo ili waweze kufanya kazi zao kwa tija. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tuendelee na Elimu Sayansi na Teknolojia. Swali litaulizwa na Mheshimiwa Mwanaisha Ng’anzi Ulenge. Mheshimiwa Mwanaisha, tafadhali.

Na.108

**Mitaala ya Vyuo vya Uhandisi Nchini Kuendana na  
Mitaala ya Bara la Asia**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Miradi mikubwa ya ujenzi nchini inafanywa na kampuni kutoka Bara la Asia wakati wahandisi nchini wanasoma uhandisi kwa mitaala ya Uingereza na Marekani.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuongeza mitaala ya Asia katika mitaala ya Vyuo vya Uhandisi ili Wahandisi wetu wapate utalam katika miradi ya ujenzi?

(b) Je, suala la kubadilishana weledi limepewa kipaumbele gani katika miradi inayoendelea kujengwa hapa nchini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo toka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Omari Kipanga, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng’anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Uhandisi ni fani ya Kimataifa ambayo mitaala yake haitofautiani kijiografia. Kwa muktadha huo mitaala ya shahada za uhandisi katika vyuo vyetu nchini nayo ni ya viwango vya kimataifa. Hata hivyo, ni kawaida

kuhuisha mitaala mara kwa mara ili kuingiza utaalum mpya kwenye fani. Hivyo basi ni nia ya Serikali yetu kuhuisha (*review and update*) ya mitaala ya kihandisi na fani nyingine za kipaumbele kwenye Tanzania ya viwanda kama tunavyoongozwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025, Ibara ya 80 Ukurasa 130 Kipengele (c) ambayo inaagiza " kuhuisha Mitaala (*curriculum review*) na kuanzisha programu kulingana na mahitaji ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili wahitimu wawe na stadi stahiki za kumudu kufanya kazi mbalimbali za kuajiriwa na kujajiri na hasa kwa kuzingatia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda".

(b) Mheshimiwa Spika, suala la kubadilishana uweledi wa kihandisi kati ya miradi mikubwa inayoendelea tayari linatekelezwa ambapo wahitimu wetu wa uhandisi hupata nafasi za utarajali katika miradi yetu mikubwa ya Kitaifa ili kupata weledi. Kwa mfano, kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi (*Engineers Registration Board*) wapo wahandisi wahitimu 197 ambao wanashiriki kwa sasa katika miradi mikubwa mbalimbali mfano Mradi Umeme wa Mwalimu Nyerere na Mradi wa Reli ya Mwendu Kasi. Hivyo, Serikali itaendelea kuweka mfumo wa kuhakikisha kuwa katika miradi mikubwa inayotekelezwa nchini suala la kubadilishana uweledi linaendelea kupewa kipaumbele. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanaisha.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati mimi nilipokuwa nasoma chuo tulikuwa tunapata ziara za mafunzo (*study tours*) mara kwa mara kwenye maeneo ambayo kazi zilikuwa zinatendwa kwa vitendo. Hata hivyo, utaratibu huo ulikoma na tukabakiwa tu na utaratibu wa mafunzo viwandani (*industrial practical training*) sasa ili kuzalisha vijana mahiri, wabunifu na wenye uwezo wa kuhamisha maarifa ya kisayansi katika uzalishaji. Je, Serikali haioni haja ya kuongeza utaratibu wa

*study tours* pamoja na huu uliopo wa mafunzo viwandani?  
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, niishukuru Serikali na niipongeze kwa kutambua mchango wa wataalam wanawake wa kisayansi mpaka wameamua kupanga kujenga shule za masomo ya kisayansi kila mkoa. Je, Serikali inaweka utaratibu gani sasa kuhakikisha wasichana waliofaulu vizuri masomo ya sayansi wanapata mikopo na fursa nyingine za elimu ya juu bila kuhangaika na usumbufu wowote kama ambavyo imetoa hivi karibuni?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo ya nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Omari Kipanga, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ulenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika utaratibu wa kawaida vyuoni tunakuwa na program zile za *practical training* baada ya kumaliza mwaka husika wa masomo, lakini tumekuwa na utaratibu wa zamani ule wa kufanya *study trip*. Hata hivyo, kutokana na uhaba wa bajeti program hizi zilisimama.

Naomba kulithibitishia Bunge lako tukufu, hivi sasa tunakwenda kuimarisha na kuboresha bajeti yetu katika maeneo haya ya elimu, *especially*, katika vyo vikiu na utaratibu huu sasa wa hizi *study tour* unaweza ukarejea.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la pili ambalo ni wasichana; kama mnavyofahamu Mheshimiwa Rais wakati anahutubia Bunge hili alizungumza hapa kwamba tunakwenda kujenga shule 26 katika kila mkoa kwa lengo la kuhakikisha kwamba wasichana wanakwenda kupata *study* za masomo ya sayansi katika maeneo haya. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba wasichana hawa pindi watakapomaliza masomo yao haya tunakwenda kuwa-

*absorb* kwenye vyuo ili sasa tuweze kupata wataalam wasichana na wanawake wengi katika masomo haya ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kipaumbele chetu kama Serikali na katika mikopo yetu ya elimu ya juu tutahakikisha kwamba masomo haya ya sayansi yanapewa kipaumbele, hasa kwa wasichana wetu hapa nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana na sisi Bunge tumekuwa mfano tulipojenga shule yetu ya *Bunge Girls* ambayo kuna wasichana wanaosoma *PCM, PCB, CBG* na *EGM*. Hongereni sana *TWPG*. (*Makofi*)

Tutafanya utaratibu Waheshimiwa Wabunge wote akina mama ama mwishoni mwa Bunge hili au lijalo muweze kutembelea shule yetu hiyo na kuiona na kuzungumza na watoto hawa wa kike.

Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, uliza swali lako.

Na. 109

**Elimu Bure toka Shule za Msingi, Kidato cha Tano na Sita**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukamilisha dhana ya elimu bure kwa kutoa elimu bure kuanzia Shule ya Msingi hadi Kidato cha Tano na cha Sita?

**SPIKA:** Majibu ya swali namba 109. Bado tuko elimu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Omari Kipanga, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dhana ya utoaji Elimu Msingi Bila Malipo inamaanisha kuwa mwanafunzi atasoma bila mzazi au mlezi kulipa ada wala michango ya fedha iliyokuwa inatozwa shuleni kabla ya kutolewa kwa Waraka wa Elimu Na. 5 wa mwaka 2015. Gharama hizo zote ambazo mzazi au mlezi alitakiwa kutoa kwa sasa hulipwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, dhana ya Elimu Bila Malipo inalenga elimu msingi. Elimu hii inaanzia Elimu ya Awali hadi Elimu ya Sekondari, Kidato cha Nne ili kuwajengea watoto wa Kitanzania misingi imara ya masomo ngazi zinazofuata na ustawi wa maisha yao kwa ujumla. Elimu ya kidato cha tano na sita nchini hutolewa kwa ushirikiano kati ya wazazi/walezi na Serikali. Wazazi au walezi hutakiwa kuchangia ada ya shilingi 70,000 kwa wanafunzi wa shule za bweni na shilingi 20,000 kwa wanafunzi wa shule za kutwa kwa mwaka. Serikali hugharamia gharama nyingine zilizobaki kama vile mishahara ya walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa mfano vitabu na vifaa vya maabara pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere, swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika swali langu la msingi nimesema kwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi nzuri ya kutoa elimu bure katika shule za msingi mpaka sekondari; na kwa kuwa Waraka wa Serikali Namba 5 wa 2015 unasema, elimu bure ni kutoka shule ya msingi mpaka sekondari; na kwa kuwa kidato cha tano na kidato cha sita ni sekondari, ni kitu gani kinazuia Serikali kutoa elimu

bure kwa kidato cha tano na cha sita kwa sababu ni sekondari hiyohiyo ambayo inazungumzwa?

Mheshimiwa Spika, umesikia Wabunge wengi wanasema hapa, Mheshimiwa Oliver, Mheshimiwa Sanga na wengine kwamba imetajwa katika Waraka kwamba elimu bure ni shule ya msingi mpaka sekondari, kidato cha tano na cha sita ni sekondari. Sasa ni lini Serikali itatoa elimu bure kwa kidato cha tano na cha sita?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, tumezungumza humu mara nyingi sana na hili swali naliuliza kama mara ya tano sasa, Shule ya Sekondari za Unyali, Mkomalilo, Mihingo, Esparanto, Makongoro, Wamamta, Salama, hazina walimu wa sayansi. Watu wanachanga, tumejenga majengo mazuri watoto wanasoma lakini hawana walimu. Lini Serikali itapeleka walimu kwenye shule hizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu; *form five* na *form six* kwa nini nao wasisome bure? Walimu wa sayansi hamna, hata Kongwa hakuna.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Waraka Namba 5 wa mwaka 2015 wa Elimu Msingi, unaelekeza kwamba itakuwa elimu bure kuanzia elimu ya awali mpaka kidato cha nne. Mheshimiwa Mbunge anauliza kwa nini kidato cha tano na cha sita hakipo katika mpango huo. Ni kweli, kidato cha tano na cha sita hakipo kwenye mpango huu lakini naomba nilieleze Bunge lako tukufu kuwa tunaendelea kuboresha bajeti yetu ya Serikali, mpango huu unaweza kufikiwa iwapo tu bajeti ya Serikali itakuwa imekaa sawasawa.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu, baada ya kupata fursa hii ya kutoa elimu bure usajili wetu wa wanafunzi, tuchukulie mfano wa darasa la kwanza, umeweza kuongezeka kutoka wanafunzi 1,300,000 mwaka 2014 mpaka

wanafunzi 2,070,000 mwaka 2016/2017. Utaona kuna ongezeko hilo kubwa kutokana na Sera hii ya Elimu Bure. Kwa hiyo, upatikanaji wa fedha utatupeleka kuhakikisha kwamba kidato cha tano na cha sita tunawaingiza katika mpango huu.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika napenda kueleza kwa zile kaya ambazo ni maskini tuna mpango wetu wa *TASAF* ambapo kwa mwanafunzi wa shule ya msingi anapata shilingi 12,000/= kwa mwezi na wale wa sekondari wanapata shilingi 16,000/= kwa mwezi. Hawa wanaweza wakasaidiwa katika mpango huu ili kuhakikisha kwamba tunaweza kufikia yale malengo ya kulipi hiyo ada ndogo ambayo inalipwa katika kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili, shule alizozitaja na hasa kuhusu wale walimu wa sayansi, Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa ametoka kujibu swali kama hilo katika kipindi kifupi kilichopita, Serikali tayari imeshaanza mpango wa kuajiri walimu. Katika mwaka 2020 tumeajiri zaidi ya walimu 8,000 wameshapelekwa shuleni. Sasa hivi Serikali iko kwenye mchakato wa kuajiri tena walimu 5,000 ambao katika kipindi kifupi kijacho tunaamini shule hizi alizozitaja zinaweza zikapata hao walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu. Nilikuona Mheshimiwa Mrisho Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, Mkoani Arusha kuna shule ya *St. Jude*, ni shule ambayo inasomesha watoto wenye mazingira magumu na kwa kupitia misaada ya watu mbalimbali huko duniani. Siku za karibuni *TRA* imeenda kwenye *account* ya shule hiyo imechukua fedha na kusababisha shule hiyo kupata misukosuko na kufungwa kiasi ambacho watoto wenye mazingira magumu wamekosa nafasi ya kwenda kusoma pamoja. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ahueni kwa shule hii ili suala la elimu ambayo ni kipaumbele chetu liweze kupewa mstari wa mbele?



**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, majibu ya swali hilo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Arusha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyobainisha uwepo wa shule hiyo na changamoto zilizotokea kuhusiana na wenzetu wa *TRA*, suala hili naomba tulichukue twende tukalifanyie kazi na badaye tutaweza kutoa majibu muafaka kwa Mheshimiwa Mbunge na Mkoa wa Arusha kwa ujumla. Ahsante.

**SPIKA:** Hiyo ni ahadi ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri tutaomba itekelezwe. Napenda kupata nakala ya majibu hayo yatakapokuwa tayari. Nasema hivyo kwa sababu ni hatima ya watoto wa maskini, kwa hiyo, tungependa kujua hatima ya jambo hilo ili tujiridhishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu maswali amezungumzia neno elimu bure, lakini najua anajua tofauti kati ya elimu bure na elimu bila kulipa ada. Nazungumza hivi kwa sababu kinachofanyika mashuleni huko wanafunzi na wazazi wanatozwa fedha ama za kulipa mlinzi ama za kulipa maji ama za kulipa walimu wa sayansi ambao wanawatafuta wa ziada ama masomo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka Serikali iweke hoja wazi kabisa hapa mezani, kinachofanyika ni elimu bila kulipa ile ada ya Sh.20,000 na Sh.70,000 na siyo elimu bure, ili wazazi wanapochangia huko wajue kwamba wao kwenye mchakato wa elimu ya Tanzania wana-*stake* yao ya kuchangia na Serikali ina *stake* yake ya kuchangia. Kwa hiyo, aweke wazi hapa ni elimu bila ada na sio elimu bure. Sasa kwa tafsiri ya kamusi bure ina maana yake na ada ina maana yake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana umeeleweka Mheshimiwa. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu; elimu bure au elimu bila ada?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu yangu ya msingi, Waraka Namba 5 wa mwaka 2015 ulikuwa unaeleza kwamba elimu bila malipo kwa elimu ya awali mpaka kidato cha nne.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna michango ambayo huenda ikawa inatokea huko ambayo ni michango ya hiari...

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hiyo, ni elimu bila malipo siyo elimu bure.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, elimu bila malipo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nisikuwekee maneno mdomoni Mheshimiwa Naibu Waziri, nilitaka tu uweke vizuri, hebu rudia wewe mwenyewe.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumzia Waraka Namba 5 wa mwaka 2015 unaeleza kwamba elimu ya awali mpaka elimu ya kidato cha nne itakuwa ni elimu bila malipo, tafsiri yake ni elimu bure. Kwa hiyo, waraka huo unaeleza hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huo, amezungumzia kwamba kuna michango wazazi wanachangishwa ya walinzi, usafi au ya vitu vingine, naomba nilieleze Bunge lako Tukufu kuwa Serikali katika Waraka ule imebainisha wazi kwamba michango ile yote ambayo mzazi alikuwa anachangia katika kipindi cha nyuma katika maeneo haya ya elimu ya awali kwa hivi sasa haipo na gharama hizo zinakwenda Serikalini. Sambamba na hilo,

nadhani keshawahi kusikika Mheshimiwa Waziri wa Elimu lakini Mheshimiwa Rais ameshawahi kuzungumza mara nyingi sana, kama mzazi au mlezi ana mchango wa aina yoyote ambao anaona bora au inafaa mchango huo autoe ni vema aufikishe au auwasilishe kwa Mkurugenzi ambapo yeye atapanga kitu gani cha kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaenda Wizara ya Maji Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Issa Ali Mchungahela, Mbunge wa Lulindi.

Na. 110

### **Mradi wa Maji wa Chipingo – Jimbo la Lulindi**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA** aliuliza:-

Mradi wa maji wa Chipingo uliopo katika Jimbo la Lulindi ambao umegharimu Shilingi Bilioni 3.9 ni wa muda mrefu tangu mwaka 2013, lakini umekuwa hauna tija kwa kuwa hautoi maji; mabomba kupasuka mara kwa mara na mpaka sasa bado haujakabidhiwa kwa Serikali:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya mradi huo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la maji, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. Mheshimiwa *Engineer* Maryprisca Mahundi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Jimbo la Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Chipingo upo katika Jimbo la Lulindi, Wilaya ya Masasi. Mradi huu ulianza kujengwa Aprili, 2013 na ni miongoni mwa miradi ambayo

haikukamilika kwa wakati kulingana na mkataba. Katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi, Serikali ya Awamu ya Tano imefanya jitihada za kukamilisha mradi huu na hivi sasa mradi huo unatoa maji na upo katika hatua za majaribio ambapo vijiji 6 kati ya 8 ambavyo ni Manyuli, Chipingo, Mnavira, Chikolopora, Namnyonyo na Mkaliwala vinanufaika.

Mheshimiwa Spika, Vijiji viwili vya Rahaleo na Mapiri vya mradi huo bado havijaanza kupata huduma ya maji ambapo ujenzi wa mtandao wa maji kwa ajili ya vijiji hivyo unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Machi, 2021.

Aidha, kuhusu suala la upasukaji wa mabomba katika kipande cha bomba kuu chenye urefu wa kilomita 1.2, Serikali inaendelea kusimamia maboresho yanayofanywa na mkandarasi kipindi hiki cha majaribio ya mradi ili wananchi waweze kupata huduma ya maji kama ilivyokusudiwa. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 90.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Lulindi, swali la nyongeza, tafadhali.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Spika, ninayo maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikipoteza pesa nyingi sana, hasa kwenye miradi na miradi ya maji ikiwapo hasa huu mradi wa Chipingo. Hii imetokea mara nyingi kutokana na watendaji ambao sio waaminifu wakishirikiana na wakandarasi kuhujumu Taifa kwa kutotimiza majukumu ya mikataba yao. Je, Serikali ina tamko gani kuhusiana na suala hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, sina shaka na utendaji wa Wizara hii; Mheshimiwa Aweso pamoja na timu yake wanachapa kazi sana lakini wale watendaji wenu kule wanawaangusha. Je, Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri anakubali kuambatana na mimi kwenda kuangalia hali halisi

mkajiridhisha kisha mkatatua changamoto hii kwa umakini kabisa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa mnaotaka kuambatana na Mawaziri inabidi mniletee majina yenu wote, ili nipange ratiba kadiri inavyofaa kwa kumshirikisha Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Maryprisca Mahundi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge Issa Mchungahela kutoka Jimbo la Lulindi, kama ifauatvyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa sasa hivi tumekuwa tukifanya jitihada za kuona kwamba watendaji wanaendana na kasi ya hitaji la Wizara yetu kwa sababu, madeni yote na miradi ambayo imekuwa ya muda mrefu awamu hii tunaelekea kuikamilisha.

Mheshimiwa Spika, hivyo, napenda kumtoa hofu Mheshimiwa Mbunge kwa hawa watendaji ambao wanakiuka maadili yao ya kazi na kuweza kuwa wahujumu katika shughuli zao tayari tunawashughulikia na tayari tuna mkeka mpya wa Wahandisi ambao wanashindwa kutekeleza majukumu yao kadiri ambavyo tunahitaji watuvushe.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusiana na suala la kuambatana, Mheshimiwa Mbunge aondoe hofu. Hiyo ndiyo moja ya majukumu yangu na ninamhakikishia baada ya kukamilisha ziara yangu kwenye maeneo mengine, basi na hata huko Masasi pia nitakuja na nitajitahidi kufika kwenye majimbo yote kuona suala la maji linakwenda kupata muarobaini.

**SPIKA:** Huko Lulindi mbali huko. (*Kicheko*)

Tunakwenda Mambo ya Ndani ya Nchi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Agneta Lambert Kaiza.

Na. 111

## Ucheleweshaji wa Kupandisha Vyeo kwa Askari Polisi

**MHE. AGNESTA L. KAIZA** aliuliza:-

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu ucheleweshaji wa kupandisha vyeo kwa Askari wa Jeshi la Polisi katika ngazi ya Wakaguzi Wasaidizi na kwa Wakaguzi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agneta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi ni Taasisi ya Serikali ambayo mfumo wake wa upandishwaji wa vyeo huzingatia sheria na kanuni za utumishi. Askari, Wakaguzi na Wakaguzi Wasaidizi wa Jeshi la Polisi hupandishwa vyeo pamoja na watendaji wengine wa Jeshi la Polisi kwa kuzingatia ikama na bajeti ya mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2015 mpaka 2018 jumla ya askari 2,354 walipandishwa vyeo kuwa Wakaguzi Wasaidizi na kwa kipindi cha kuanzia 2015 mpaka 2020 jumla ya Wakaguzi Wasaidizi 1,163 walipandishwa vyeo kuwa Wakaguzi wa Polisi. Serikali itaendelea kuwapandisha vyeo Askari Wakaguzi na Maofisa mbalimbali wa Jeshi la Polisi kulingana na taratibu zilizoelzwa hapo awali. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agneta inabidi u-*declare intetest* wewe ni njagu au? Mheshimiwa uliza swali la nyongeza. (Kicheko)

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu na takwimu zilizotolewa na Serikali, ukweli ni kwamba kutoka ngazi ya Mkaguzi Msaidizi kwenda Mkaguzi kamili inapaswa kufanyika ndani ya mwaka mmoja mpaka miaka miwili. Je, Mheshimiwa Waziri anayo taarifa kwamba kuanzia mwaka 2015 mpaka muda huu ambapo nimesimama mbele ya Bunge hili Tukufu kuna Wakaguzi Wasaidizi ambao hawajapandishwa madaraja?

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Mheshimiwa Waziri atueleze hapa ikiwa anazo hizo taarifa ni kwa nini basi hao Wakaguzi hawajapandishwa madaraja?

**SPIKA:** Ahsante sana. Hayo ni maswali mawili tayari Mheshimiwa Agnesta. Swali la kwanza una taarifa na la pili kwa nini hawajapandishwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba tangu 2015 mpaka hapa tulipo watu hawajapandishwa madaraja. Kama ataangalia kwenye jibu langu la msingi nilitoa takwimu ambazo zinaonyesha kwamba kuna watu walipandishwa madaraja.

Mheshimiwa Spika, kingine nimfahamishe tu Mheshimiwa kwamba ni vizuri wakapata nafasi wakaipitia hii *PGO (Police General Order)* itawasaidia kujua baadhi ya taratibu ambazo zinatumiwa kupandisha madaraja. Kuna mambo ya msingi huwa yanaangaliwa, siyo kwamba watu wanapandishwa tu kwa sababu hawajapandishwa muda mrefu. Kwanza, lazima kipatikane kibali cha kupandisha majaraja. Pili, tunaangalia pia uwezo wa kiuongozi wa yule

ambaye anatakiwa kupandishwa daraja. Tatu, tunazingatia zaidi vigezo vya kimaadili kwamba tunayekwenda kumpandisha cheo ana maadili gani katika kutumikia Taifa hili. Nne, tunaangalia kama hana mashtaka mengine. Tano, huwa tunaangalia na bajeti maana tukimpandisha cheo lazima tumpandishie na mshahara wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa afahamu kwamba utaratibu ndiyo huo lakini tumeanza na tumepandisha madaraja mbalimbali kwa watumishi wa Jeshi la Polisi kama ambavyo taratibu zimeeleza.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na swali la Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete.

Na. 112

### **Ahadi ya Ujenzi Daraja la Mto Mbaka**

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Daraja la Mto Mbaka linalounganisha Jimbo la Busokelo na Rungwe litakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Daraja la Mto Mbaka ambalo lipo katika barabara ya Katumba - Lwangwa - Tukuyu yenye jumla ya kilometa 81, linaunganisha Halmashauri ya Busokelo na Mji wa Tukuyu. Barabara hiyo ni ya mkoa na inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

Mheshimiwa Spika, hapo awali daraja hili lilikuwa la chuma (*Bailey*) lakini kwa kuzingatia umuhimu wa daraja hilo lililopo kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao



ya kilimo na mazao ya misitu, Serikali iliamua kulijenga kwa kiwango cha zege kuanzia mwaka 2018. Hata hivyo, wakati ujenzi ukiendelea kulijitokeza changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na usanifu ambao ilibidi urudiwe kuendana na hali halisi ya eneo husika. Usanifu huo ulikamilika mwezi Oktoba, 2019.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mkandarasi anaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa daraja hilo ambapo kazi za ujenzi zimefikia asilimia 68 na kazi zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Atupele.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali nataka kufahamu ni hatua gani za kinidhamu zinazoweza kuchukuliwa na Serikali kwa wataalam wetu wanaosababisha *variation* ya miradi kuwa na gharama kubwa, kwa mfano, daraja hili la Mbaka ambalo limechukua muda mrefu sana. Kuna kitu tunaita *geotechnical investigation* hakikufanyika na ndiyo maana imechukua muda mrefu zaidi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa daraja hili litakapokamilika kutakuwa kuna madaraja mawili, kutakuwa kuna daraja hili ambalo linajengwa pamoja na lililokuwepo la chuma.

Je, Serikali ipo tayari kulichukua hili daraja la chuma kupeleka katika mto huo huo Mbaka lakini kwa kuweza kuunganisha kati ya Majimbo ya Busokelo, Kyela pamoja na Rungwe katika Kijiji cha Nsanga? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa *Engineer Msongwe*, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tayari ni utaratibu wa Serikali pale ambapo mfanyakazi yeyote amefanya kinyume na utaratibu anachukuliwa hatua na kwa sababu umakini huo ndiyo maana ilionekana kwamba daraja hili lilikosewa *design* na ikafanyiwa *redesign* na tayari ujenzi unaendelea kwa hiyo ni utaratibu wa kawaida pale panapotokea tatizo hatua zinachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, anauliza endapo daraja la chuma lililokuwepo litakwenda kwenye daraja lingine alilolisema ni utaratibu wa Serikali kwamba madaraja haya ya chuma ni madaraja ambayo yanatumika kwa ajili hasa ya dharura. Kwa hiyo utaratibu utawekwa kama itaonekana ni muhimu liende hapo litakwenda lakini vinginevyo tunayatunza maeneo ambayo ni ya kimkakati ili kunapotokea tatizo la dharura basi hayo madaraja yatakwenda hapo. Ahsante.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo litaulizwa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba na kwa niaba yake Mheshimiwa Nape Nnauye, nimekuona.

Na. 113

### **Barabara ya Kuunganisha Mkoa wa Njombe na Morogoro**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliuliza:

Serikali ina mpango wa kuunganisha mikoa yote kwa mtandao wa barabara za lami, ikiwemo barabara yenye urefu wa kilometa 223 inayounganisha Mikoa ya Njombe na Morogoro kupitia Mlimba ambayo pia iko katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara hiyo?

**SPIKA:** Bado tuko Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge ni Barabara ya Ifakara – Mlimba – Taweta – Madeke yenye urefu wa kilometa 220.22 ambayo ni barabara ya mkoa inayosimamiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*).

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya kutoka Ifakara hadi Kihansi (kilometa 126) ili kuunganisha na kipande cha barabara ya lami (kilometa 24) kilichojengwa hapo awali kati ya Kihansi na Mlimba.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu iliyosalia kati ya Kihansi na Madeke (kilometa 94.2) umepangwa kufanyika katika mwaka huu wa fedha wa 2020/2021 kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*). Kazi hii ipo katika hatua ya manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ina kamilisha usanifu wa kina, imeendelea kutenga fedha na kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iendelee kupitika kipindi chote cha mwaka ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021, jumla ya shilingi bilioni 2.29 zimetengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa Nape Nnauye.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa upembuzi yakinifu wa kipande cha Ifakara – Kihansi chenye kilometa 125

umekamilika. Je, Serikali iko tayari kuanza kutenga fedha ya kujenga hiki kipande katika mwaka huu wa fedha?

Mheshimiwa Spika, swali la pili barabara ya Lutamba-Chiponda-Mnara-Nyengedi inayounganisha Halmashauri ya Mtama na Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ambayo pia inaunganisha barabara ya Mkoa ya kwenda Ruangwa lakini pia ya kwenda Masasi kwa maana ya Mkoa wa Mtwara, ni barabara ya muhimu sana kwa uchumi wa eneo hili, lakini hii barabara imekuwa chini ya *TARURA* kwa muda mrefu na *TARURA* kwa kweli hawana uwezo wa kuendelea kujenga. Je, Serikali iko tayari kuipandisha hadhi barabara hii sasa ianze kuhudumiwa na *TANROADS*?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri *Engineer* Godfrey, tafadhali

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Nape, Mbunge wa Mtama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoiuliza ya Mheshimiwa Kunambi ni barabara ambayo inaunganisha Mkoa na Mkoa na kwa kuwa usanifu wa kina umekamilika, tunaamini katika bajeti ijayo Serikali itanza kujenga kwa kiwango cha lami. Nikiri Mheshimiwa Kunambi kila anaposimama imekuwa akiipigia sana kelele barabara hii. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi kwamba katika bajeti tunazoanza kuzitekeleza kwa mwaka ujao naamini itatengewa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Nape Mbunge wa Mtama sitazitaja barabara zake zimekuwa ni nyingi Lutamba-Chiponda-Mtama-Lindi na kwamba ni barabara za *TARURA*, naomba Mheshimiwa Nape nimshauri waweze kupitia kwenye taratibu za kawaida za kupandisha hadhi hizi barabara kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS* ambapo lazima watakaa na Bodi ya Barabara ya Mkoa halafu itakwenda kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa na

baadaye zinakuja kwenye Wizara kwa ajili ya kuziangalia kama zinakwenda kupandishwa hadhi. Kwa hiyo kama zitakuja kwa utaratibu huo nadhani kuna utaratibu zitafikiriwa na Serikali itaona namna gani ifanye ili kuzipandisha hizo hadhi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa mkiangalia saa yetu mtaona muda wetu umepita kweli kweli. Tunao wageni wengi sana kwenye *galleries*, nitajitahidi kwa haraka haraka tuweze kuwatambua.

Wageni watano wa Mheshimiwa Spika kutoka Benki ya *Equity* wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Ndugu Robert Kiboti; Ndugu Godwin Semunyu, Mkuu wa Kitengo cha Masoko; Ndugu Isabela Maganga, Mkuu wa Kitengo cha Biashara; na Ndugu Upendo Makula, Meneja wa Tawi letu la Dodoma hapa la *Equity*. Ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Julieth Mahugi, Afisa Mikopo, ahsante sana. Afisa Mikopo hebu simama tena Waheshimiwa wakuone, jamani ndiyo anashughulika na mikopo, Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiongozwa na Mwenyekiti wa *DUKSA* Ndugu Janja Silas kutoka *UDSM* simameni wote kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Karibuni na ahsante sana. *(Makofi)*

Wageni 23 wa Mheshimiwa Deo Ndejemi, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni Madiwani na Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Chamwino, Mkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mheshimiwa Olipa Maganyila, Wanyachamwino. Karibuni sana, hawa wanatoka Jimbo la Ikulu. Waheshimiwa Madiwani karibuni sana kututembelea, mjifunze mambo mbalimbali. Kama mtakuwa na mahitaji yoyote kwa muda ambao mtakuwa hapa mtatujulisha na Mheshimiwa wenu natumaini mmemwona anapokaa, Mheshimiwa Ndejemi naomba wakuone bwana,

mmemwona Mheshimiwa wenu. Ahsanteni na karibuni sana ndugu zangu wa Chamwino. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa ambao ni Viongozi wa Muungano wa Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori Nchini kutoka mikoa mbalimbali wakiongozwa na Ndugu Christopher Mademla, WMA karibuni sana. *(Makofi)*

Ndugu Byabato, Naibu Waziri Nishati ana wageni wawili, ndugu Lyakurwa, Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Bukoba Mjini na Aidan Bigirwa, mpigakura. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 19 wa Mheshimiwa David Kyenzile ambao ni wakulima wa chai kutoka Kata ya Ruhanga, Mufindi, Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Ndugu Balo Mgonzo. Karibuni sana popote pale mlipo. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Grace Tendega ambao ni wapigakura wake kutoka Kalenga, Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Katibu wa Mbunge ndugu Mwanaidi Mkwawa. Karibuni sana wajomba zetu kutoka Iringa huko. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Stella Ikupa ambao ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Mbeya wanaoitwa David Mwangaba na Asunta Nombo, karibuni popote mlipo wageni wa Stella Ikupa. *(Makofi)*

Wageni 21 wa Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Robert Willy, UDOM karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni wapiga kura wake wakitoka Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro Amran Kessy, Mohamed Yussuf na Athuman Ally. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Stella Fiyao ambao ni ndugu zake kutoka Mkoa wa Songwe wakiongozwa na

mume wake Ndugu Simon Fiyao. Karibuni sana. Shemeji yetu yuko wapi Simon, Ndugu Simon unaweza kusimama tena. Ahsante sana, nyie watu wa kamera hamjaweka vizuri, hajaonekana, wewe mtu wa kamera namna gani, weka vizuri kamera yako, Simon hebu simama bwana, *camera* peleka kule ambako natangaza siyo unanionyesha mimi. Ahsante sana sasa tumekuona shemeji. (*Kicheko/Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Ngwasi Kamani ambaye ni mwanachama wa Chama Cha Mapinduzi toka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Kelvin Barege. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Kasalali Mageni ambao ni familia yake kutoka Sumve Mkoani Mwanza wakiongozwa na mke wake ndugu Rebecca Mageni, wale kutoka Sumve karibuni sana, Rebecca yuko wapi karibu sana, huyu binti inaelekea ni wa Kigogo na mjukuu amekuja, hebu msimamisha tumuone bwana, wako wawili, watatu, eee ayayayaaa. Mheshimiwa Mageni taratibu bwana. Ahsante na karibuni sana kama familia. (*Kicheko/Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Sylvia Sigula ambao ni vijana wajasiriamali wanaosafirisha mizigo kutoka China ambao ni Ndg. Issa Ibrahim, Ndugu Frank John na Ndugu Safir Sekule. Karibuni sana wasafirisha mizigo. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaye ni Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2015 Ndugu Amaold Litimba. Karibu sana sana na hongera kwa kukimbiza Mwenge mwaka huo. (*Makofi*)

Wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. John Pallagyo ambao ni wapigakura wake kutoka Arumeru wakiongozwa na Ndugu Aminiel Mungure. Karibuni sana ndugu zetu kutoka Arumeru. (*Makofi*)

Wanachuo 50 wa Chuo Kikuu cha Kiislam kilichopo Mkoa wa Morogoro ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi zake. Wale wa *Islamic University*

*Morogoro*, ooh, karibuni sana sana Bungeni vijana wetu muweze kujifunza mambo mbalimbali. (*Makofi*)

Wanafunzi 90 na walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mtakatifu Monica iliyopo Jijini Arusha ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi. Mtakatifu Monica, karibuni sana Bungeni, wamependeza watoto hawa, hongereni sana na Mbunge wenu wa Arusha, Mheshimiwa Mrisho Gambo yupo, natumaini mmemuona anapokaa, hongereni sana Mtakatifu Monica. (*Makofi*)

Shule za wasichana ni nyingi, nzuri, wanapendelea mbona shule za wavulana sizioni? Naibu Waziri wa Elimu, hivi unajua shule za wavulana yaani *boys only* sekondari *schools* za kiwango hicho ni chache? Ziko wapi? Kwa mfano, hapa Dodoma ipo wapi? Hamna shule za wavulana, sasa wataolewa na nani hawa? (*Kicheko/Makofi*)

Msiwaache wavulana, hivi Waheshimiwa Wabunge mnajua ni kweli wavulana wanaachwa? Kabisa wanaachwa hivi hivi. Kwa hiyo, tuangalie kidogo hii hali, nafikiri badala ya *TWPG* itengenezwe ya wanaume nayo tuanze kuangalia hii hali maana wanaachwa. (*Makofi/Kicheko*)

Wanafunzi 90 na walimu 10 kutoka Shule ya Msingi ya *Assumption* ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi. Wanafunzi wa *Assumption*, karibuni sana. (*Makofi*)

Wanachuo watatu wa Chuo cha St. John's ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyofanya kazi, Ndugu Brighton Bernard, Ndugu Deus Polepole na Ndugu Tumaini Mseche. Karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna baadhi yetu wanasema kuna joto sana humu ndani wanaomba baridi iongezeke kidogo.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaaaa! (*Kicheko*)



**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Naibu Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Dkt. Mabula anawatangazia baadhi yenu mmepata bili za malipo ya viwanja vyenu mnavyovimiliki sehemu mbalimbali hapa nchini basi mjiitahidi kulipa. Pia anawakumbusha kujaribu ku-*search* viwanja mliyonyavyo kila mmoja wetu popote pale hapa nchini ambavyo mnadaiwa na Serikali basi ni wakati wake wa kulipia mapema iwezekanavyo. Tunaombwa sana tulipie viwanja tukiwa kama mfano kwa jamii.

Mheshimiwa Jasson Rweikiza anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM, saa saba kikao pale Msekwa na Wabunge wengine wote na hasa wa ACT Wazalendo mnakaribishwa kwenye kikao cha CCM. Mheshimiwa Khatib siyo mimi ni Mheshimiwa Jasson Rweikiza. *(Kicheko)*

Niwatangazie Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi kukutana saa 6.00 hapa *lounge*, Mheshimiwa Naibu Spika ataongoza kikao hicho. Mheshimiwa *Chief Whip* saa 6.00, kwa dakika chache tu Kamati ya Uongozi ili muweze kutoa mrejesho wa kikao chetu cha mara ya mwisho.

Pia niwataarifu Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kutakuwa na kikao leo kuanzia saa 6.00 pia kwenye ukumbi wenu wa kawaida ambako mnakutana ili muweze kuzingatia suala la Mheshimiwa Felister Njau. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anawatangazieni Waheshimiwa Wabunge kuwa kuna kampuni inaitwa *Natural Therapies Limited* ambayo inafanya maonesho ya dawa zake hasa dawa yake inayoitwa *Immune Booster* kwenye viwanja vya Bunge, nyuma ya ukumbi wa Msekwa. Imeelezwa kuwa dawa hiyo ina uwezo mkubwa sana wa kukabiliana na magonjwa ya mfumo wa upumuaji yanayosababishwa na virusi mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge, mnakaribishwa sana kutembelea nyuma ya ukumbi wetu wa Msekwa na kujiridhisha na kinachoendelea kule.

Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MIPANGO**

**SPIKA:** Kamati ya Mipango.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Kamati ya Mipango.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, orodha yangu ni kubwa kwa hiyo, tunakwenda moja kwa moja na uchangiaji ni moto moto. Tuanze na Mheshimiwa Zungu, utafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Tabasamu ajiandae.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo la Chama cha Mapinduzi kwa Serikali kutaka uchumi uwe asilimia nane unaweza kufanikiwa katika Taifa letu ikiwa ni pamoja na asilimia za juu zaidi. Ili kufikia hapo ni lazima Benki Kuu ya Tanzania iwe ina-*regulate* (inasimamia) riba kwenye mabenki ya biashara nchini mwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, riba za mabenki ni kubwa mno, ili kukuza uchumi ni lazima riba zishuke. Riba zikishuka zitafanya vilevile na kodi kwa upande wa *TRA* ambapo sasa hivi wanakusanya kodi vizuri, wanaweza kukusanya zaidi wakiwa na kodi rafiki. Kodi rafiki itamwezesha mlaji au *private sector* kuwa na mishahara mizuri kwa watumishi wao. Ukiwa na mishahara mizuri *nominal wages* ikiwa *above inflation rate* mlaji anakuwa na *disposable economy*. *Disposable economy TRA* watapata kodi kutoka kodi ya ulaji ambayo mteja wake

atakuwa na uwezo wa kwenda kununua bidhaa katika soko ndani ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe TRA pamoja na kazi nzuri wanayoifanya, wajaribu kuwa na kodi Rafiki. Kwa takwimu za TRA walipaji kodi Tanzania ni wachache sana, tuwe na wigo mkubwa wa walipaji kodi na kodi ikiwa rafiki lazima TRA watapata kiwango kikubwa sana cha ukusanyaji kodi na itaendana sawasawa na pato la Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi rafiki inachangamsha biashara ndani ya nchi. Leo shughuli za za biashara Kariakoo asilimia kubwa zimelala kwa sababu ya kodi za TRA wanazozitwika siyo rafiki. Wakiweza kubadilika kuweka kodi rafiki wataweza kuwafikia wateja wengi na wateja wengi wakilipa volume ya kodi itakuwa kubwa na kuifanya TRA iweze kukusanya mapato kwa rekodi kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajenga barabara kwa pesa za ndani, ni jambo nzuri sana. Daraja la Kigamboni ni mfano mzuri wa PPP kati ya Serikali na private sector. Leo Daraja la Kigamboni linakusanya shilingi 1,100,000,000 kwa mwezi takribani shilingi 13,000,000,000 kwa mwaka. Kwa hiyo, inaelekea kwa miaka 15 ijayo deni la uwekezaji wa Daraja la Kigamboni litakuwa limekwisha. Maana yangu nini? Serikali na wataalam wa TRA wawe sasa na muono wa kutazama road toll kugharamia barabara ambazo zitakuwa zinatumika ili fedha hizi ziweze kutumika kujenga barabara zetu za ndani na za mikoani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mijini katikati barabara zinajengwa na TARURA lakini barabara hizi bado zinakuwa na msongamano kwenye barabara za TANROADS kwa sababu barabara za mijini hazina uwezo wa kubeba magari haya. Wakiweza kutengeneza barabara za ndani au za mitaani zitaweza kusaidia barabara zinazounganisha Mkoa na Wilaya kuweza kupitika kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali watizame namna gani *road toll* itakavyoweza kusaidia kujenga barabara ndani ya nchi yetu. Kwa kufanya hivyo, tutaipunguzia Serikali mzigo kwa sababu pesa nyingi za ndani zinaweza zikatumika kuwekeza kwenye kilimo, elimu na kwenye mambo mengine sana ya tafiti ambayo ni muhimu kwenye Taifa letu. Barabara za ndani ambazo ndiyo zinabeba mazao ya wakulima zitaweza kuwa zinapitika ikiwa barabara kubwa zitajengwa kwa njia ya *road toll*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali pamoja na mikakati mizuri inayoendelea kufanywa tufungue wigo wa kuongeza walipa kodi. Walipa kodi waliokuwepo sasa hivi wanalipa kodi vizuri na sasa hivi kutokana mwamko wa Serikali yetu hii ya Awamu ya Tano wafanyabiashara wote wana-*appetite* ya kulipa kodi, wako tayari kulipa kodi, lakini kodi yenyewe walipe wengi wasilipe wachache ili kufikia *target* ya Serikali. Nina uhakika kama tukiwa na kodi rafiki, makusanyo ya Tanzania yatazidi asilimia 30 ya pato la Serikali na yakizidi maana yake Serikali itakuwa na uwezo wa kujiendesha na itajipa heshima kubwa sana ndani ya Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kununua ndege ya mizigo. Naiomba Serikali, ndege za mizigo ni jambo muhimu sana kwa ajili ya kusafirisha bidhaa zetu kuzitoa hapa na kuzipeleka kwenye masoko. Ndege hii isifanye kazi tu ya kupeleka bidhaa zetu kwenye masoko ya nje ifanye vilevile kazi ya kubeba mizigo yetu ndani ya soko la Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ndege itakayonunuliwa lazima iweze kukidhi malengo haya yaani iwe ndege kubwa lakini iweze vilevile kutua kwenye viwanja vidogo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Umeniwekea dakika kumi Mheshimiwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana tayari.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakumbushwa na Katibu hapa kwamba tangu jana ni dakika tano tano. Kwa hiyo, tunakwenda kwenye tano tano Waheshimiwa. Mheshimiwa Josephine Genzabuke nilishakutaja.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kazi kubwa na nzuri iliyokwishafanya kufikisha maji vijijini. Kazi imeshaanza na inaendelea na mwenye macho haambiwi tazama maana kazi kubwa inaendelea kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumejaliwa kuwa na vyanzo vingi vya maji, ikiwa ni pamoja na maziwa, mito mikubwa pamoja na mito midogo midogo. Kwa kutumia fursa hizo nashauri tutumie vyanzo hivyo tulivyojaliwa na Mwenyezi Mungu kuhakikisha tunafikisha maji vijijini. Maji ni uhai, maji ni kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wengi vijijini wamejajiri katika shughuli za kilimo. Hivyo basi, maji yakifikishwa vijijini watapata nafasi ya kwenda kushughulika na shughuli nyingine za kuzalisha mali na kuchangia kipato chao na pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishindwa kufikisha maji vijijini wananchi wengi wakiwemo wanawake wataweza kupata magonjwa ya matumbo na tutaweza kutumia pesa

nyingi kwa ajili ya kununulia dawa. Tukifikisha maji vijijini tutaweza kuepusha magonjwa na pesa zitaweza kwenda kufanya shughuli zingine badala ya kwenda kununua dawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Kwa kutumia vyanzo hivyo hivyo vya maji tuendeleo kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Ipo miradi ya maji ambayo ilianzishwa, tunaomba miradi hiyo iendelezwe na iweze kukamilika na mingine mipya iweze kuanzishwa ili kwa kutumia maji tuliyojaliwa na Mwenyezi Mungu tuweze kunufaika kwa kilimo cha umwagiliaji. (Makofi)

Mheshimiwa mwenyekiti, wananchi wengi wamehamasika kulima michikichi na wamehasika haswa na imepelekea wananchi wengi kulima kilimo hiki. Naiomba Serikali iendeleo kutusaidia mbegu. Kwa awamu ya kwanza tumeshapata mbegu za kutosha, tunaomba sasa Serikali iendeleo kuongeza mbegu ili wananchi wale ambao tayari wameshamasika waweze kulima kilimo cha michikichi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kila anapopata nafasi anafika Kigoma. Tunakushukuru sana kwa kuweza kuuangalia Mkoa wa Kigoma na kuweza kufanya zao la mchikichi liwe zao mkakati. Kwa juhudi ambazo umeendelea kutuonesha na sisi tutaendeleo kukuunga mkono kuhamasisha wananchi waendeleo kulima zao hilo la mchikichi hatimaye tuweze kupata mazao ya mchikichi tuachane na kuagiza mafuta nje, tuweze kutumia mafuta tunayozalisha wenyewe. Pesa za kigeni tunazotumia kuagiza mafuta nje zibakie kwetu na kuweza kufanya shughuli nyingine za maendeleo. (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Genzabuke. Nitamuomba tu Mheshimiwa Waziri Mkuu siku nyingine akifanya ziara ya Kigoma akague mashamba binafsi ya michikichi ya Waheshimiwa Wabunge na Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Tabasam nitakupa dakika kumi.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya wananchi wa Sengerema naomba ushauri wangu kwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mpango. Nimeangalia Mpango wake nimeusoma vizuri uliowakilishwa hapa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa niaba yake, lakini kuna maeneo ambayo nataka nipite katika kuishauri Serikali katika Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kelele nyingi zimepigwa na Waheshimiwa Wabunge hapa kuhusiana na *TARURA*, wamezungumza sana kwamba *TARURA* iongezewe pesa na wengine wamekwenda mbali zaidi wakitaka pesa za kuongeza *TARURA* zitoke katika mafuta. Sishauri mafuta yaongezwe bei kwa sababu anayeumia ni mwananchi wa chini, mwananchi maskini na mfumuko wa bei utakuwa ni mkubwa sana na sisi tunajitahidi kupunguza mfumuko wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kuhusu *TARURA*; kwa Waziri wa Serikali za Mitaa ni kwamba *TARURA* wabadilishe mfumo wao kwa hiki kidogo kilichopo. Hawa ma engineer wa *TARURA* waliopo katika miji, manispaa, majiji na halmashauri zetu wapewe mikataba *performance* watakayoifanya katika maeneo yao ndiyo itakayowapa nafasi ya kurudi. *TANROADS* wametoa mikataba kwa ma-engineer wao wa Mikoa na wamefaulu kwa mfumo huo. Haiwezekani meneja wa *TARURA* anaharibu, anahamishiwa sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ushauri wangu pia kwa Waziri Mpango katika Mpango huu aliyenao na kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawa *TARURA* sasa hivi waruhusiwe kufanya kazi za *force account*, tutaona matokeo yake. Kwa mfano, katika wilaya yangu, halmashauri moja tu, Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, tuna kilometa 1,730, bajeti milioni 607, haiwezekani! Ukichukua kwa bei za *TANROADS* ambazo zipo za mkoa, kilomita moja inaanzia milioni 15 mpaka milioni 20. Kwa hiyo, milioni 600 inatengeneza kilometa thelathini na una kilometa 1,700, kwa hiyo nahitaji miaka 50, wakati huo nitakuwa nimeshindwa uchaguzi na nimezeeka na nimestaafu. Wabunge wote hakuna atakayerudi kwa mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, *TARURA* waruhusiwe kununua mitambo na mitambo yenyewe watakayoruhusiwa kununua ni mitambo mitatu tu *motor grader* moja, *roller compactor* na *roller excavator*, vingine vinaweza vikakodiwa. Kwa hiyo, *TARURA* watatengeneza barabara kwa uzuri, pesa za *TARURA* zitatoka wapi? Hapa ndipo pazuri, ni kwamba uwagizaji wa mafuta katika nchi hii hapa kuna tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wanapeleka Muswada huu wa kuagiza mafuta kuagiza mafuta kwa pamoja 2014; Muswada huu uliletwa hapa Bungeni kwa zimamoto, mbio mbio, sasa hapa ndiyo kuna tatizo. Kwa mfano, bei ya mafuta ya Januari, bei yake ilikuwa karibu shilingi 230 au 300 kwa lita, lakini bei ambayo imeonekana ipo kwenye kukokotoa kwa *EWURA*, bei ya mafuta imefika shilingi 708. Katika shilingi 708 ya *petrol* kuna nauli iko pale shilingi arobaini na tisa na senti. Mafuta yale ya *petrol* yamefika hapa shilingi 757 wakati bei halisi kwa wakati huo, mwezi Januari wakati yanaagizwa, hayakuzidi shilingi 300. Sasa kama nchi inataka kufanya mageuzi makubwa ya kiuchumi, hatukwepi sasa hivi nchi kuagiza mafuta yetu kama nchi, tuna matenki *tipperyana* mamilioni ya hifadhi, kwa nini tusinunue mafuta kwa shilingi 300. Katika nchi ambazo zinazouza mafuta nchi za *OPEC* wananaauza mafuta haya kwa *discount*.



Mheshimiwa Mwenyekiti, leo bei ya mafuta ni dolla 160 kwa tani ambayo ni sawasawa na Sh.370 kwa lita. Kama huyo mwagizaji anayepewa tenda anayafikisha mafuta hapa kwa Sh.708, kuna *gap* pale karibu ya Sh.300. Hii ni hatari sana kwa uchumi wa nchi, sisi tunalalamika hatuna pesa, halafu tunawachia watu wanaagiza mafuta. Naomba ushauri wangu uzingatiwe katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Mipango na Bajeti na Kamati ya Nishati na Madini, kwa ruhusa yako pamoja na Waziri wa Uwekezaji, tukutane kwa dharura, mimi naomba, tukajadili hili kwa manufaa ya nchi. Pamoja na tozo hizi, kuna pesa ambayo ni *excise duty* shilingi mia tatu na kitu, kuna pesa ambazo ni *levy* shilingi mia tatu na sabini karibu, kuna fedha ya *petrol fees* shilingi mia moja. Hizi ndiyo pesa zinazokwenda Hazina, zaidi ya shilingi mia saba, lakini kuna tozo, hapa ndiyo roho yangu inaniuma, kuna tozo ya shilingi 80 ya hizi mamlaka, zimeweka hapa pesa zao shilingi 85. Tukizichambua pesa hizi zitakazobakia halisia ni karibu shilingi 60, zitolewe kwa sababu hizi mamlaka ziko chini ya Wizara ambazo zinaleta hapa bajeti zao, tunawapitishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wapeleke kule wakapewe hela Hazina. Shililingi 60 itakayobakia hapa katika hiyo 85, ninachotaka kuomba, pesa hizo ziende *TARURA*, zinatoshia kugharamikia barabara zetu. Haiwezekani tukaliacha hili jambo likapita na tukikutana leo kwa dharura, kesho tunakuletea majibu hapa na tunaondoa hili jambo. Tuishauri Serikali, tumshauri Mheshimiwa Mpango atengeneze bajeti, lakini kuna pesa kwenye mafuta huku zinapigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna *GFI*, hawa *GFI* hawa ni watu wanaweka *marking* katika mafuta wanachukua shilingi 14 kwa lita. Mauzo yetu ya mafuta ni karibu ni lita milioni sita mpaka 12 kwa siku. Huyu mtu anayechukua shilingi kumi na nne anaondoka na pesa zaidi ya milioni 90, kila siku ya Mungu huyu mtu anachukuwa milioni karibu kumi na mbili kwa mwezi, kwa mwaka na gharama za *marking* kuweka ile dawa ya *marking* utaona *Finland* na wapi, nchi zote zinazouza zinauza gharama ndogo sana. Mtu

huyu ana wafanyakazi wawili wawili kila *depot* katika nchi hii ambao hawazidi wafanyakazi sabini, anachukua shilingi 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna *EWURA* sijui anachukua shilingi ngapi, kuna watu wa mizani wanachukua pesa pale, kuna watu wa *survey* kuangalia tu mafuta yamepita kwenye bomba hii shilingi 85, mambo mengine naogopa hata kuyasema hapa kwa ajili ya usalama wa nchi, haiwezekani! Naomba turudi mezani tufukue hii kitu Waziri wa Nishati hiki kitu wakati kinapitishwa hakuwepo, Waziri wa Fedha hakuwepo, Waziri wa Uwekezaji hakuwepo. Naomba kutumia Bunge hili kwa hizi kamati tulizopo, iwe ni msaada katika nchi, turudi mezani kwa amri yako, halafu kesho tuje na majibu. Hawa watu wote ambao wanaingiza tozo zao hapa uagize waje hapa Bungeni haraka leo...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HAMIS H. T. MWAGAO:** Aaaaaa.

Ndiyo ninachotaka kukwambia.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam, dakika kumi zimeisha.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukwambia pamoja na hali hii, naomba tamko lako ili tuokoe hii pesa, tupate pesa za *TARURA*, tutengeneze barabara zetu. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tupatie muda tutawasiliana na Mheshimiwa na Waziri Mkuu halafu tutakuja na mwelekeo unaotakiwa kwa jambo hilo.

Mheshimiwa Munde Tambwe atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda na Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia Mpango wa Serikali. Niungane na Wabunge wenzangu kuipongeza Serikali yote kwa ujumla, kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na watendaji wote kwa mpango mzuri waliotuletea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufinyu wa muda naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Tuko kwenye kupambana kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa nchi ya uchumi wa kati, lakini na kuendelea Zaidi. Tuko kwenye kukusanya fedha lakini tuwe na matumizi mazuri ili nchi yetu izidi kufaidika, lakini tuendeleo kupata maendeleo kama kiu aliyonayo Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuingia Kamati ya Kilimo nimejifunza mambo mengi sana. Kuna miradi inaendelea kule kwenye majimbo yetu tulipotoka unakuta mradi wa bilioni nne lakini *consultants* hawa wanaofanya upembuzi yakinifu wanapata bilioni moja *point*, unashanga. Ukiangalia *consultant* ana ma-*engineer*, ana watu wa *NEMC*, ana Mhasibu sijui wa mradi, lakini ndani ya halmashauri zetu, ndani ya ofisi zetu za mikoa kuna ma-*engineer*, kuna watu wa *NEMC*, kwa nini kazi hizi zisifanywe na ma-*engineer* wetu wenyewe. Hivyo, hii bilioni moja *point* ambayo anaenda kupewa sasa huyu *consultant* ziendeleo kufanya kazi kwenye halmashauri, ziendeleo kuimarisha miradi mingine na kujenga miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali, niwaombe Mawaziri wanaohusika pamoja na watendaji wetu, sasa hivi tumefika *stage* ya kuionea huruma pesa ya Serikali, ma-*engineer* wetu wafanye hizi kazi. Unaweza ukachukua labda milioni mia mbili ama mia tatu ukasema vijana hawa tumewapa kazi hii wafanye upembuzi yakinifu, basi tutawalipa posho hii, kuliko kuchukua bilioni moja *point* kumpa *consultant* ambapo tunao uwezo, tumeajiri watu hao kwenye ofisi zetu, wanalipwa mishahara lakini unaenda kuchukua kampuni binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli unabaki pale pale hizi kampuni ni za kwao wenyewe, ni hawa hawa *ma-engineer* ndiyo wenye hizi kampuni. Kwa hiyo, naomba kabisa yale mambo yanayowezekeana madogo madogo yafanywe na *ma-engineer* watu wetu wa *NEMC* walioajiriwa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuongelea suala la kilimo. Tuko hapa tunaangalia tunavyopata shida ya mafuta, tumekuwa tukiagiza mafuta takribani milioni mia mbili themanini dola kila mwaka. Uwezo tunao wa kulima alizeti, ukiangalia mfano Wilaya ya Manyoni, Mkurugenzi huyo wa Manyoni kama humu ndani yupo kaka yangu Mheshimiwa Jafo, anastahili sifa kubwa, amefanya *block farm* ambayo ameweka heka elfu 30 za korosho. Leo hii heka zile za korosho wameanza kuvuna, lakini baada ya muda pato la mtu moja moja wa Manyoni litaenda kuimarika. Baada ya muda halmashauri yao itakusanya *Cess* zaidi ya bilioni 10 na kuhakikisha watajenga zahanati zao, watajenga madarasa yao na watatengeneza madawati yao. Hiyo ni *block farm* tu moja iliyowekwa na Mkurugenzi mmoja katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira zitapatikana, kodi italipwa, wakiuza nje Serikali Kuu itapata pesa na kadhalika, lakini mambo mengine mengi mengi yatapatikana hapo. Sasa ninachojuliza imekuwa halmashauri nyingi kupitia Kamati zao za Fedha wanaenda kutembea pale, wanaenda kujifunza pale, lakini toka wameanza kujifunza hakuna halmashauri nyingine yoyote ambayo imeanza kuweka *block farm* labda ya alizeti au ya kitu gani ili kuondokana na huu umasikini wa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza, Uganda walienda kujifunza pale Manyoni, leo Uganda wameanzisha *block farm* kama ya Manyoni, sisi kwa nini Tanzania tunashindwa, leo tukianzisha *block farm* kila wilaya katika mikoa mitano, heka elfu 10 za alizeti zikaangaliwe na Maafisa Ugani wetu, wataalam wetu wakaa pale kwenye *block farm*, wananchi wakapata ile ardhi kwa bei nafuu, wakapata mbegu za bure au za bei nafuu, tunaweza tukalima alizeti

nyingi na tukapata mafuta ya kwetu sisi wenyewe na tukaacha kutoa pesa yetu ndogo hii ya Serikali kuagiza mafuta ambapo tunaacha kufanya huduma za muhimu tunaagiza mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufinyu wa muda niongelee kidogo umwagiliaji. Kule kwetu Tabora tumelitewa bilioni mbili kwa ajili ya kujenga bwawa la umwagiliaji, hakuna kinachoendelea bilioni mbili zimewekwa kule ndani lakini kumelimwa heka kumi na tano tu...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE TAMBWE ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana sana. Kwa kweli Manyoni hata mimi na halmashauri yangu, nilikusanya Madiwani wote, Viongozi wa Chama, tulikwenda kutembelea Manyoni. Baada ya ziara ile tumebadilika sana ndiyo maana Kongwa sasa hivi tunapanda korosho, yaani kuliko maelezo.

Kwa hiyo, Mkurugenzi kama yule ni mzuri sana, lakini watu kama wale siyo wa kuwapandisha daraja unampeleka sijui Wizarani, hapana yule akae kule kule ili azidi kufanya vitu ambavyo ni *more innovative* katika eneo hili.

Waheshimiwa Wabunge ambao hamjawahi kufika Manyoni *make it a point* safari moja *weekend* moja unakwenda na kurudi. Ni *just two hours* unakwenda, unashinda kule *five or six hours*, badaye tena unarudi *two hours on the weekend*, mwende mkaone ubunifu wa Watanzania wenzetu hawa, Manyoni *they doing very good thing*, Mheshimiwa Chaya endeleza kile kitu cha korosho Manyoni, ni safi sana na inatia moyo sana. Ndio maana siku zote huwa nawatania kwamba, Mtwara na Lindi msipoangalia kanda ya kati inaweza ikachukua nafasi katika

muda siyo mrefu, kabisa kabisa. Ahsante sana Mheshimiwa Munde.

Nilikutaja Mheshimiwa Joseph Kakunda, halafu Mheshimiwa Esther Bulaya.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nimesoma mapendekezo ya Mpango kwa makini na nimeona kwamba kuna maeneo mazuri kama kwa mfano maeneo ya malengo. Eneo la malengo limekaa vizuri; eneo la kazi za kufanya kufika malengo limekaa vizuri; eneo la mahitaji ya rasilimali watu na rasilimali fedha limekaa vizuri, lakini kuna tatizo kwenye maeneo mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo la mfumo wa ukusanyaji wa mapato, hili eneo inabidi Serikali iangalie kwa makini kwa sababu bado kuna vyanzo vingi havikusanywi. Vile vile Sheria ya *TRA* inaruhusu mapatano, yaani unakwenda kwa mtu unamkadiria alipe milioni mia nane, halafu akikaa kwenye mapatano unaweza ukashusha mpaka milioni mia nne. Hili ni tatizo kubwa. Hakuna utawala bora wa namna hiyo kwenye sheria. Kama sheria inaruhusu mapatano, hiyo sheria inakuwa haifai. Kwa hiyo, inatakiwa kwa kweli wafanye mapitio makubwa kwenye Sheria ya *TRA* ili sheria ikisema sharti hili kodi yake ni shilingi kumi na tano, iwe shilingi kumi na tano isiruhusu mapatano. Kuruhusu mapatano huo ni mwanya mbaya sana kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nimeona kwamba limefanyiwa mapitio ni mifumo ya udhibiti wa nje na ndani *internal and external* controls yaani ni muhimu sana kudhibiti matumizi ya fedha kama tunataka matokeo mazuri. Jambo la tatu eneo la ufuatiliaji na tadhimini, nalo halijakaa vizuri katika utekelezaji. Kwenye maandishi linaweza kukaa vizuri, lakini katika utekelezaji haijakaa vizuri, nani anawajibika pale ambapo kunakuwa na tatizo, anatakiwa *a person*, lazima mtu binafsi awajibike siyo taasisi kuwajibika. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo linatakiwa lifanyiwe mapitio ya kutosha ili tuwe na mpango mzuri hapa baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikipitia utekelezaji uliofanyika, umefanyika vizuri sana. Kwenye huduma za jamii, elimu, afya na maji, utekelezaji umefanyika vizuri sana kwa nchi nzima. Hata humu ndani walio wengi wa majimbo wamepita kwa sababu ya utekelezaji mzuri uliofanyika kwenye sekta za huduma za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia utawala bora; sheria kama haitoi usawa, hiyo sheria ina matatizo. Kwenye eneo la utawala bora tulikuwa tunaathiriwa na upande wa sheria, sheria kwanza ni za zamani sana, zimepitwa na wakati, lakini kuna sheria hazitowi usawa. Kwa mfano, Sheria ya Trafiki, trafiki akikamata pikipiki anatoza shilingi 30,000 kwa kosa lolote lile; akikamata gari dogo shilingi 30,000; akikamata gari kubwa la mizigo shilingi 30,000. Hiyo sheria haitoi usawa, kwa mfano ingekuwa sawa pikipiki atoe shilingi 5,000; gari dogo atoe shilingi 10,000; gari nyingine yenye uzito fulani atoe shilingi 15,000 na gari kubwa atoe shilingi 30,000. Hapo ndio sasa Sheria ingetoa usawa kulingana na uzito wa matumizi ya vyombo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo ambalo limefanyika vizuri sana, nalo ni la amani, usalama na utulivu wa nchi. Kwenye eneo la kukuza uchumi, nina ushauri maeneo machache. Nchi hii haitaendelea bila ardhi kupimwa. Ardhi ndiyo uchumi, ardhi ndiyo itawafanya Watanzania wapate uchumi. Kama Wizara ya Ardhi itaendelea kushugulikia migogoro midogo midogo tu na kuwasubiri watu kwamba tunamsubiri mtu ambaye atakuja kuomba kupimwa kieneo chake badala kupima ardhi yote, mtu kama anataka ardhi aende akachukue ardhi ambayo imepimwa, kitakuwa kitu kizuri sana kwa uchumi wa nchi hii. Kwa hiyo, Serikali lazima ioneshe kwenye Mpango namna ambavyo watapima ardhi yote katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kazi imefanyika vizuri sana kwenye maliasili, kwenye eneo la mawasiliano vijijini, barabara, madaraja makubwa, reli na bandari. Tatizo liko kwenye bajeti ya *TARURA*, namuunga mkono mzungumzaji,

ndugu yangu Mheshimiwa Tabasamu, lazima *TARURA* waongezewe bajeti kama tunataka kusaidia uchumi wa nchi hii.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ni kweli Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, tuwe na mpango halisi wa namna ya kupima ardhi nchi nzima kama alivyosema. Hata hivyo, watumishi wa ardhi kwa kila halmashauri ni wachache sana, unakuta watano, wanne, sita, hawataweza. Kama kuna eneo mnahitaji watumishi wengi sasa hivi ni eneo la ardhi ili ardhi ya nchi hii ipimwe. Ikipimwa tutapata hayo mabilioni tunayohitaji, tutafanya mambo mengi ya maendeleo.

Ni kweli tunapeleka watumishi wengi sana kwenye huduma za jamii; afya, elimu, *good*. Hata hivyo, usipopeleka watumishi kwenye huduma za uchumi nalo ni tatizo, lazima huduma za uchumi ambazo ni ardhi na zingine zikuletee fedha. Kwa hiyo, tukiajiri 15 huku, huku tuajiri hata 500, hata 1,000, itatusaidia sana katika kufikia lengo hilo. Kwenye mpango huu tupime ardhi, kabisa.

Mheshimiwa Ester Bulaya, utafuatiwa na Mheshimiwa Abdullah Mwinyi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa tunapoamua...

**MWENYEKITI:** Una dakika kumi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama Taifa tunapoamua kupanga katika mipango mbalimbali ya kitaifa, dhamira ni kuhakikisha mipango



inatekelezeka kwa lengo la kukuza uchumi wetu, kwa lengo la kuhakikisha tunaongeza pato la Mtanzania mmoja mmoja na kwa lengo la kuhakikisha tunaongeza ajira kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unajua, katika mipango yote suala la Mpango wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma ni takribani zaidi ya miaka 20 linaongelewa katika Bunge hili. Liganga na Mchuchuma ilikuwepo katika mipango yote. Lazima tujiulize Serikali ya Chama cha Mapinduzi mna dhamira, mikakati na malengo ya kuhakikisha mnamuondoa Mtanzania kwenye umasikini na mna lengo la kuinua pato la Mtanzania mmoja mmoja au tunafanya kazi kwa mazoea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaliwa kuwa na madini ya chuma takribani tani milioni 126. Tumejaliwa kuwa na madini ya makaa ya mawe takribani tani milioni 428. Leo tunajenga reli ili ule mradi ukamilike unatarajiwa kutumia shilingi trilioni 17 na katika hizo ziko pesa za mikopo lakini tunaagiza chuma kutoka nje wakati Mwenyezi Mungu ametupa chuma chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza kupitia Shirika letu la *NDC* ambalo lina hisa asilimia 20 na kampuni ya Kichina tumeingia mkataba zaidi ya miaka saba lakini hakuna kinachoendelea katika Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Sheria ya Madini, kifungu cha 47(2) kimeweka wazi ukipewa mkataba na leseni unatakiwa utekeleze ndani ya miezi 18. Tuna hisa asilimia 20 kupitia *NDC*, kuna Mchina ana asilimia 80 amevunja sheria, anafichwa. Kuna *interest* gani, kuna nini kinajificha huku pesa tunakwenda kukopa nje, tunaagiza chuma kwa kukopa nje halafu kuna mtu tunambeba, tuna madini tumepewa na Mwenyezi Mungu, tuko *serious*? Halafu tukihoji mnatupa tu maneno, timizeni wajibu wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi kule wa Njombe na Ludewa hawaendelezi maeneo yao. Wamesema wapishe eneo la mradi...

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UWEKEZAJI):**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester, upewe taarifa;  
Mheshimiwa Waziri nimekuona.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UWEKEZAJI):**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea kuwa Mradi wa Liganga na Mchuchuma una vipengele sita. Vipengele vitano vimeshafanyika, kimebaki kipengele kimoja ambacho kinahusu mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii mikubwa ina maslahi makubwa kwa nchi. Unapoingia mikataba na mashirika ya kimataifa lazima uwe makini. Kwa hiyo, majadiliano yanaendelea na yapo katika hatua za mwisho kuhakikisha kwamba mkataba huu unakuwa na maslahi mapana. Kwa hiyo, anavyosema hakuna kinachoendelea siyo sahihi kwa sababu ina mambo sita, matano yameshafanyika, limebaki jambo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba apokee taarifa hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, pokea hiyo taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei taarifa, najua ni Waziri mgeni. Hili jambo tangu enzi za mama Mary Nagu, vipengele vitano miaka 20 *brother?* Hii ni taarifa ya sasa hivi ya Waziri na inasema hiyo kampuni haina uwezo wa kuwekeza dola za Kimarekani bilioni 2.9. *Shame!* Okoeni pesa za Watanzania, tunaagiza chuma kutoka nje, Mwenyezi Mungu ametupa chuma chetu; tunahitaji nini? Halafu unajibu majibu kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Ludewa, Njombe, maeneo haya takribani zaidi ya miaka saba wameshindwa kuyaendeleza. Mnasema Serikali ya wanyonge wakati kuna watu kule mnawasimamisha zaidi ya miaka saba hawaendelezi maeneo yao, hawajalipwa fidia, mnamlindwa mwekezaji mnasema maslahi ya nchi; yako wapi wakati huyu amevunja Sheria ya Madini, kifungu cha 47(2) miezi 18 imeisha, *like seriously?* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mtimize wajibu wenu. Haya madeni wanakuja kuyalipa Watanzania. Kuna mtu alisema dunia ni chuma, chuma tunacho tunaagiza nje kwa hela za mikopo; kweli? Halafu tunakuja tunafanya mzaha hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Najua Serikali imekwenda kuchukua pesa tena kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwenda kuwekeza kwenye viwanda. Hatukatai kuchukua fedha za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza kwenye viwanda kama kuna dhamira njema na Serikali mnalipa hizo fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Ripoti ya CAG, inaonesha hali ya Mifuko ni dhoofulihali, mifuko iko taabani. Ripoti ya mwanzo...

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, upokee taafifa kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba mpaka leo napoongea hapa kama Waziri wa sekta, thamani ya Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii imeshapanda

mpaka shilingi trilioni 11.510. Sasa kama thamani ya Mifuko hii imeshafika shilingi trilioni 11.510 mpaka sasa, hicho ni kiashiria kwamba sekta inakua na siyo inakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nani mwenye majukumu ya kusema kwamba sekta inakufa? Ukitaka kuwa na mamlaka ya kusema mifuko inakufa ni lazima ufanye *actuarial*. Sasa hivi ndiyo tupo kwenye huo utaratibu wa *actuarial*. Mtathmini ameshaanza kufanya utathmini wa Mfuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, manunuzi ya Mtathmini kwa ajili ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa sekta binafsi yameshakamilika. Kwa hiyo, taarifa ya Mthamini ndiyo itakayokuja kutupa uelekeo mzima wa sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka haya Mheshimiwa Ester ya kusema kwamba mifuko imekufa kabla Mtathmini hajatoa ripoti anayatoa wapi? CAG anafanya ukaguzi wa mwenendo wa fedha, Mtathmini kwa vigezo vya Umoja wa Mataifa na Shirika la Kazi la ILO ndiye atakayetupa mwelekeo wa Mifuko na sekta. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ester asubiri, asianze kuwahisha shughuli mapema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Ester Bulaya, unaipokea?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza amejichanganya mwenyewe, naye amejuaje hiyo thamani kama bado tathmini haijafanywa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya kwanza kabla Mifuko haijaunganishwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali wa kwenu amesema mifuko haina uwezo wa kulipa madeni yake pamoja na madeni ya wastaafu. Amefanya tena ukaguzi na wewe unajua tarehe moja hapa tulipitisha Sheria ya Kikokotoo ukaliahidi Bunge na wewe ukaponea chupuchupu akaondolewa yule Mkurugenzi mwingine, ukaahidi hapa Bungeni mnakwenda kufanya tathmini ya madeni, huu mwaka wa nne *sister*, hukufanya. *(Makofi)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua ni lazima tutoe taarifa kwa sababu watu wasipotoshe mambo humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya Mtathmini wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii ilifanyika kwa mara ya mwisho mwaka 2016/2017. Tathmini ile tuliifanya baada ya kupata maoni kutoka kwa wadau mbalimbali na walitushauri namna ya kwenda kwenye *merging*. Tulipitisha sheria hapa ndani kwamba mwaka mmoja, miwili baada ya *merging* ndiyo sasa tutafanya tathmini yenye uhalisia wa kujua baada ya *merging* mifuko yote na sekta inakwendaje. Sasa asichanganye tathmini ya *merging* na tathmini hii baada ya *merging* tunakwendaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo masuala mengine ya kupona au kutokupona siyo kazi yake, iko mamlaka ya kutathmini haya yote. Mimi nasimama kama Waziri wa sekta namwambia Mheshimiwa Ester, tathmini ni mbili; ya *merging* ilishakwisha, tunasubiri ya mwenendo tunaokwenda sasa hivi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, taarifa hiyo, ipokee.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu atulie tu, hayo mambo mimi hayanihusu ila ninachomwambia, mlipe madeni. Mnakopa hamfanyi tathmini, wastaafu hawalipwi humu ndani kila Mbunge anapiga kelele. Haya, kwa tathmini tu aliyofanya CAG Serikali

mnadaiwa shilingi trilioni mbili na bilioni mia nne kumi na saba, fedha za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo sijazungumzia deni la *PSPF*, takribani shilingi trilioni 11, mliwaamrisha wawalipe watu ambao hawachangii. Leo kwenye viwanda 12 mmekwenda kuchota tena fedha shilingi bilioni 339 kuendelea kuwekeza huku mnadaiwa shilingi trilioni mbili.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Eeoh.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, utanisamehe sana. Unajua ni lazima Bunge hili lielewe mwelekeo wetu ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria, kazi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya kwanza ni kuandikisha wanachama, ya pili ni kukusanya michango. Huwezi ukakusanya michango ukaitunza benki eti isubiri tu watu watakapostaafu uwape. Kazi ya tatu ni kuwekeza na unapowekeza michango unaongeza thamani ya ile michango muda utakapofika uweze kuwalipa wastaafu kwa kuzingatia sheria na taratibu zinazowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo kweli kwamba Serikali inajichoteachotea tu, hapana. Serikali inawekeza kwenye uwekezaji wenye tija ili muda unapofika mafao yaweze kupatikana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):** Sasa kama anataka hiyo michango iwekwe tu benki bila kuongeza thamani utapata wapi fedha? Kwa hiyo, Mheshimiwa Ester aelewe hesabu hizi za hifadhi ya jamii, azielewe vizuri.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Halima, haiwezekani taarifa juu ya taarifa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Ester Bulaya, unapokea taarifa?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei. Halafu anajua mimi nilikuwa Waziri Kivuli wa Sera na Uratibu wa Bunge, anajua nilivyomkimbiza humu ndani kupitia Sheria ya Kikokotoo na Mheshimiwa anazungumzia michango, anataka nije huko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta zenu za Kiserikali, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi mliacha kupeleka michango shilingi bilioni 85; Mfuko wa Hifadhi ya Jamii shilingi bilioni 61; Mfuko wa Bima ya Afya bilioni 24 michango mlichelewa ninyi ndani ya siku 30, unazungumzia michango? Nazungumzia mlipе madeni, muwekeze kwenye maeneo ya mikakati. Hizi pesa siyo zenu, ninyi ni wasimamizi, pesa hizi za wastaafu wa taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hatuoni dhambi kila Mbunge akisimama humu kuna wastaafu wana miaka miwili, wengine miezi sita hawajalipwa halafu hela zao mlizokopa hamlipi, mnachukua zingine mnakwenda kuwekeza, kwanza mmefanya tathmini hivyo viwanda vinalipa; mmefanya? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipeni pesa za wastaafu wa nchi hii, wamelitumikia taifa hili kwa jasho la damu. Mnataka morali iongezeke kwa hawa waliopo kazini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, muda hauko upande wako, muda umekwisha. *(Makofi)*

Nilikuwa Mheshimiwa Abdullah Mwinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mheshimiwa Asia Halamga ajiandae.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa zawadi hii. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na Ardhi kwa kutujalia uhai, afya na ustawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza toka tulivyoinjia Bungeni kuongea ndani ya Bunge hili Tukufu, napenda vilevile kuwashukuru wannachi wa Jimbo la Mahonda pamoja na chama changu cha CCM kwa kunipa ridhaa na kuniingiza hapa mjengoni niwe mwakilishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais, Mwenyekiti wetu wa Taifa, kwa uamuzi, ujasiri na umahiri wake mkubwa katika kuongoza nchi hii kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Sina haja ya kuyazungumza yote aliyoyafanya, walionitangulia, Mheshimiwa Askofu Gwajima na Mheshimiwa Polepole wameyasema yote ya msingi kabisa ambayo yamefanyika katika hii miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite katika maeneo matatu. Eneo la kwanza huu Mpango umekamilika na umefanyika kwa kiwango cha hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kugusia maeneo ambayo nahisi hayajawekewa mkazo mkubwa ambayo ni haya matatu. La kwanza, mchango wa *diaspora* katika uchumi wetu; la pili, dhana ya Tanzania kuwa *logistics* na *transit hub*; na la tatu, ushiriki wa Watanzania kwenye uwekezaji wa rasilimali zetu. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, *diaspora* ina mchango mkubwa sana katika chumi za nchi. Kuna *study* ambayo nimeitazama ya mwaka 2018, katika nchi nne; Nigeria, Kenya, Uganda na sisi Tanzania. Mwaka 2018, fedha zinazotoka kwenye *diaspora* kuingia Nigeria, zilikuwa Dola bilioni 23.6 sawa na asilimia 6.1 ya *GDP* ya Nigeria. Kwa ule mwaka *diaspora* ili-*contribute* fedha nyingi kushinda *export* ya mafuta. Nigeria ndiyo nchi ya nne ulimwenguni kwa ku-*export* mafuta. Hata hivyo, Wanaijeria waliokuwa nje wameleta fedha zaidi ya mara mbili ya *export* yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya mwaka 2018, *contribution* ya *diaspora* ni Dola bilioni 2.72 sawa na 3% ya *GDP* yao. Uganda mwaka 2018 imeingiza Dola bilioni 1.24 sawa na asilimia 4.5 ya *GDP* ya Uganda. Mwaka huo huo Tanzania tumeingiza Dola milioni 430, sawa na 0.8% ya *GDP* yetu. Bayana kabisa, sisi kama Tanzania hatujalea hii sekta muhimu ambayo inaweza kuwa mchango mkubwa sana katika maendeleo yetu na katika Mpango wetu wa Miaka Mitano. Hii sekta ni lazima ilelewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haki fulani fulani ambazo zinakuwa vichochezi. Kwa mfano, Mkenya mwenye *passport* ya nchi nyingine hadhibitiwi kununua ardhi. Halikadhalika na Uganda, lakini Tanzania huwezi. Sasa naiomba Serikali iyatazame haya, tuweze kuwapa hawa *incentives* ili sekta hii, hawa watu, Watanzania wameamua kuishi nje, washiriki na watusaidie katika mchango wa uchumi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tumejenga miundombinu mikubwa sana katika sekta ya *transport: SGR*, barabara nyingi, tumeboresha bandari na nyingine tunaziongeza; dhamira yetu siyo tu kuiendesha Tanzania bali kusaidia nchi zilizokuwa jirani. Tanzania inapakana na nchi tisa. Mbili tu kati ya hizo tisa zina *access* ya bahari ya hindi. Mbili tu; Kenya na Msumbiji. Saba hazina; na zote hizo saba, kuna *advantage* kubwa sana kwa wao kupitisha mizigo yao kwetu. Uganda, Rwanda, Burundi, Congo, Malawi, Zambia, wote wana *advantage* kubwa na ndiyo *distance* fupi, hupiti

katika nchi nyingine. Ikitoka baharini inapita Tanzania, inaingia kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *advantages* zote *strategically* tunazo. Kwa nini hawazitumii? Mambo magumu yote Serikali ya Awamu ya Tano imeyafanya. Upungufu wetu ni katika yale mambo mepesi (*soft skills*). Yapi hayo? *Customer service*; urasimu. *Civil service* kwa kijeshijeshi badala ya kuwa kirafiki na kibiashara. Haya mambo mepesi lakini thamani yake ni kubwa mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashauri Mawaziri wa sekta, hilo jambo walitazame kwa macho makini ili tukuze uchumi na mpango wetu utimie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni ushiriki wa Watanzania kwenye uwekezaji. Serikali hii kwa nia njema kabisa inataka Watanzania tumiliki rasilimali zetu zilizokuwa kubwa. Sheria zilizopitishwa kwenye *Extractive Industry*; madini, *oil and gas*, sasa Tanzania ina hisa asilimia 16 katika kila *investment* kubwa ya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu vinaitwa *mutual farms au collective investment schemes*. Hii ni mifuko tu; maneno makubwa tu haya ya Kiingereza, lakini ni mifuko ya kuwachangisha sekta binafsi washiriki kwenye miradi ya mkakati. Kunakuwa na mfuko maalum, mnasema pengine Kabanga *Nickel*, mahesabu yake haya; Kabanga *Nickel* tunajua ina idadi gani? Faida yake ni hii. Nyeie mnaotaka kuchangia na mkawa na hisa, karibuni. Hiyo ndiyo njia sahihi ya kuongeza *ownership*.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa badala ya 16 tu ile ya Serikali peke yake, Watanzania sisi katika sekta binafsi, pamoja na wale wa *diaspora* walioko nje, wanaweza waka-*invest tuka-own* zaidi na ile fedha ya faida ikawa *repatriated* kwenda nje ikabaki hapa hapa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ABDULLAH ALI MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimemwongezea dakika Mheshimiwa Abdullah Mwinyi kwa sababu pamoja na mambo mengine alikuwa Mbunge wetu wa Afrika Mashariki. Kwa hiyo, anapojunga na Bunge letu sasa basi anatuletea baadhi ya mambo ya kutoka kule. (*Makofi*)

Tunakushukuru sana kwa mchango wako mzuri na hasa jambo la *customer care*. Iko haja kubwa sana watumishi wa Serikali kufundishwa *customer care*. Sijui mfanyeje, yaani mahali pengi iwe ni mahospitalini, iwe mashuleni, yaani *customer care* inakosekana sana, yaani mtu akishakuwa Afisa wa Serikali anafikiri yeye ni mtu wa kuamrisha na kuburura. Kumbe mwanafunzi ni mteja wa mwalimu; mgonjwa ni mteja kwa mtumishi wa huduma ya afya. Mtu yeyote anayeonekana kwenye Ofisi ya Serikali huyo ni mteja, kuna namna ya kum-*treat*. (*Makofi*)

Hata *TRA* itambue kwamba inaowadai kodi ni wateja pia. Tena *TRA* ndiyo inahitaji kweli *customer care*, ndiyo maana wanalalamikiwa kila wakati. Wakati mwingine wako sahihi, lakini ile *approach* ni *hardline* sana.

Nilikutaja Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mheshimiwa Asia Halamga atafuatia, halafu Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu kwenye Bunge hili. Kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote na kwa Taifa na sisi Watanzania wote. Pia nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoongoza Taifa letu toka kipindi kilichopita na sasa. Vile vile nawapongeza wachangiaji wote wa leo kupitia Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sitachangia mpango huu, naomba univumilie, nizungumze kama Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mji, lakini pia kama Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mchango wangu ni mdogo sana. Kwanza, ni namna gani ambavyo wananchi wangu wa Jimbo la Mbulu Mji wanapata tabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kigugumizi cha kuzungumza suala la *Corona*. Jimbo langu wamepotea nikiwa huku Bungeni kwa mwezi mmoja watu wengi kidogo. Ukanda ule ni wa baridi. Naomba niishauri Serikali, tumekuwa na matumizi ya dawa za asili, tumekunywa kama gongo, yaani tunakunywa tu bila kujua hali halisi ikoje. Ni kwa nini Serikali isichukue jukumu la kuchukua dawa zote za Waganga wa Asili ikapeleka kwa Mkemia Mkuu wa Serikali halafu ikaja na kauli ya kutuambia angalau ni dawa zipi tuweze kutumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu inaonyesha vifo vilivyotokea kwenye Jimbo langu, sehemu kubwa vina viasharia vya mtu kushindwa kupumua, maumivu ya kifua na hali kadhalika. Nimekwenda Jimboni, nikaja kwako mara kadhaa kuomba kibali, wakati mwingine nimetoroka hata bila kuja kwa sababu nakwenda Jimboni, narudi; nafika huku mtu wa karibu amefariki, narudi tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza sana Waganga wa Asili waliochemsha miti shamba wakanywesha Watanzania. Waheshimiwa Wabunge tuliokuwa na kigugumizi, asilimia kubwa tumeshakunywa; nami nimeshakunywa. Ni kwa sababu sikubaliani na chanjo ya watu wa Magharibi, lakini nakubaliana na naamini dawa za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inashindwa nini kutumia wataalam wa ndani na vyombo tulivyonavyo kufanya utafiti ili angalau hizi dawa za asili sehemu fulani tujue ina msaada? Kwa sababu Jimbo langu la Mbulu watu wanapata matatizo. Hata leo niliitwa kwenda kuzika mtoto wa Diwani, nikawaambia jamani, Bunge liko ukingoni, ninyi

muendelee tu. Ukiuliza, dalili ni hiyo hiyo; na ukanda wetu una baridi. Hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, majaribio haya ya dawa za asili ambayo tunakunywa kutoka Bunge lililopita na Bunge hili la sasa, mimi nimekunywa, sijui wengine, lakini naona matokeo yake ni chanya katika kutatua tatizo hili. Je, ni kwa nini basi kama hatuna wataalam au vyombo tusiagize hata wataalam wa nchi nyingine na vyombo nchi nyingine tufanye utafiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza haya kwa sababu nina machungu. Itafika mahali hata hao wanaotupima hapo getini, Manesi wanaotuhudumia hospitalini; juzi nilienda Benjamin Mkapa kupata vipimo nikaambiwa Mheshimiwa mitungi haitoshi. Mitungi ya *oxygen* Benjamin Mkapa haitoshi. Pia mashine za *oxygen* hazitoshi. Najua kuna watu watanielewa vibaya, wacha wanielewe vibaya, mimi nimepewa dhamana ya kuja kuzungumza hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao watumishi wa Afya hatujajiweka vizuri namna ya kuwalinda, namna ya wao kuwa na imani. Dawa hizi za mitishamba tunazokunywa ni ghali sana. Ni kati ya shilingi 30,000/= mpaka 50,000/=. Mwananchi wa kawaida hawezi. Je, haiwezekani Serikali ikachukua jukumu la kufanya utafiti angalau kwa dawa zetu? Siyo lazima sisi tuamini vitu vya watu wa ng' ambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kabisa Tanzania tuna hazina kubwa ya dawa za asili. Tatizo letu ni namna ya kuzichambua ili tujue ni dawa gani zina mchango kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu la Mbulu Mji lina Hospitali ya Mji ambayo iko katikati. Ina vituo vya afya lakini hawana mashine hiyo ya *oxygen*, hawana mitungi na watu wanakufa. Wanapokufa kwa ugonjwa huu pengine wa kifua au kushindwa kuhema, mashine hizo zingeweza kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita siku pata kuchangia, nilikuwa naenda Jimboni nazika, narudi; nafika hapa, narudi naenda kuzika; ifike mahali niseme wazi tu kwamba hali halisi ikoje. Kwa Mbulu, ukanda ule ni wa bonde la ufa. Juu ya bonde la ufa kuna baridi sana. Mwezi wa tatu, wa nne, wa tano, wa sita na wa saba, mafua haya yatakuja tu na watu watapata shida.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, lakini naomba mitungi hiyo ipelekwe katika Hospitali ya Mbulu na hospitali nyingine nchini na vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Polepole, alisema, *Corona* ataishi Tanzania kwa adabu na sasa anaishi kwa adabu, lakini kwa kutegemea dawa zetu tulizonazo na mifumo yetu tuliyonayo na maombi yetu tunayoomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali, hospitali za wilaya, vituo vya afya, wapelekewe hiyo mitungi isaidie.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umenionea, sijamaliza dakika kumi.

**MWENYEKITI:** Ni dakika tano tano.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Ni tano?

**MWENYEKITI:** Eeh, ni tano.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Mpango uliokuwa umejadiliwa na wenzangu. Ila hili ombi langu lifanyiwe kazi kwa nchi nzima. Tunalo tatizo, tusifiche.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lipo tu, kwa heshima na taadhima nikwambie. Maana sisi tuliko huku tusifikiri siku moja hatutakuwa wananchi. Tutakuwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono Mpango wetu ulioletwa kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharia. Nilikuongezea vidakika, nilikuwa natambua uchungu ulionao na shida uliyokuwa unaijeleza, natambua kabisa; na msisitizo kwamba kule kuna baridi. Sasa Waheshimiwa Wabunge wakati mwingine hamwelewi, yaani kukiwa na baridi si mnaelewa kuhusu utaratibu! Sasa na kuambukizana kunaongezeka. Maana kwenye baridi lazima watu wasogeane. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Asia Halamga, halafu Mheshimiwa Vita Kawawa.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo wa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri ambazo anazifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri wa Mipango pamoja na timu yake yote, bila kusahau Kamati ya Bajeti kwa hotuba yao nzuri waliyotuletea. Naomba nijikite kuchangia katika eneo la kilimo na hasa kilimo cha ngano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Manyara kupitia Wilaya ya Hanang ni miongoni mwa sehemu inayolima ngano kwa asilimia kubwa. Nikichukua takwimu za Serikali ambazo zimetumia fedha ya kwenda kununua ngano katika msimu uliopita, Serikali ilitumia zaidi ya shilingi trilioni 1.3 kwa ajili ya kununua zao hili la ngano na kuliingiza nchini. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaweza kuipongeza Wizara ya Kilimo kwa kuamua sasa Wilaya ya Hanang kuwa kitovu cha kilimo hiki cha ngano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba sasa zao hili na kilimo hiki katika Mkoa wa Manyara, hususan Wilaya ya Hanang, tunaomba sasa Serikali ichukue hatua ya kuleta mbegu kwa wakati na kwa haraka kama ambavyo imetufanyia kwa sasa kutuletea tani 22 kwa ajili ya mbegu. Naiomba sasa Serikali kupitia mnunuzi ambaye iliamua awe Bakhresa kuja kununua ngano hizi za wakulima zaidi ya tani 477.8 ili wakulima hao waweze kukidhi kilimo chao kwa wakati na tuweze kwenda sambamba na uchumi wa viwanda kupitia malighafi watakazozitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Hanang ina ekari zaidi ya 100,000 ya kilimo cha ngano. Pamoja na ekari hizi, ekari 40,000 ziko kwa mwekezaji anayeitwa *Ngano Limited*. Tunaomba sasa, kwa sababu Serikali imeamua Hanang iwe kitovu cha ukulima cha ngano ili kuweza kukidhi mahitaji ya ndani ya nchi, mwekezaji huyu wa *Ngano Limited* mikataba yake iweze kuangaliwa kwa sababu anamiliki ekari zaidi ya 40,000 lakini halimi kiwango hicho cha ekari 40,000 na ekari hizo zilikuwa ni pori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Hanang wanatamani kweli kulima ngano ili kukidhi haja ya Serikali, lakini tunaiomba Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, iweze kumsaidia mwekezaji huyu mkataba wake, kwa sababu eneo allionalo ni kubwa na limekuwa ni pori. Kama tumeamua kweli kuwekeza katika ngano, basi ikiwezekana shamba hilo liletwe katika halmashauri, halmashauri ilimiliki kwa maana ya Serikali au wananchi waweze kugaiwa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji huyu anamiliki eneo la Gidamocha, Sechet pamoja na Murjanda. Wananchi wanapolingia kulima hata kidogo tu, mwekezaji huyu anakwenda kuweka mazao sumu, mazao ya wananchi yanakufa, lakini pia halimi eneo hili la ekari 40; na lengo la Serikali ni kuhakikisha tunafikia...

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukuza uchumi, naipongeza Wizara ya Habari, Sanaa na Utamaduni kwa kazi kubwa ambayo inafanya, lakini naomba sasa Wizara ifike mahali iweze kuwasaidia wasanii wetu. Kwa sababu ni ukweli usioplingika, wasanii wanaingiza mapato. Vijana pamoja na ninyi wazee humu ndani mnapenda burudani, basi ifike sasa, Wizara iweze kuona ni namna gani inaweza kuwasaidia vijana hawa ku-*promote* kazi zao na hasa kimataifa ili wasanii hawa waweze kukubalika Kimataifa kama ambavyo Nigeria na nchi nyingine zinavyofanya. Wasanii wetu wana uwezo mkubwa wa kuliingiza Taifa letu pato kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania Mungu ametubariki sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda, ndiyo nilikuwa nimeanza. Naunga mkono hoja. Naendelea kumshukuru Mwenyekiti wetu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa huruma ya Serikali na hata leo Serikali hii kwa huruma yake, ina hadi watu ambao walifukuzwa kwenye vyama vyao, lakini Serikali kwa sababu imezingatia maslahi ya Watanzania imeweza kuwaweka humu ndani ili kuendelea kuchukua michango yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nasema tena, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vita Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Mpango wetu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nia na lengo la Mpango wetu huu ni kuendelea kukuza uchumi, kupambana na umaskini na ku-*maintain* hali ya nchi kuendelea kuwa nchi ya kipato cha kati lakini kuelekea kwenye *higher middle income*. Hii ina maana Mpango una malengo ya kuleta ustawi wa watu wake na kuongeza kipato cha chini na uchumi wa jamii na kuleta ajira zilizo rasmi na zisizo rasmi. Ili kuleta ustawi mimi nashauri Mpango uende sambamba na utekelezaji wa miradi ya utoaji huduma iliyokusudiwa katika Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika katika Mpango uliokwisha. Serikali imewekeza kwa wingi sana kwenye miradi mkakati au naweza nikasema *product capacity project* kubwa, reli, umeme, viwanja vya ndege, barabara na kadhalika. Katika eneo hili la umeme imewekeza sana, leo tunao umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji yeyote anayewekeza anatakiwa lazima pia afahamu anatakiwa apate kile alichowekeza na Serikali imewekeza umeme ili kusaidia shughuli za kiuchumi kuanzia chini. Hapa nashauri Mpango uangalie uwezekano wa ku-*trickle down economic activities* katika maeneo ya vijijini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakulima tunalima lakini kazi yetu tukishalima mara moja tunauza basi, watu wanakaa wanasubiri mwaka unafika. Sasa umeme umefika vijijini, Mpango lazima uangalie kuhamasisha sekta binafsi kuona uwezekano wa kuleta viwanda vidogo kule vijijini lakini pia wale wawekezaji wengine waliokuwepo hapa kuona uwezekano wa kuanzisha viwanda vya kuwekeza kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namfahamu kijana ambaye anatambulika na *SIDO*, NYUMBU pia wanamtumia, amesoma

Urusi na Uchina, yeye ana-*assemble* viwanda vidogo vya kutengeneza mafuta haya ya michikichi na pia anatengeneza viwanda vidogo vya kutengeneza sabuni. Ushauri wangu Serikali iwe na mpango wa kushawishi makampuni makubwa yanayoweza kuingiza viwanda vidogo kwenye vijiji vyetu ili wanaozalisha alizeti wakachakata alizeti, wanaozalisha mpunga wakakoboa mpungu. Hii itasaidia kuwa na *activities* za mwaka mzima pale, wa kuchakata mpunga, pumba za mpunga zitatumika kuchomea tofali; unga wa pumba za mpunga utaingia katika viwanda vya chakula cha mifugo na pia tutaendelea kuuza mali ambayo imeongezewa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuuangalie jinsi gani ya kupata wawekezaji wakubwa wanaoweza kuingiza viwanda hivi vidogo. China kuna viwanda vidogo na vya kati ambavyo vinauzwa kuanzia Dola 3,500 mpaka China. Sasa tukiweza mazingira mazuri kwa wafanyabiashara wa sekta binafsi wakaweza ku-*import* hizi tukapeleka huko vijijini, tukaondoa *mentality* sasa hivi ya kijijini mtu akistaafu, mtu akiwa mwalimu au mtumishi wa Serikali, akikopa ananunua pikipiki ndiyo anafanya biashara, kwa hiyo, biashara yake ni ya *service*. Sasa tutoe *mentality* zile wawekeze kwenye viwanda vidogo hivi vya uzalishaji ambavyo vitaajiri vijana wetu waliokuwepo kule vijijini na tutaongeza thamani ya mazao tuliyonayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naomba nizungumzie ustawi wa shughuli zetu za kiuchumi, kilimo na mifugo. Leo kuna mifugo 33,000,000 na inasambaa tu na inasumbuana na wakulima lakini sasa hivi imefikia mahali inasumbua pia Hifadhi za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alielekeza katika hotuba yake humu Bungeni kwamba watatenga hekta milioni 6 kwa ajili ya kuweka *blocks* za wafugaji ili waweze kufanya shughuli zao vizuri na wasiteswe, hili ni jambo zuri kabisa. Naomba sana hili lifanyike kwa sababu wafugaji wanaingiliana sana na wakulima. Leo hii sisi kwetu Namtumbo wafugaji waliondolewa Morogoro wameingia Namtumbo

sasa hawana mahali maalum, wako ndani ya hifadhi na wako ndani na wakulima.

*(Hapa kengele iligonga kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mpango utenge ardhi kwa ajili ya hawa wafugaji ili kuleta ustawi katika maeneo yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa. Nilikutaja Mheshimiwa Cecilia Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela atafuata.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie.

**MWENYEKITI:** Dakika tano.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie katika hoja iliyoko mbele yetu kuhusiana na Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni kama desturi au taratibu zinatutaka tupitithe Mipango hii na mara nyingi imekuwa ni Mipango mizuri sana kwenye maandishi na imekuwa ni Mipango mingi kwa mara moja lakini ukija kwenye utekelezaji ndipo ambapo kunakuwa na changamoto kubwa. Utekelezaji umekuwa ni hafifu kwa sababu kwanza tumekuwa na mipango mingi ndani ya mwaka mmoja wakati tunaambiwa hako kasungura tunakokusanya nako ni kadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora tuwe na Mipango michache ambayo inahusiana moja kwa moja na maisha ya mwananchi wa kawaida, tukaitekeleza kwa ufanisi, tukamsaidia yule mwananchi wa chini kabisa maskini.

Tukipitisha mipango tukaenda kupitisha na bajeti maana yake fedha zitolewe na bajeti hiyo iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, tunapitisha mipango mbalimbali kwenye sekta zote muhimu zinazomgusa Mtanzania mfano ya kilimo, maji, viwanda, afya, yote kwa namna moja au nyingine inamgusa mtanzania wa chini kabisa. Hata hivyo, tukipitisha Mipango hii ukija kwenye kuangalia namna gani bajeti zinapitishwa kwenye Wizara hizi haiendani kabisa na kile ambacho tumekipitisha. Fedha hazitolewi kwa wakati, wakati mwingine hata kikitolewa hicho kidogo kinafika kwa kuchelewa maana yake kile tulichokipitisha basi kinakuwa ni kama hakuna kwa sababu hakuna matokeo ambayo yanafikiwa kulingana na kile ambacho tumekipitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la mfumuko wa bei, ukisoma Mpango hapa unaeleza kabisa kwamba mfumuko wa bei Serikali imeendelea kudhibiti. Uhalisia sidhani kama iko hivyo, inawezekana imedhibitiwa kwenye makaratasi lakini tukitoka nje ya jengo hili huo mfumuko wa bei unaosemwa haujadhibitiwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Desemba mwaka jana mpaka leo hii January tunapooonea kuna mfumuko mkubwa sana wa bei ya bidhaa. Mfano, unga wa ngano wa kilo 50 ilikuwa inanunuliwa kwa Sh.60,000 leo unanunuliwa kwa shilingi 69,000. Unaenda kwenye mafuta ya kula ya lita 20, yalikuwa yananunuliwa kwa shilingi 52,000 leo yananunuliwa kwa shilingi 82,000. Ukienda kwenye bidhaa za ujenzi, vivyo hivyo, bati zimepanda bei, saruji ndiyo usiseme. Saruji sio tu kupanda bei, yaani saruji imekuwa bidhaa adimu ndani ya nchi hii na tuna viwanda. Saruji ilikuwa inanunuliwa kati ya shilingi 13,000 au shilingi 14,000 leo unaitafuta kwa shilingi 17,000 mpaka shilingi 28,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukisoma Mpango, Hali ya Uchumi wanakwambia mambo ni mazuri, Serikali ya wanyonge inasema hakuna mfumuko wa bei mambo yako sawasawa. Sasa, mambo kweli yako sawasawa kwenye

makaratasi lakini hayako sawasawa tukitoka nje ya hapa. Bati za geji 8 zilikuwa zinanunuliwa kwa Sh.62,000 leo zinafika Sh.70,000 na zaidi. Nadhani yale mnayoyanena kwenye makaratasi basi yanenwe kwa vitendo huko nje tunakotoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la mfumuko wa bei nadhani lipatiwe ufumbuzi sasa hivi halisubiri bajeti. Mtuambie, Watanzania huko nje wanataabika, mambo ni magumu, kila kitu kimepanda bei hatuelewi ni kwa nini kimepanda bei na bidhaa nyingine hazipatikani kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ambayo napenda kuichangia ni kuhusu wafanyabiashara. Wafanyabiashara wa nchi hii imekuwa kama ni ule mchezo wa paka na panya. Ni mchezo wa kuviziana, wa kutafutana. Leo wafanyabiashara wa nchi hii wako wengine ambao wanaamua kufunga biashara kwa sababu mazingira ya ufanyaji wa biashara siyo rafiki hata kidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa Dodoma hivi tunavyoongea kuna wafanyabiashara wengi tu wameshaandikiwa barua na TRA; wengine wanataka kufungiwa akaunti na wengine wanaanza kufikiriwa kupelekewa hiyo *task force* ya kuangaliwa kodi ya miaka mitatu nyuma. Kuna wafanyabiashara kule Karatu wamepelekewa hizo *task force* zinawachunguza eti wanachunguzwa mapato yao kwa miaka mitatu nyuma yalikuwaje wakati huyu mtu analipa kodi yake kila mwaka hajawahi kukwepesha kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaambiwa mashamba hayatozwi kodi, Karatu kule kuna wafanyabiashara kwenye Bonde la Eyasi wanalima vitunguu, wote wameambiwa wanapelekewa hiyo *task force* inachunguza kwa miaka mitatu namna gani wanalima, mapato yao ni nini, wana wafanyakazi kiasi gani, wanatakiwa kulipa nini na kwa nini hawajalipa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wote wanalima mashamba ya vitunguu, lini tumeanza tena kutoza kodi mpaka mashamba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ushauri wangu kwa Serikali.

**SPIKA:** Muda wako umeisha.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kidogo tu nimalizie, ili uweze kuongeza mapato ni kuwatengenezea wafanyabiashara mazingira rafiki na unapunguza kodi, ndivyo ambavyo utapata kodi nyingi. Ukiongeza kodi unafukuza na kufunga biashara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso. *(Makofi)*

Nilishakutaja Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, utafuatiwa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uzima na zawadi ya kuwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Rais ambaye amefanya mengi na ambaye tunategemea ataendelea kuyafanya mengi kwa kipindi cha miaka mitano iliyobaki. Pia nishukuru sana viongozi wenzake Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pekee ziende kwa watumishi wa umma Tanzania nzima. Hawa ndiyo

wanaotekeleza mipango ambayo sisi tunaipanga hapa na kama ambavyo wamemsikia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba wasiwe na wasiwasi Serikali yao inawapenda na kama alivyosema Mheshimiwa Rais yeye haongezi vibaba vibaba ataongeza mzigo wa kutosha, kwa hiyo, waendeleo kushirikiana nasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, lipo jambo nimeliona hapa. Wakati najiandaa kuchangia hapa, nimesoma kwanza Mpango uliopita yale mapendekezo yaliyoletwa humu Bungeni, nikasoma *Hansard* za Wabunge walivyochangia na nikapitia kwenye changamoto ambazo zimesababisha Mpango ule usitekelezwe kwa asilimia 100, nikajifunza kitu ambacho naomba sasa wakati Waziri anakuja kuhitimisha atuambie hapa ni kwa asilimia ngapi hii michango ya Wabunge hapa inaenda kufanya mabadiliko kwenye rasimu hii tunayojadili na kuleta Mpango ulio kamili? Tusipopata asilimia ya namna ambavyo michango yetu inaingizwa kwenye Mpango huu na mabadiliko yakatokea tutakuwa tunazungumza hapa halafu hayafanyiwi kazi. Kwa hiyo, niombe sana wakati anakuja kuhitimisha atuambie michango yetu imeingizwa kwenye Mpango huu kwa asilimia ngapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo lingine, wote hapa tunasema, hata dada zangu kule wanakiri kwamba Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri mno ya kutukuka lakini swali langu, hii kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Rais itakuwa *sustainable*, itaendelea kuishi? Hii miradi mikubwa inayoanzishwa na Serikali itaendelea hata kama yeye hayupo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachokishauri sasa tuweke mifumo ambayo itasaidia hizi shughuli nzuri zinazofanywa ziendeleo kuishi. Hapa kuna wanasheria na Mwanasheria wa Serikali atusaidie, huko kwenye nchi zilizoendelea wana vitu vyao kama *interest* za Taifa lao, hivi hapa Tanzania hatuwezi kuwa na mambo yetu ambayo ni *interest* ya Tanzania na yakae kwenye Mpango wa muda mrefu hata kama ni miaka 50 kwa kuanzia baadaye twende miaka 100 ili tuwe na



Mipango ya muda mfupi ya mwaka mmoja kama tunavyojadili sasa hivi lakini tuwe na Mipango ya miaka mitano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu tunafahamu namna siasa zetu zinavyoenda. Mara nyingi unakuta viongozi wanacheza *beat* kulingana na mpigaji anavyopiga ngoma. Sasa tunataka tutengeneze ngoma ya Watanzania ambayo tunaweza kuipiga kwa kipindi cha miaka 50 tuone hayo mambo ambayo yamewekwa yawe ni msingi na yaendeleo. Namna ya kuyafanya yawe endelevu ni sisi Wabunge kuweka sheria za kubana lakini pia kuwa na taasisi ambazo ni *strong* zinazoweza kufanya maamuzi na kuyasimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo tutakuwa tumemfaidi Mheshimiwa Rais tuliyenaye sisi wa kizazi hiki na kizazi kijacho. Tukiacha haya, iko hatari kwamba akiondoka Mheshimiwa Rais na haya yataondoka, atakuja mwingine tutacheza ngoma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia hebu tutazame mfumo wa elimu ya Tanzania, je, unatupa *output* nzuri kwa watu wetu? Wapo Wabunge wamechangia hapa na utaona kuna kitu ambacho tunakifanya. Sisi tuna-*base* kwenye kuangalia mazingira zaidi lakini ubora wa elimu bado hatujauweka vizuri. Je, mtaala tulionao una-*reflect National objectives* maana yake ni kwamba hii Mipango ya Taifa tunayoipanga tukienda kwenye mitaala yetu tunaikuta? Tunataka Serikali ya viwanda, je, mifumo ya elimu inatupeleka huko kuandaa watu waje wafanye kazi kwenye viwanda hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe pia wakati tunapanga Mipango hii tutazame pia suala la mitaala yetu. Kwa sababu moja ya changamoto iliyosababisha Mpango ule usitekelezwe kwa asilimia 100 ni kwamba nchi hii hatuna wataalam wa kuandika maandiko. Hii siyo sawa, watoto wanamaliza vyo kila siku tunawezaje kuweka *challenge* kama hii, kwa hiyo, kuna shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine hapa tunaangalia michango yetu na hili siyo zuri sana ninavyolitazama mimi. Nitoe mfano mtoto wangu aliniuliza swali juzi hapa, akaniuliza baba hebu niambie, mle Bungeni kuna Mbunge anaitwa Musukuma na Mbunge mwingine wa Kahama, wanachangia vizuri kweli lakini wao wanasema darasa la saba. Zaidi ya hivyo, tunaambiwa wamefanikiwa kwenye maisha, hivi kuna sababu ya kusoma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili swali ingekuwa ni wewe, ungemjibuje mtoto akikuuliza kitu cha namna hiyo? Iko sababu ya kupita kwenye mfumo wa elimu ili tuweze kuwa na wataalam ambao wana *output* nzuri. Hata hii tunayosema kuwa sisi tuna sera nzuri, sera nzuri ni ile ambayo ina *strong tools of implementation* ambazo zinaleta *output* nzuri. Kwa hiyo na hili pia tunapoangalia tulitazame. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nimetaka kuchangia ni kwenye kilimo.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda hauko upande wako Mheshimiwa.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo...

**MWENYEKITI:** Dakika tano tayari zimeisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nilikuwa naanza? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa dakika moja tu tafadhali sana, kwa kuwa Jimbo la Hai lilifanya kazi kubwa sana, naomba niongezee.

**MWENYEKITI:** Haya, dakika moja.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwenye eneo la kilimo. Pale Hai tukiamua kuna vyanzo vya maji vya kutosha, kuna ardhi nzuri tuko tayari kufanya kazi. Tukipewa vyanzo hivi vya maji tutalima na tutachangia kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye Vyama vya Ushirika, kaka yangu Mheshimiwa Nape tumezungumza sana, iko shida. Kule Hai hatuna ardhi ya kutosha lakini tuko tayari kufanya kazi lakini Vyama vya Ushirika vimekumbatia mashamba yetu, wanachokifanya mle ndani hatujui, ukiwaambia ni wataalam wa kufanya *lobbying* za kutosha. Tafadhali sana ile *team* niliyoomba iende kule Hai, Mheshimiwa Waziri Mkuu uko hapa, iko shida, uko utajiri mkubwa kule Hai kama tukiamua kufanya kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Saashisha. *(Makofi)*

Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Anne Kilango.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi. Kwanza naomba nizungumze kwamba, naipongeza sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Tangu Awamu ya Tano imeanza wote tunashuhudia kazi zinazofanywa na Serikali. Nina uhakika wote ambao tuko *sobber* tunaona kwamba, Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi inafanya kazi kubwa sana. Naomba nichukue nafasi hii niipongeze na sio mimi na wananchi wangu wote wa Jimbo la Same Mashariki wanapongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuzungumzia sehemu mbili ambazo zimeongelewa vizuri kwenye mpango, viwanda, lakini pamoja na kilimo. Naomba mimi niviunganishe hivi vitu viwili, viwanda na kilimo. Niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano kuisitiza sana na kutuwezesha kufungua viwanda; viwanda vidogo, viwanda vya kati, viwanda vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi vyote vinavyofunguliwa Tanzania vinasaidia sana kilimo kwa sababu, vinachukua malighafi kutoka kwenye kilimo chetu, nafikiri hapo nimeeleweka, lakini kuna tatizo kubwa ambalo tusipoangalia vizuri tutakwenda tunajenga viwanda kwa nguvu sana baadaye vitakosa malighafi. Naomba nizungumzie kule ninakokuona, tumejenga kiwanda cha tangawizi, kile ni kiwanda kimejengwa na wananchi na Mbunge aliyekuwepo madarakani wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi tumefika tumeungana na *PSSSF* ni mbia wa kiwanda cha tangawizi sio kwamba, ameleta mitambo, ni mbia wa Kiwanda cha Tangawizi cha Mambamiamba, naomba mnielewe vizuri ninalozungumza. Sasa hili jambo tuliangalie kwa nchi nzima, kiwanda kile kilipofika pale Same Mashariki nakiri kinakwenda kupanua kilimo cha tangawizi kwa sana. Wananchi watakuwa wana mahali pakuuzia tangawizi tena sio Same Mashariki tu na Same Magharibi watalima mpaka tukija Mlalo watalima, Lushoto watalima, Tanga watalima, kiwanda kiko pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo nililoliona maana kwa sisi viongozi tuwe tunaangalia huku na huku, tutafute kila njia Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu namnyenyekea, watafute kila njia ya kwenda kuhakikisha miundombinu ya kilimo cha tangawizi inakuwa inayofanya wananchi waweze kulima kile kilimo. Sasa hivi wanaolima tangawizi kule kwangu ni wengi mno, nilianza na kata mbili, nikaja kata nne, sasa ni tarafa tatu zote za jimbo langu, wote wanalima tangawizi; miundombinu ya kilimo imekuwa haiwatoshelezi. Mifereji imekuwa ni midogo, mito imekuwa haina uwezo tena, lakini bado kuna uwezekano wa kuboresha miundombinu ya kilimo kama Serikali ikija kule na kuangalia hali halisi. Kuna sehemu ambazo zinawezekana kuchimbwa mabwawa makubwa wakati wa mvua maji yakajaa, mvua zinapokuwa hazipo mito ikapata maji kutoka kwenye mabwawa yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namnyenyekea Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri wa Kilimo ni mwepesi sana, namkaribisha.

Baada ya Bunge hili twende naye kule kwangu akaone hali halisi ya kuboresha miundombinu ya kilimo kwa ajili ya tangawizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye mpunga ni hilo hilo, nina tarafa inayolima mpunga. Tarafa ya Ndungu kuanzia Bendera, Kihurio, Ndungu, Maore ni mpunga, lakini miundombinu ya kilimo imechoka. Sijui kwa majimbo ya wenzangu, lakini miundombinu ya kilimo Same Mashariki, Same Magharibi ni jirani yangu hata yeye ana hilo tatizo. Naomba Serikali itusaidie kuja kutuangualia kwa sababu, bila ya kilimo hata hivi viwanda tunavyovizungumza itakuwa havina malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kuzungumza hilo tu. Nashukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika Mpango huu wa Mwaka Mmoja, lakini pia wa Miaka Mitano inayokuja. Kipekee kabisa nikupongeze kwa namna unavyoendesha Bunge hili, kikao hiki. Hakika unatutendea haki kama Wabunge na tunafurahia uendeshaji wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu dakika tano ni chache, lakini namuomba Mungu aniongoze ili niweze kuongea vyema kwenye suala la *TANESCO*, suala la nishati kwa ujumla, lakini pia, suala la *TRA*. Hakuna changamoto kubwa ninayoipata katika Mkoa wangu wa Songwe kama kusikia umeme umekatika, umeme hauna nguvu, umeme hautoshi, hakika wanavyokuwa wanaelezea wananchi kule huwa inasikitisha sana. Unakuta mwananchi ana ofisi, ofisi yake inategemea umeme. Analipa pango, analipa gharama

nyingine zote, lakini mwisho wa siku anachokipata anakuta ni kichache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika kusema hayo nasema gharama za uendeshaji wa umeme katika nchi yetu bado ni za juu. Ukiangalia kwa upande wa *TANESCO*, ni baskatika suala la *domestic electricity*, gharama inayolipwa kwa kila *watt below 75* ni shilingi 100. Gharama inayoenda kulipwa *above 75 kilowatts* ni 350, hapa sijazungumzia suala la *industrial electricity*. Tunapongelea ushindani wa soko na Mheshimiwa wetu Rais amejitanabahisha kuwa sera yake kubwa ni kuifanya nchi ya Tanzania iwe nchi ya viwanda na tunajua viwanda haviwezi kuendelea pasipokuwa na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia kwa namna gharama hizi za umeme zinavyokuwa na nikiangalia soko la bidhaa zetu tunakotaka kuzipeleka, unakuta wakati mwingine tunawapa wakati mgumu wajasiriamali wetu na wawekezaji kwenye ushindani wa soko katika mataifa mengine. Nitarejea katika mfano mdogo tu wa sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme kwetu sisi Tunduma hatuna shida sana na sukari kwa sababu, tuko mpakani tunatumia sukari ya Zambia. Wakati mwingine nawaza kwamba, inakuwaje nchi ndogo kama Zambia inatushinda sisi Tanzania kwenye uwekezaji wa sukari mpaka inaanza inafanya *supply* kwetu katika kanda zetu za mpakani kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari Zambia inauzwa Sh.2,000 ukija huku kwetu sukari inaenda hadi Sh.3,000. Sasa unapongelea shilingi 3,000 na sidhani kama kuna Mtanzania yeyote humu ndani asiyependa kitu cha bei rahisi, hata kama tunasema ni uzalendo hauwezi ukaenda kwa *style* hiyo kwamba, nafanya uzalendo huku naumia. Kwa hiyo, niombe, niombe kwanza Bodi ya Sukari itafute namna ya kuifanya biashara ya sukari kama fursa ya kuipatia Serikali pesa. Kama watawekeza vizuri na kama pia watu wa nishati watatuonea huruma kupunguza gharama za uendeshaji wa viwanda

naamini nchi yetu inakoenda itakuwa ni nchi ambayo ina mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Zambia nchi ambayo ni ndogo walipe umeme kwa gharama za shilingi 77 kwa *domestic*, lakini pia kwa *business* wanalipa shilingi 108.99 wakati hapa Tanzania *domestic* tu ni shilingi 100 na tena ni shilingi 350 yani kwa wale ambao wanatumia *above 75 kilowatts*. Kwa hiyo, niombe Serikali iangalie na itathmini vizuri kwenye suala la nishati ili viwanda vyetu viweze kukua, lakini pia iweze kufanya tathmini vizuri kwa kutafuta mazao ambayo yataweza kupunguza adha kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nirudi kwenye suala la *TRA* ambalo pia yamekuwa ni malalamiko...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba niishie hapo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, tunakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Florent Kyombo nilishakutaja, utafuatiwa na Mheshimiwa Atupele Mwakibete, kama hayupo basi Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. FLORENT G. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee nishukuru kwa nafasi ya kuchangia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa nguvu na sisi wote kuwa hapa kwa ajili ya kujadili Mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu ambao umeletwa kwetu ni mpango mzuri na faraja kubwa ni kwamba, katika Mpango huo takribani asilimia 65 unatekelezwa kwa mapato ya ndani ya nchi yetu. Kuna maeneo machache ambayo mimi nataka nijielekeze kwa sababu ya huo muda wa dakika tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, tunaona *key players* ambao watahusika katika kutekeleza Mpango huu ni Halmashauri zetu za Wilaya kupitia Wakurugenzi wetu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Majiji na Miji, lakini pia na Wakuu wao wa Idara pamoja na watumishi wote ndani ya halmashauri hizo. Ni jambo jema kwa kiongozi yeyote kuhakikisha kwamba, mazingira ya wale wote ambao watahusika katika kutekeleza Mpango huu kwa kiasi kikubwa yameboreshwa na changamoto zile ambazo wanakabili ana nazo zimetatuliwa ili waweze kutekeleza Mpango wetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme katika eneo hili la Wakurugenzi wa Wilaya pamoja na Wakuu wa Idara limekuwa ni eneo ambalo lina changamoto nyingi sana na hasa kutopewa mazingira mazuri kwa ajili ya kutekeleza mipango mingi ya Serikali. Badala yake unakuta katika eneo kubwa Wakurugenzi wamekuwa wakishughulishwa na shughuli nyingine ambazo hazina tija kubwa kwa Serikali na *value for money* haipo. Unakuta kuna tume nyingi ndogondogo zimeletwa kutoka ofisi zetu za Wakuu wa Wilaya, kutoka kwenye ofisi zetu za Makatibu Tawala wa Mikoa na kutoka kwa Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyingine ukiziangalia natija yake kwa kweli unaona zinamfanya Mkurugenzi badala ya ku-*focus* kwenye suala la msingi na akajikita kwenye kutekeleza Mpango anashughulika kujibu hoja ambazo kimsingi nyingine unaona tija yake kwa Taifa letu haipo. Kwa hiyo, niombe sana mazingira wezeshi ya Wakurugenzi wetu wa Halmashauri za Wilaya pamoja na wasaidizi wao ambao ni Wakuu wa Idara ziweze kutolewa na waweze kutekeleza Mpango huu, ili tuweze kufikia malengo mahususi ya ndani ya miaka mitano tuwe tumefikia malengo yote ambayo yameainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili katika eneo hili, ni kwenye sekta ya ardhi. Mwaka 2000 Serikali ilikuja na mpango mzuri wa *retention scheme* ya fedha ya kodi yote ilikuwa inatolewa katika viwanja na mashamba, ikawa inakusanywa inapelekwa serikalini, lakini asilimia 20 inarudi.



Hiyo fedha ilisaidia sana katika kupanga na kupima maeneo yote kupitia Serikali zetu za Halmashauri za Wilaya, lakini mwaka 2011 Serikali kwa kuona ubora wa kazi ile iliongeza ile *percentage* ya *retention scheme* ikawa asilimia 30 na kazi zilizendelea kufanyika kwa ubora zaidi, zikapangwa na maeneo yakaainishwa, fursa za uwekezaji zikija zinakuta eneo tayari limeshapangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mwaka 2015/2016 *retention scheme* hiyo ilitolewa na Wakurugenzi wa Wilaya waliendelea kuhangaika kudai zile fedha zitoke Wizara ya Fedha, hakukuwa na majibu. Mwaka 2017 yakatolewa maelekezo kwamba, *retention scheme* ilifutwa katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2015/2016 kupitia Wizara ya Fedha na Mipango. Zile fedha kazi ilikuwa inafanyika kipindi hicho haikutolewa maelekezo, sasa hizo kazi zinafanyika kupitia bajeti ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo Halmashauri za Wilaya kupitia Idara ya Ardhi, zimebaki zimekatwa miguu, kazi hizo hazifanyiki kwa ufanisi. Tunatambua kazi nzuri ambayo Wizara ya ardhi imefanya kwa kutatua migogoro, lakini kwenye suala la kupima na kupanga na kudai fedha ambazo zinatakiwa ni masuuli ya Serikali yake, imebaki ni giza. Tuwaombe kwa muktadha huo hiyo *retention scheme* irudi na irudi katika asilimia 40 ili hizo kazi zifanyike kwa kuzingatia dira ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru. Naunga mkono Mpango ni mzuri kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Atupele Mwakibete.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii nami niweze kuchangia rasimu ya Mpango iliyowasilishwa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Ni dhahiri kwamba, Waheshimiwa Wabunge wamechangia hapa, lakini nataka tu niweke kumbukumbu sawa hasa katika masuala haya ya mipango kwa maana ya

tunapopanga, maana tunasema kupanga ni kuchagua, lakini mipango yote hii ni mizuri na Serikali yetu imeendelea kuitekeleza; mingine imetekelezeka, mingine bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nishauri katika eneo hili la Tume ya Mipango. Tunapopanga lazima tuwe na Tume ya Mipango iliyo imara sana. miaka ya nyuma kulikuwa kuna Wizara kabisa inayoshughulikia masuala haya ya mipango, sasa hivi Tume ya Mipango ni Idara ndani ya Wizara ya Fedha. Tafsihi yake ni kwamba, kama hakutakuwa kuna *coordination, monitory and evaluation*, tathmini na ufuatiliaji wa mipango yote tunayotaka kuipanga katika kipindi cha mwaka mmoja ama miaka mitano, itakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai kwa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ya Mipango ndio mpango mzima wa kutekeleza mipango hii ambayo tunategemea kuifanya. Kwa mfano mwaka 2010, mfano tu rahisi, Wizara ya Kilimo kipindi hicho pamoja na Wizara ya Maji walijenga vituo katika maeneo mengi nchini, zaidi ya vituo 200 na zaidi, hata kule jimboni kwangu kipo kimetumia zaidi ya milioni 900, hivi ninavyosema ni gofu, hakiendelezwi kiko vilevile tu. Maana yake thamani ya fedha iliyowekezwa pale haina tija kwa wananchi wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo lilikuwa zuri tu kwamba, wananchi itakuwa ni kituo cha kwenda kumwagilia pamoja na kujifunza mambo ya kilimo, lakini kimetelekezwa. Kimetelekezwa kwa sababu gani, hakuna muunganiko kati ya sekta moja na sekta nyingine ili kuishirikisha hiyo mipango na hatimaye iwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka nichangie ni suala la elimu yetu ya Tanzania. Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa elimu yetu ya Tanzania asilimia kubwa ni *theory* zaidi na sio *practical* kuanzia chekechea mpaka chuo kikuu. Naweza nikatoa mfano rahisi tu, kuna mwenzangu mmoja ambaye nilisoma naye zamani, tulikuwa tunasoma *computer science*, lakini *computer science* hiyo *computer* yenyewe tumekuja kuiona mwaka

wa tatu, ndio *computer* hata kuifungua, hebu *imagine*. Tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake tulikuwa tunafanya ma-*integrations* mengi, ma-*theory*, lakini *practical* ile yenyewe ile hatukuwa tunafanya. Kwa hiyo, niombe Wizara ya Elimu kwamba, sasa ni wakati wa kubadilisha mitaala yetu ya elimu. Ndio maana nchi zilizoendelea kama China wamewekeza sana katika ufundi na huku na sisi tumeanza kujenga vyyo vya ufundi ni jambo jema, lakini huko *technicians* wale ndio wataalam hasa. Hata akiwepo *engineer* mmoja, lakini *technicians* kwa wingi zaidi ndio mpango mzima kwa maana ya kutekeleza yale ambayo tunategemea yawe. Kwa hiyo, mfumo wetu wa elimu kuna haja kubwa sana ya kufanya *transformation*, tusipofanya hivi hawatakuwepo watu wa kusimamia na ambaye atajituma. Maana kila mmoja ukiwa na *degree* unategemea atakuwa boshi wa nani juu ya nani? Sio rahisi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la mfumo wa elimu ndio linasababisha pia changamoto katika ajira kwa vijana. Kwa mfano *South Africa* wana mfumo mmoja unaitwa *YES*. *YES* tafsiri yake ni *Youth Employment Service*, una *accommodate* wanafunzi wote wanaomaliza vyyo vikuu na vyyo vya kati kwenda kwenye taasisi binafsi. Namna gani inafanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko namna hii; Rais wa nchi ile Cecil Ramaphosa alipokuwa ameuzindua lengo lake kubwa ni kwamba, badala ya vijana katika matangazo mengi ya kazi ambayo yanahitaji pengine uzoefu wa miaka mitano, uzoefu wa miaka kumi na hawa ndio wametoka ku-*graduate* wametoa wapi huo uzoefu; kwa hiyo, ikabidi waanzishe mfumo ambao utakuwa rahisi kuwachomeka kama vile *field* wanapokwenda. Wanakwenda katika kampuni, wanakwenda katika taasisi, wanakwenda katika mashirika, lakini unaratibiwa na Serikali na Serikali kazi yake ni kuwezesha hizo kampuni ama hizo taasisi ama sekta binafsi, ili sasa wale vijana ambao wanakwenda kusoma kule au wanakwenda kujifunza kazi kule baada ya muda fulani

watakuwa tayari wamepata *experience* na kazi inapotokea Serikalini ama binafsi wao wenyewe ndio watakaokuwa wa kwanza kuajiriwa badala ya hivi tulivyo kwa sasa kwa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda sio rafiki sana, lakini nitaandika kwa maandiko suala la uchumi wa kidigitali. Namna gani Tanzania tunaweza tukaneemeka na uchumi wa kidigitali. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kupewa nafasi ili niweze kuwasilisha mambo machache ya kuishauri Serikali. Vilevile niishukuru Serikali kwa Mpango huu wa Miaka Mitano na hata huu wa Mwaka Mmoja ambao umeletwa mbele yetu kwa ajili ya kuujadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie mambo matatu. Jambo la kwanza ambalo nataka kulizungumzia ni kwenye sekta ya elimu. Kwenye sekta ya elimu nataka kuzungumzia jambo moja. Rais wetu tuliye naye kwa sasa alikuja na mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba, kila shule inakuwa na madawati. Mpango huu ambao Rais alituletea hatujauona nini ambacho Serikali inapanga kwenda kukifanya kuhakikisha kwamba, kila mwaka shule zinakuwa na uhakika wa madawati kuliko kuwa na huu mtindo wa zimamoto. Sijaona mpango wa kuona Serikali na sekta ya viwanda wakijadiliana kwamba, wana uwezo wa kujenga angalau kiwanda kimoja cha kimkakati Mkoa wa Njombe au mkoa wowote ambao unatoa malighafi kama mbao, ili Serikali iweze kupata madawati kwa uhakika kwa ajili ya shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukulia mfano mwaka 1985, Mwalimu Nyerere aliamua kujenga kiwanda cha Mgololo kwa ajili ya karatasi, ili shule zetu ziwe na uhakika wa kupata madaftari. Kiwanda hiki kilifanikiwa, lakini kwa sasa

kwenye hili suala la madawati hatuoni jitihada zozote ambazo zinafanyika za makusudi za Serikali kuona inajenga kiwanda ambacho kinaweza kikasaidia kupata *furniture* mbalimbali kwa ajili ya Serikali yetu na kwa ajili ya shule zetu. Sisi watu wa Mkoa wa Njombe tuko tayari ku-*offer* maeneo kama haya ya viwanda kusaidia Serikali yetu iweze kupata haya mambo ya madawati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka nichangie; wewe ni Mbunge wa Kongwa, *NARCO* ilianzishwa kwa ajili ya kuendesha hifadhi za Taifa, lakini tumeona *NARCO* ikijikita kwenye kutatua tu migogoro. Miaka inaenda, miaka inarudi hifadhi ya Kongwa pale toka Nyerere alivyoiacha ng'ombe ni walewale inawezekana na idadi imepungua, hakuna ng'ombe wanaoongezeka. *NARCO* inafanya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, wewe kwako Kongwa pale, kuna eneo kubwa ambalo hata Watanzania wangetengewa tu sehemu kidogo tu wapewe vile vitalu wafuge, angalau tungeona kwamba, kuna jitihada zinafanyika. Leo ukienda pale Ruvu mradi wa zaidi ya bilioni 5.7 wa machinjio ya kisasa umekufa. *NARCO* wapo na mambo yanaendelea, wamejikita Misenyi, wamejikita Kagera kwenye kutatua migogoro ya wafugaji tu, lakini *NARCO* haina mkakati wowote ambao tunauona kwenye Mpango hapa ukurasa wa 89, Kuendeleza *Ranch* za Taifa. Maeneo yamebaki ni makubwa, hayana msaada wowote kwa Watanzania, ni vema wananchi wangepawia, waweze kufuga ili Serikali iweze kukusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kwenye sekta ya wafanyabiashara. Hivi ninavyozungumza wafanyabiashara Makete, akina mama mafundi cherehani wanaambiwa wawe na mashine ya *EFD*. Ni masikitiko makubwa kwamba huyu mtu ana kitenge anashona anaambiwa awe na mashine ya *EFD*. Kodi *now is not to collect they are just trying to grab it* kitu ambacho siyo kizuri kwa sababu wananchi wetu wana uchumi mdogo, wana tozo nyingi lakini pili ukamuaji wake umekuwa ni wa tofauti.

Hata ng'ombe unayemkamua unatafuta jinsi ya kumkamua, unamlisha, unazungumza naye lakini sisi *TRA* yetu hawafanyi jambo hilo, wanakusanya kodi kwa nguvu. Pia naendelea kusisitiza tozo ni nyingi na zimegeuka kero kwa wafanyabiashara wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasihi na naomba *TRA* watafute mazingira bora na salama. Mbona Rais ametusaidia vitambulisho vya wajasiriamali vimeondoa kero za wafanyabiashara wetu kukamatwa mitaani na mgambo, watafute njia sahihi ya kukusanya kodi. Nashauri wakusanye kodi kwa utaratibu siyo kutuma *tax force* kama Mheshimiwa Nape alivyosema, wanaenda wanakamata maofisi ya watu na kompyuta za watu, huyo mtu utegemee kesho akusaidie tena kulipa kodi? Ni jambo ambalo linasikitisha, tunaomba *TRA* wasaidie wafanyabiashara wetu wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama ambavyo leo tuna vitabu vinavyoonyesha kwamba Wizara ya Kilimo kuna tozo ambazo imeziondoa kwa maana kwamba ni tozo kero, ndivyo tunavyotamani kwamba keshokutwa kwenye Bunge linalofuata au Bunge la mwakani tuje na kitabu kutoka *TRA* kinachosema hizi tozo ambazo ni za hovyoy kwa wafanyabiashara zimepungua kwa sababu wafanyabiashara wetu wanaumizwa. Vijana wadogo ajira mtaani hamna wakitaka kufungua biashara *TRA* wameingia, watu wa *OSHA* wameingia, watu wa Bima wameingia, watu wa *lift* wameingia yaani hadi kukagua *lift* kukagua ni Sh.400,000 kwa mwaka, *lift*? Sasa huyu mtu ata-*survive* vipi na tunatamani tuendelee kukusanya kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali hii nchi itajengwa na wenye moyo ambao ni sisi lakini kama mkiendelea kubomoa wafanyabiashara wadogo hatuwezi kukusanya kodi. Mwisho wa siku tunachoomba Wizara husika watuletee takwimu kama idadi ya wafanyabiashara inaongezeka au inapungua kwenye taifa hili. Kwa sababu kila siku wafanyabiashara wanalia kutokana na changamoto za tozo, wapunguze tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mchango mwingine nitaleta kwa maandishi lakini kwa kweli Watanzania wana matumaini makubwa na Mpango huu, naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Pius Chaya

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii lakini nimshukuru sana Waziri kwa kuleta Mpango huu. Nimeupitia Mpango huu ni mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nishukuru kwa miradi mikubwa ambayo tumeiwekeza kwa miaka mitano. Huo ndiyo mwelekeo sahihi wa nchi, lazima tuwe na *capital investment*. Kama tunataka hili Taifa baadaye liwe lenye heshima lazima tuanze kuwekeza sasa hivi kwenye miradi ya muda mrefu; miradi ya umeme, barabara, reli na ununuzi wa ndege. Bila kufanya hivyo litakuwa taifa lenye aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye tatizo la ajira kwa vijana wetu wanaomaliza vyuo vikuu. Watu wengi wameongelea kero mbalimbali upande wa elimu kwamba elimu yetu ni mbovu na kadhalika. Mimi naomba niwatoe mashaka kwamba ingekuwa mbovu mimi leo nisingekuwa Daktari hapa wa *Policy*, ingekuwa mbovu Mwigulu leo asingekuwa Daktari pale wa Uchumi. Nadhani kuna maeneo ambayo sisi kama wataalam tunahitaji kuishauri Serikali, ni *case by case* na tusi-*generalize*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia Mpango huu kwa kweli naomba niseme tunahitaji kuja na *chapter* ya pekee ni jinsi gani tunakwenda kutatua tatizo la ajira kwa vijana wetu waliomaliza vyuo vikuu. Mimi naomba nijikite kwa vijana waliomaliza vyuo vikuu tu kwa ngazi ya cheti, diploma na digrii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Mwalimu wa Chuo Kikuu cha Dodoma na nimefundisha Chuo cha Mipango, nina vijana wangu ninaowafahamu wamemaliza wana miaka 8 bado wapo mtaani. Wanaoathirika zaidi ni

watoto wa maskini ambao hawapo *aggressive*, hawajui wapi pa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashauri nini Serikali? Kwanza, natambua kuna program ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inaendeshwa na ndugu zetu wa *TAESA*, wengi tumepiga kelele hapa kwamba vijana wanamaliza vyuo hawana uwezo, huwezi kupata uwezo chuoni, uwezo tunaupata kwa kupitia *on job training*. Kule tunafundisha *theory* lakini lazima tuje na programu ambayo itawahamisha wale vijana kutoka kwenye *theory* kwenda kwenye *practice* na ndiyo kitu ambacho Ofisi ya Waziri Mkuu wamefanya kupitia program hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamefanya nini? Wamechukua vijana kama *internship program* wamewaweka pale kwa mwaka mmoja wakawapa *token* ya 150,000 *then* wakawasaidia kuwa-*groom*, wanawapitisha kwenye zile *life skills, interpersonal skills, communication skills, computer skills* na kadhalika, aki-*graduate* pale wanam-*link* na *job seekers* au wale *supplier* wanaotaka watu kwa ajili ya kuwaajiri. Hiki ndiyo kitu ambacho mimi nashauri huu Mpango ujikite kwamba tuendeleze ile program ambayo imeshaanza, *financing* yake ambayo bado ipo *weak* vijana wanapomaliza vyuo wajiunge pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka tuje na Sera ya *Internship*. Tuna vijana wengi wapo mtaani tunalalamika kwenye vituo vya afya hakuna watoa huduma wa afya, tunalalamika kwenye sekondari hakuna walimu lakini tuna vijana wengi mtaani. Ile program ambayo Waziri alikuja nayo wanawapa shilingi 150,000 kwa mwezi kwa nini tusiifanye hiyo *program* tuajiri vijana wale tuwaweke kwenye *health facilities*, tuwalipe shilingi 150,000. Kwanza itakuwa tumewapunguzia *stress* ya maisha, tumepunguza *stress* ya wazazi kuwatunza na tumepunguza *stress* ya watoto wa kike kuolewa tukawaweka pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuja na hiyo program kwenye huu Mpango kwamba sasa *internship*



*program iwe compulsory*, tutengeneze sera na sheria kijana yeyote akishamaliza ile miaka mitatu anakuwa *mainstreamed* kwenye *internship program*. Akishamaliza pale, hapa sasa uhusiano kati ya TAESA na Sekretarieti ya Ajira, nitashangaa kuona Sekretarieti ya Ajira unamuacha kijana ambaye Mheshimiwa Waziri amem-*groom* mwaka mzima kupitia *internship program* unaenda kumchukua mtu hajapita kwenye program hiyo. Tunapiga kelele vijana hawana *skills*, hizo *skills* tutazijenga kwa kupitia *internship program* na Sekretarieti ya Ajira sasa fanyeni kazi na TAESA ili kuhakikisha kwamba vijana wanaokuja kule hatutakuwa na malalamiko hawawezi kujieleza, tayari tumeshawa-*groom* kwa mwaka mmoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine hili ni la Wizara tofauti. Tunapoenda kutumia hii program ya *internship*, nataka tuje na kitu kinaitwa *policy maximum*, hebu sisi kama nchi tujiwekee ukomo wa kisera, kijana asikae zaidi ya miaka miwili tangu amemaliza chuo. Tunajisikia aibu vijana wanakaa miaka mitano mtaani wanatembea na vyeti, sisi wenyewe tumewafundisha, tumewekeza na tunataka warudishe zile kodi. Hebu tuje na sera ambayo nime-*propose* tuweke kiwango cha ukomo kwamba sasa Viwanda, Uwekezaji na watu wengine ambao sisi ndiyo *creators* wa kazi tukae pamoja tutengeneze *modeling* ya vitu gani ambavyo tunahitaji kuvifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kitu kimoja, kwa mfano, kwenye huu Mpango sijaona zile ajira milioni 8 ambazo tumeahidi tunaendaje kuzifikia? Tunahitaji kufanya *modeling* mwaka wa kwanza tutahitaji kufikia labda watu milioni mbili, mwaka wa pili milioni 3. Halafu pia tunawapataje hawa, ni kutoka *private sector* au *public sector*? Hicho kitu natamani kifanywe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni Mfuko wa Kuchochea Ajira kwa Vijana. Nashukuru Mheshimiwa Waziri ameliweka vizuri kwenye Mpango wake na namuunga mkono lakini naomba niboresha kwenye ....

## T A A R I F A

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, nimekuona Mheshimiwa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba vijana wanaomaliza vyuo vikuu akiona zizi la ng'ombe, akiona kinyesi anakimbia, akiona banda la kuku anakimbia. Vijana hawa wanaomaliza chuo kikuu hawajapata mahali popote pale pakwenda ku-*practice* hata kama ni kilimo kidogo. Shule zetu kuanzia sekondari tumeondoa mashamba darasa, hakuna mahala ambapo mwanafunzi anaenda ku-*practice*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *graduate* anawazungumzia mchangiaji hawajawahi ku-*practice* hivyo vitu kuanzia wanaanza darasa la kwanza mpaka wanamaliza hiyo *degree*. Mimi napigiwa simu kama Mbunge, Mheshimiwa Mbunge tunaomba utusaidie kazi, nawauliza kazi gani? Wanasema kazi yoyote hata kufagiafagia. Hii inaonesha kwamba mpaka anamaliza chuo kikuu haja-*define exactly* na kile kinachofanyika nyumbani kwake ufugaji na kilimo haoni kama ni kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimpatie taarifa mwalimu ambaye amefundisha chuo kikuu muda mrefu kwamba watoto kwa upande wa ku-*practice* vitu ambavyo tunataka viendeleze taifa kwenye kilimo hawa *graduates* hawajapata fursa hiyo na ni weupe kabisa. Ukimwambia *chips* kuku anakimbilia kuila ila mchakato wa kupatikana kwa mayai na viazi hataki kusikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Chaya muda wako ulishapita, nilikuvumilia tu.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nilikuvumilia kwa sababu mjadala huu ulikuwa unachokoza mjadala ule mpana ambao mtaona unarudi mara kwa mara na kwenye orodha yangu hapa Profesa Kishimba ataongea jioni sijui kama hatakuja kwenye *line* hiihii lakini *it's a very serious problem*. (*Makofi*)

Kuna binti ambaye alinitafuta kwa muda mrefu sana lakini jana nikawa na nafasi kidogo nikamwambia basi hebu tuonane. Nimekaa na yule binti saa mbili anamwaga machozi tu. Amemaliza Mzumbe miaka sita iliyopita na ni kutoka familia maskini, hana pa kwenda, anaona mbele giza. Alikuwa na mkopo ananiambia kuna malimbikizo ya miaka sita na zile *percent* na sijui na madudu gani. Kwanza hilo lenyewe ni pasua kichwa yaani hata cha kumu-*advice* unakosa. Hili ni tatizo kubwa jamani, kubwa sana lakini ndiyo mfumo wa elimu yetu. Sasa huyu aende wapi, kozi za Mzumbe zile na vyo vingine vinafanana tu, kwa sababu hawana *element* yoyote ya ujasiriamali, hamna! (*Makofi*)

Katika Taifa jirani kila mfanyakazi au mwananchi anayemaliza pale, nchi jirani ile, ana *element* yaku-*hassle*. Ndiyo maana kama mnafuatilia vyombo mnaona ma-*hassle* wanataka kuchukua nchi pale, kabisa, *what is hassling?* Yaani kila mtu hata mwenye ajira, Kenya kila mwenye ajira ana ka-*side hassle* yaani uhangaikaji ni sehemu ya maisha yao. Sisi Mtanzania kama mtu ameajiriwa anachoweza kufanya ni kununua kiwanja basi, viwili, vitatu. Ukimuuliza wewe maendeleo yako nini atakuambia aah nina viwanja. Hajajenga kwenye hicho kiwanja, ndiyo Mheshimiwa Mabula anatumkumbusha tulipe viwanja hapa kichwa kinauma hata hivyo vyenyewe kulipia kodi ya ardhi ni pasua kichwa. Sijui nani alituambia kwamba viwanja ndiyo *investment* lakini kila mtu hapa ana kiwanja kama huna kanunue leo. (*Kicheko*)

Ni eneo linahitaji Bunge hili tujadiliane na Serikali tusaidiane. Si tatizo la kumlaumu mtu, kumlaumu Serikali au kumlaumu nani, ni jambo ambalo lazima tulitazame wote

maana tuna-*frustrate* vijana wanamaliza kwa maelfu, tumewajaza fikra za kwamba kuna ajira mahali yaani anawaza kuajiriwa tu hawazi kwamba anaweza akajihangaisha akaishi, hawazi kwamba na yeye ni *employer* anaweza akafika mahali akaajiri wengine.

Ndiyo maana mnaona mjadala wetu kila wakati unaonesha mtoto wa darasa la saba anakuwa na nafuu zaidi kama alivyosema Mheshimiwa pale, yule darasa la saba haoni kama kinyesi cha ng'ombe ni tatizo, haoni kama kwenda shambani ni jambo geni, haoni kama kusukuma mkokoteni ni tatizo, yeye ni bodaboda, yeye ni kila kitu, yeye kibarua wa fundi baadaye anakuwa fundi yeye mwenyewe. Ni mjadala fulani wa wasomi wetu wa kuangalia tunakokwenda. Ni changamoto nzuri Mheshimiwa Dkt. Chanya ametupatia mnavyoona wasomi na hali halisi ya mtaa inavyodai.

Kitu kingine kila chuo kinaongeza kozi, hivi Chuo cha Kilimo SUA, Naibu Waziri wa Kilimo yuko hapa, eti nacho kinafundisha walimu wa sekondari, *what is this?* Nye si fundisheni watu wa kilimo? Mnaitwa kabisa Chuo cha Kilimo sasa walimu wa historia na geografia wa nini SUA? Unajua kwa nini wanachukua kozi hizo? Ni ili wapate hela kwa sababu idadi ya wanafunzi inakuwa kubwa ili chuo kiwe na *source of income*, tunapoteza hata *direction* ndiyo tunakotaka kwenda. Kwa hiyo, mjadala huu ni mpana, tuendeleo kujadili lakini ni jambo la afya kwa Watanzania. Naamini *out of* kujadili hivi na hasa hapa Bungeni tutafika mahali pamoja na Serikali yetu tutaona nini chakufanya.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu mtaona umekwisha lakini niwahakikishie wale wote ambao mmejiandikisha kwamba mtapenda kuongea leo mtapata nafasi ya kuongea. Kwa hiyo, endeleeni kujiandaa. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango imemaliza kazi yake kwa muda huu.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimwia Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokwishasema kwamba tutakaporudi jioni tutaendelea na uchangiaji na ataanza Mheshimiwa Hamad Hassan Chande ataendelea na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata na wengine wote tutapata nafasi jioni ya leo.

Basi kwa jinsi hiyo, naomba nitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 kamili jioni ya leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH ISSA – KATIBU MEZANI:**

### **KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji kwa jioni ya leo na ni dakika tano tano. Nilishaahidi kwamba tutaanza na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande na atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi.

**MHE. HAMAD HASSAN CHANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mtu wa awali katika wachangiaji kwa jioni hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah-wataala* ambaye ametuwezesha sisi kufika katika jengo hili na ametujalia kuwa na rasilimali ya uhai

ambayo ndiyo inatoa thamani ya ubinadamu. Maana yake bila rasilimali ya uhai, basi binadamu anakosa thamani ya ubinadamu. Ushahidi wa hilo, moja kati ya sisi akipoteza uhai tu, basi wapenzi wake wa karibu ikiwemo familia yake, wanakaa kwa pamoja vikao tofauti kujadili wapi wanaenda kumweka na kumtoa kwenye nyumba hata kama ni nzuri aliyojenga kwa gharama kubwa. Kwa hiyo, tumshukuru Mungu kutujalia rasilimali hii ya uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nakishukuru sana Chama changu Cha Mapinduzi kwa kunipa nafasi hii, kuiteua tangu awali mpaka kufika hapa leo, kwa sababu ni chama makini chenye viongozi imara sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo, naomba kwa ruhusa yako nianze na neno la Mungu kutoka katika Kitabu cha Qurani aya ya nane, Sura ya 102 inayosema:

*Kisha kwa hakika mtaulizwa siku hiyo juu ya neema mlizopewa, mmezitumiaje? Kwa hakika tumepewa neema nyingi sana. Mungu ametujalia neema nyingi sana katika nchi yetu ya Tanzania pande zote, sisi ni wa kujivunia kwa neema hizo. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mimi ni Mbunge kutoka Jimbo la Kojani na Wakojani tunajulikana sana kwa shughuli za uvuvi, naomba tu nijielekeze huko kwenye masuala ya uvuvi. Neema hizi ambazo ametupa Mungu hasa katika suala la uvuvi baharini na hata kwenye maziwa, zipo kanuni ambazo zimewekwa na baadhi ya watendaji wetu wa Wizara ama Idara ambazo zimekuwa vikwazo vya kutumia vizuri neema hizo.

Kwa mfano, Kanuni ya 58A(1) na (2) inayomtaka mvuvi lazima atumie mtego wenye urefu wa mita 144. Hiki ni kikwazo kikubwa sana kwa wavuvi wetu, inayotaka uvue samaki wa sentimeta 26. Kwa kweli baadhi ya samaki ambao wala hatuharibu mazingira, tunawahitaji kuwapata, lakini inakuwa ni ngumu sana kwa wavuvi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya pili ambayo ni kikwazo kidogo ni 58A ya uvuvi wa dagaa. Inataka dagaa wanaovuliwa wawe ni wa sentimeta tano. Kwa kweli dagaa wa sentimeta tano hadi saba, unaweza ukamwita sio dagaa tena huyo, anaweza kuwa ni samaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kanuni ya 66(1)(hh), taa za utumiaji katika uvuvi wakati wa usiku. Kanuni inataka taa ziwe ni za *watts* 50. Ni mwanga mdogo sana unaopatikana hasa kwa jiografia kwa baadhi ya maziwa kama vile Tanganyika au Bahari Kuu. Kuvua kwa *watts* 50 ni ndogo sana, samaki au dagaa hawezi kushawishika kuja katika mwanga na kuweza kumvua kwa urahisi. Kwa hiyo, ni vyema angalau iwe inafikia *watts* 200 au 300 kama kawaida ambavyo tunavua sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni nyingine ambayo ni kikwazo ni ile inayomtaka mvuvi asivue wakati wa mbalamwezi, lazima avue mwezi unapokuwa giza. Sasa hizi sisi wavuvi kwa mfano wa *ring net* ambao tunavua usiku wote ikiwa ni wa mbalamwezi au wa giza, ukisema tuvue msimu huo, ukifika wakati wa mbalamwezi tukale wapi jamani? Au tsubiri mpaka uingie usiku mwingine wa giza, siku 15 zile, au siku 10; nadhani hiki ni kikwazo kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubaya wa kanuni hizi, zinawafanya wavuvi wetu kutoroka katika nchi yetu na kwenda nchi za jirani. Baya zaidi, sisi tunafuga samaki, tunawalea, wanakua, wenzetu wa jirani ndio wanavua na kutumia samaki hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa hili ni kwamba, hizi kanuni zitakapowekwa au zitakapotungwa ni vyema kuwashirikisha na wavuvi, sio wataalam wa uvuvi peke yao ambao wanajisomea tu kwenye meza na viti. Walengwe kabisa wavuvi wenyewe kusudi washiriki kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nashauri kwa kuwa ni wa mwanzo nilinde kidogo; kanuni hizi zisiwe uzi wa buibui. Nadhani unaujua; *spider* yule. Kanuni

hizi zilikuwa zinamnasa yule mdogo tu, kama vile uzi wa buibui, akipita kurumbiza, inzi, kipepeo, wanakamatwa na ule uzi; lakini akipita njiwa tu, anaondoka nao uzi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kusema kwamba kanuni hizi zinapowekwa na idara zetu ni vyema ziwe zinakamata wale wakubwa na wadogo. Siyo wadogo tu ambao wanakamatwa hatimaye nyavu zao kuchomwa moto, tukasababisha watu kukataliwa majumbani kwao, tukaongeza idadi ya wajane na vijana wanaotelekezwa.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hamad.

**MHE. HAMAD HASSAN CHANDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Huyu ni Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge wa Kojani. Naweza nikasema Wakojani ndio wavuvi nambari *one* Tanzania. Kwa hiyo, sishangai kwamba hoja yake kwa kweli dakika zake amezitumia katika uvuvi. Tunakushukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mbunge wa Musoma Mjini, nilishakutaja kama ndio unayefuata, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua nafasi hii kukushukuru kwanza kwa kunipa nafasi. Vile vile nimepitia hotuba ya Mpango, umekaa vizuri pamoja na kwamba yapo marekebisho na ndiyo maana tuko hapa kwa ajili ya kuweka sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa tunapanga mipango hii, lazima ianzie kule kwetu kwa maana ya Halmashauri zetu. Wakati mwingine yako mambo ambayo



yako kwenye uwezo wa Serikali, lakini kunakuwa na ukiritimba ambao unakwamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nikianza na Jimbo langu la Musoma Mjini, huwezi kuamini lile jimbo ambalo lina wakazi wasiopungua laki mbili lakini lina ukubwa wa *square kilometer* zisizopungua 63. Kwa maana kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine haizidi kilometa kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya shida kubwa ambayo tumeendelea kuipata toka miaka na miaka, maana pale mimi nimekuwa Mstahiki Meya toka 2000 mpaka 2005, lakini vile vile nikawa Mbunge toka wakati huo 2005. Tumekuwa tukipambana au tukijitahidi sana kuongeza maeneo, kwa sababu kusema kweli *square kilometer* 63 kwenye wakazi 200,000, maana yake ni kwamba leo ukija pale Musoma unataka tu uwanja; kuna mwekezaji amekuja anataka uwanja ajenge tu hata shule. Hiyo nafasi haipo. Hakuna chochote utakachotaka kufanya kwa sababu ya eneo kuwa dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utaratibu unasema tuzungumze na halmashauri husika. Tumezungumza lakini mwisho wa yote hawako tayari kutoa yale maeneo. Sasa athari kubwa tunazozipata ndizo hizo kwamba leo hii hatuwezi kujipanua, hatuwezi kufanya uwekezaji, kwa hiyo, hata namna ya kuongeza mapato katika Mji wetu wa Musoma imekuwa ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inalifahamu hili. Tumejaribu kupitia katika vikao vyote mpaka *RCC* lakini suala hili hadi leo tunazungumza limeshindikana. Ukiangalia, hata wale wenyewe wanaokatalia hayo maeneo, unamkuta mtu, pale tulipo kwa sababu ni kata za jirani, kuja mjini kwa maana ya Makao Makuu, anatembea, ni kama kilometa tano. Kwenda kwenye Makao Makuu ya Jimbo lake, anaenda kilometa 80. Kwa hiyo, ukiangalia kwa namna moja au nyingine, yule mwenyewe kwa maana ya mwananchi, anapata adha kubwa kwa kwenda kuhudumiwa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokuja kwenye hizi huduma za jamii, mfano leo ukizungumza hospitali, hawa wote wanakuja wanakuja pale mjini. Anapotaka kwenda shule, anaacha shule mita 200, lakini anaenda shuleni kilometa tano mpaka saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hizo juhudi ambazo tumezifanya, tunajikuta kwamba wale wananchi hata tulipowazungukia katika kuzungumza nao, wote wanataka kuja mjini. Pamoja na kwamba wanataka kuja mjini, ukifika tu kwenye Baraza la Halmashauri, basi mnakaa vikao lakini wanasema watawajibu, wakijibu wanasema hatukukubaliana na hilo ombi lenu. Ndiyo maana wakati mwingine tunasema, Serikali kwa sababu inayo nafasi ya ku-*intervene* katika kuhakikisha kwamba vile vile inatusaidia ili tupate maeneo makubwa, wawekezaji wakija wapate. Watu wakitaka viwanja wapewe. Basi hiyo itatusaidia sana katika kukuza Mji wetu wa Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia Musoma, naamini umefika pale umeona, Musoma lazima ufunge safari kwamba unaenda Musoma. Yaani huwezi tu kupitia kwamba unaenda Mwanza, unaenda Sirari, lazima ufunge safari kwamba unaenda Musoma. Pale uchumi pekee tulionao, kidogo ni ziwa ambapo lile ziwa nalo liko vijijini. Kwa hiyo, hakuna uchumi ambao tunaupata kutokana na lile ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunahitaji tufanye biashara, yaani watu wetu wawe na zile biashara ndogo ndogo zinazowapa uchumi. Sasa unapotaja biashara, watu 200,000 halafu wameji-*confine* katika *square kilometer* 63, kwa hiyo, unakuta tatizo la ajira Mjini Musoma ni kubwa sana. Ndiyo maana tunasema kwamba Serikali inahitajika ku-*intervene* ili tuweze kupata maeneo na kwa kufanya hivyo basi tutakuwa tumewasaidia watu wetu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedasto Manyinyi. *Actually issue* yako inagusa Manispaa na baadhi

ya majiji kama Arusha na mengine yaliyobanwabanwa hivi ambayo yanahitaji yapumue kwenye vijiji. Ni hoja ya msingi sana, nafikiri Serikali wanaweza wakaiangalia.

Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Katani.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Mpango uliopo mbele yetu. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima. Pia nawashukuru wanawake wa Mkoa wa Rukwa kwa kunichagua tena kwa kura nyingi sana za kishindo, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe na ofisi yako na Wabunge wenzangu wote kwa ujumla wao kwa kunisaidia nilipopata matatizo ya kufiwa na kaka yangu hapa Dodoma, lakini Wabunge hawakuniacha, waliweza kunisaidia mpaka kwenda kuhifadhi mwili huko kwenye nyumba yake ya milele. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie sasa kwenye mchango wangu. Nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanya. Imeweza kufanya miradi mingi mikubwa ndani ya kipindi cha miaka mitano. Kwa kweli kazi inaonekana, kwanza kabisa imeweza kumtua mama ndoo kichwani kwa asilimia 90, pia imeweza kutengeneza barabara, umeme, mambo ya afya, sisi wanawake mpaka sasa hivi tumepata heshima kubwa sana, tunajifungulia sehemu nzuri. Kwa hiyo, Serikali imefanya mambo mengi mazuri na makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, palipo na mambo mazuri na makubwa hazikosekani changamoto. Mkoa wangu wa Rukwa unakabiliwa na changamoto kubwa sana kwenye Sekta ya Kilimo. Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa mikoa minne ambayo inazalisha kwa wingi sana chakula cha aina nyingi, lakini wakulima wamesahaulika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Mkoa wa Rukwa wanalima, lakini changamoto kubwa ni masoko. Naomba Serikali yangu Tukufu ya Chama Cha Mapinduzi, iwakumbuke sana wakulima hawa hasa wa mikoa minne ile ambayo inazalisha sana chakula kwa wingi. Kwanza kabisa, kuwatambua wakulima wadogo, wa kati na wakubwa, Serikali iweze kuwatambua na mahali wanapolima. Ikiwatambua, uwezekano wa kuwasaidia kuwapa mikopo itakuwa ni rahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia iwalettee wakulima Maafisa Ugani, kwani Maafisa hawa ni changamoto kwenye maeneo yetu. Mimi mwenyewe ni mkulima, lakini sijawahi kumwona Afisa Ugani akinitembelea hata siku moja kwenye shamba langu. Kwa hiyo, wakulima wanajilimia wanavyojua wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali kama Rais wetu alivyosema kwamba tunakwenda kwenye Tanzania ya Viwanda; tukianzisha viwanda vingi vya pembejeo, nadhani pembejeo pia zitashuka bei na wakulima watapata pembejeo kwa bei nafuu. Naiomba Serikali ijikite sana katika kuanzisha viwanda vya pembejeo ili wakulima nao wapate nafuu ya kupata pembejeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba kwenye mikoa ambayo inalima sana kwa mfano Rukwa, zingeanzishwa Benki za Kilimo ili wakulima waweze kujikopea wenyewe kwenye hizo benki, walime kilimo chenye tija. Hivi sasa wanahangaika sana, kwa sababu pembejeo zenyewe ni bei kubwa, kwa hiyo, utakuta wanapata shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni masoko. Naomba ile taasisiya *NFRA* ingeweza kuongezwa fedha. Ile inasaidia sana kwa sababu wakulima wakiuza mazao *NFRA at least* wanapata soko kidogo. Hata hivyo kwa mwaka 2020 kwa mfano kwa Mkoa wa Rukwa tuliambiwa *NFRA* watanunua milioni 50, matokeo yake walinunua tani 5,000 tu, kwa hiyo ikawa ni changamoto kubwa sana. Mpaka sasa hivi wananchi wale wanapata tabu sana, mahindiyako ndani,

hawajauza hata kidogo. Kwa hiyo, naomba Serikali kupitia Wizara ijikite kuongeza fedha kwenye taasisi ile ya *NFRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata. Mheshimiwa Katani Ahmed Katani, atafuatiwa na Mheshimiwa Suma Ikenda.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipewa fursa jana, kama naweza kupewa tena niendeleo.

**MWENYEKITI:** Hapana, hapana, uko kwenye daftari langu sijui imekuwaje. Mheshimiwa Suma Ikenda.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikupongeze wewe kwa kazi nzuri na namna ambavyo unaliongoza Bunge hili Tukufu. Pia nimpongeze Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa vile ambavyo anasimamia Kanuni hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa wetu, Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna ambavyo ameweza kufanikiwa kuingia katika uchumi wa kati kabla ya kipindi kilichokuwa kimetazamiwa. Kwa namna ambavyo tumeweza kuingia kwenye uchumi wa kati Benki ya Dunia wameshangazwa na kasi ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba kuishauri Serikali iendeleo kuweka mkazo kwenye Halmashauri zetu ili ziweze kuwekewa fedha za kutolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili wawe kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufanikiwa zaidi kwa namna ya kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwenye uchumi wetu wa kati, ili kasi iendeleo kuhusiana na

namna ya kutoza kodi kwa wafanyabiashara, naomba elimu kwa upande wa wafanyabiashara imekuwa ni ndogo. Kipindi cha nyuma mfanyabiashara anapokuwa anafanya biashara mfanyakazi wa *TRA* alikuwa ni rafiki wa mfanyabiashara lakini sasa hivi hali imekuwa siyo, wafanyabiashara wamekuwa wakilalamika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo napenda kuishauri Serikali kuanzia elimu ya msingi, sekondari na vyuo ikiwezekana kuwe na elimu kuhusu kodi kwa maana Mtanzania yeyote pindi anamaliza chuo asijute kwamba anaonewa namna ya kutoa kodi aone ni uzalendo kutoa kodi kwa maana ya kuendesha nchi yetu. Maana nchi inaendeshwa kwa kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Watanzania wanaelewa vizuri sana kazi ambayo ameifanya Mheshimiwa Rais wetu ya kuijenga nchi yetu ya Tanzania. Mheshimiwa Rais wetu baada ya kuchaguliwa 2015 ndani ya siku mia moja alipongezwa kwelikweli hata wananchi mbalimbali wengine walisema Mheshimiwa Rais akae miaka 100, wengine walisema miaka 40, kila mtu aliongea la kwake kwa namna ambavyo amekuwa akiendesha nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba Mheshimiwa Rais ameweka nidhamu Serikali lakini ameweka nidhamu mpaka kwenye ndoa za Watanzania. Naongea hivyo kipindi cha nyuma watu walikuwa wakilalamika sana baba anarudi nyumbani usiku wa manane, mama anarudi nyumbani muda atakao akilalamika kwamba kuna foleni kubwa. Baada ya kuingia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kama Rais, baba na mama wanawahi nyumbani kupanga mipango ya maendeleo ya familia zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo miaka ya nyuma mara nyingi sana tulikuwa tukiwashuhudia hawa watu wa Kilimanjaro ikifika Disemba wanarudi nyumbani kwao, kwetu haikuwa hivyo. Hata hivyo, baada ya kuingia Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph

Magufuli sasa hivi wazazi wanafurahia watoto wao, watoto wao walikuwa hawaonekani mikoani mwingine anakuwa hajaenda hata miaka mitano, mitatu mpaka kumi lakini sasa hivi ikifika Disemba magari yanapishana huko mikoani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana sana Watanzania tumuelewe Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Watu wanasema pesa haziko mifukoni lakini maendeleo yamekuwa ni makubwa, ukipita mitaani huko barabarani unaona jinsi wananchi wanavyojenga nyumba tena wanaezeka mabati ya m-South au tunapenda kuita mabati ya rangi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuendeleo kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri anazoifanya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Suma Ikenda, tunakushukuru sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Aida Khenani dakika tano.

**MHE. AIDA J. KIHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyenijalia afya niweze kusimama tena ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya dakika tano, nitazungumza kwa uchache. Tunapozungumzia Mpango wa Miaka Mitano tunazungumzia Dira ya Taifa. Napozungumzia Dira ya Taifa lazima nitazame wimbi kubwa la vijana ambao wamekosa ajira. Tunapozungumzia wimbi kubwa la vijana lazima tutafute suluhisho kupitia Dira ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ajira ambazo zinatolewa Serikalini lakini bado tunarudi kwenye kilimo kwamba inawezakana ikawa mwarobaini au ikasaidia angalau kwa hili tatizo la ajira. Ukizungumzia kilimo cha Tanzania, nitatoa takwimu ya 2019 – 2020, wakulima ambao walilima 2019/2020 waliotumia mbegu bora ni asilimia 20 tu;

waliotumia mbolea za viwandani asilimia 20, hapo ndiyo tunarudi kwenye lengo kweli kilimo ni uti wa mgongo, kitakwenda kutatua tatizo hili la ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunazungumza hivyo siyo kwamba tuna shida ya ardhi kwenye nchi yetu, ardhi ipo na wataalam wapo wanalipwa fedha, shida nini kwenye Serikali yetu ya Tanzania kwenye suala la kilimo? Kama bajeti tunapitisha na mipango inaletwa hapa na inapoletwa naamini kabisa wanakuwa wamewashirikisha wataalam wetu huko chini, shida inakuwa ni nini Zaidi? Kupanga mpango ni jambo moja na kupeleka fedha ni jambo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia 2015-2020, hekta zilizoongezeka kwenye umwanguiliaji ni 233,339. Leo kwenye Mpango huu tunazungumzia kwenda kufikia hekta milioni moja na laki mbili. Nilitamani kujua tu kuna miujiza gani utakaotumika hapo wa kufikia hekta milioni moja na laki mbili wakati kwa miaka mitano tunazungumzia laki mbili na thelathini na tatu mia tatu thelathini na tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache tu ya kushauri, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais nilijikita hapo na leo narudia. Kama tunataka kuboresha kilimo chetu ni lazima kwenye Mpango fedha zitengwe kwa ajili ya kupelekwa kwenye vyo vya utafiti. Kama kweli tuna nia njema ya kuokoa Taifa letu lazima tutenge fedha za kutosha tupeleke kwenye vyo vya utafiti. Tukipata fedha za kutosha mbegu zenyewe zitakuwa bora, tukipata mbegu bora lazima tutatenga fedha kwa ajili ya kupima udongo kujua udongo huu unafaa kwa zao lipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia ngano, ukitazama Mkoa wa Rukwa tunalima ngano sana lakini kama tunasema hitaji la Taifa letu ni ngano Serikali imejipangaje kwenye Mpango huu kwenda kupima maeneo ambayo yanaweza kufaa kwa kilimo cha ngano ili iendelee kuzalishwa kwa wingi Tanzania? Utakuta ni wimbo ambao tunauimba tu. *(Makofi)*



Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, kuna mikoa ambayo inazalisha sana mpunga, Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwao lakini ukiangalia kwenye Mpango hapa hakuna kitu ambacho kimetengwa kwa ajili ya kwenda kuongeza uzalishaji wa mpunga na ili twende kwenye viwanda ni lazima tuboresha *raw material*. Kwenye *raw material* mbolea leo Mkoa wa Rukwa mfuko mmoja Sh.65,000 wakati gunia la mahindi Sh.30,000, unaweza ukafikiri hapo huyu mkulima auze gunia ngapi ndiyo anunue mfuko mmoja wa mbolea? Je, kilimo kitakua au kitarudi nyuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunazungumzia viwanda nashauri tujue Tanzania tunahitaji viwanda vya aina gani. Viwanda vya kwanza vinavyohitajika ili tupunguze gharama za mbolea lazima tuwe na kiwanda kinachozalisha mbolea Tanzania ili wakulima wapate mbolea kwa bei rahisi. Tukiwa tumepeleka na mbegu bora tunazungumzia sasa kilimo cha uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili lazima tupeleke Maafisa Ugani wa kutosha kwenye kata ambazo zinazoongoza kwa kilimo. Leo kuna Maafisa Kilimo wapo mjini, hatukatai haa na mjini wanalima lakini kwa sababu ni wachache basi hao wachache wapelekeni maeneo ambayo wanazalisha, maeneo ambayo wanaendesha kilimo tujue kwamba tuko *serious* na kilimo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miradi ya umwagiliaji tunatambua kwamba Serikali imepeleka fedha nyingi ikiwemo Mkoa wa Rukwa lakini miradi hiyo haifanyi kazi. Lengo la Serikali ni nini? Kabla leo hatujabuni miradi mipya tupeleke fedha tukamalizie miradi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aida. Mheshimiwa Assa Mekanika, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Mariki. Mheshimiwa wa Mekanika, Mbunge wa Kigoma Kaskazini.

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**MWENYEKITI:** Kama hayupo basi Mheshimiwa Martha Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia jioni hii ya leo. Awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na afya njema. Kipekee naishukuru na kuipongeza sana Wizara ya TAMISEMI kwa jinsi ambavyo inasaidia kina mama kupata mikopo ya asilimia 10 ambapo ni asilimia 4 kwa vijana; asilimia 4 kwa kina mama; na asilimia 2 kwa walemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimesoma na kuuelewa sana Mpango huu wa Maendeleo wa miaka mitano. Naomba sana nijikite kuishauri Serikali kuangalia namna ambavyo inaweza kuwasaidia akina mama na vijana hawa kwa kuwaboresha kutoka kwenye asilimia zile 4:4:2 na kuwapa asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyoelewa, kina mama ndiyo wanaoweza kuibeba jamii na ndiyo wanaobeba familia katika kuzihudumia. Hivyo naiomba sana Serikali sasa ione kuna umuhimu wa kina mama hawa ambao pia ndiyo waaminifu wakubwa katika upigaji wa kura, kina mama hawa ambao wamekibeba Chama cha Mapinduzi kwa kuwa waaminifu kwa kupiga kura nyingi sana za ndiyo kwa rahisi wetu Dkt. John Pombe Magufuli, sasa ni wakati wa Serikali yetu sikivu ione umuhimu wa kuiboreshea kina mama hawa kutoka kwenye mkopo wa asilimia 4 na kuwapa asilimia 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Serikali yetu sikivu iweze kutoa elimu ya kutosha, elimu wezeshi kwa kina mama hawa ili waweze kunufaika na mikopo hii. Kuna baadhi ya maeneo kina mama kweli wamekuwa wakiomba mikopo na kupewa mikopo hii lakini mikopo imekuwa haiwanufaishi kutokana na kwamba elimu wanayopewa ni ndogo. Mfano, kina mama wanaojitolea katika kazi za za kufuga nyuki,

napenda sana Serikali yetu sikivu iweze kutoa elimu wezeshi kwa kina mama hawa ni namna gani wataweza kufuga nyuki ili waweze kunufaika wao lakini waweze kutoa wigo wa ajira katika jamii zinazowazunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana napenda nijikite katika kuzungumzia Wizara ya Maliasili. Niiombe sana Serikali yetu sikivu, sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi tunayo *Katavi National Park*, naiomba sana Serikali yetu sikivu ili kuendana na Mpango huu wa Maendeleo ituboreshee barabara katika maeneo yale ya hifadhi ili kuwawezesha watalii wanaokuja Katavi kuweza kupita kwa urahisi zaidi. Tumeona kipindi cha masika ambacho ndicho kipindi wanyama wanapatikana kwa wingi, kipindi ambacho utalii ungefanyika kwa wingi kule Katavi, barabara hazipitiki na hivyo kuwazuia watalii wengi kuvutiwa kuja *Katavi National Park*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba sana Serikali yetu sikivu kuiboresha hifadhi hii kwa ku—*promote* kwa kutoa matangazo mbalimbali ili watu wote duniani waweze kuifahamu *Katavi National Park*. *Katavi National Park* ni hifadhi pekee yenye Twiga mweupe. Natamani sana Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wenzangu muifahamu *Katavi National Park*, ni hifadhi ambayo ina vivutio vingi sana. Hivyo, Serikali ikiboresha miundombinu katika hifadhi hii itaweza kupata mapato makubwa lakini tutaweza kwenda kutoa fursa za ajira kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi wakiwepo vijana wanaozunguka mkoa ule. Pia itawasaidia kina mama kwa kuwawezesha kutengeneza *curio shop* ambapo wataweza kuuza vinyago mbalimbali kwa watalii lakini kutoa fursa mbalimbali za kibiashara ikiwepo mama ntilie kupika na kuwahudumia watalii wanaokuja katika hifadhi hii ya Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kutoa shukrani zangu za dhati kwa jinsi Serikali inavyoendelea kutuhudumia wananchi wa Katavi kwa kutupa miundombinu katika maeneo mbalimbali lakini kutupa ulinzi na kuhakikisha

hali ya amani ipo katika Mkoa wetu wa Katavi. Hivyo naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee naendelea sana kuwashukuru akina mama wa Mkoa wa Katavi kwa jinsi ambavyo wameniamini mimi kama mwakilishi wao kuja kuwawakilisha. Nawaahidi sitawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Martha Mariki kwa hotuba yako fupi lakini iliyosimama. *(Makofi)*

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Ramadhani Ighondo atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili iweze kuchangia jioni ya leo. Awali ya yote, nianze kwa kutoa pole kwa wananchi wenzangu wa Jimbo la Singida Kaskazini kwa msiba uliowapata kwa kuondokewa na mwananchi mmoja, Mzee Salimu Isango baada ya gari waliyokuwa wanasafiria kutoka Ng'amu kundumbukia kwenye Mto katika Daraja la Mwakiti. Nawapa pole na niwaambie kwamba Mpango huu wa Taifa wa Miaka Mitano umesema kwamba utajikita katika uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Kwa hivyo, daraja hilo naamini litatengenezwa na litaepusha vifo vinavyoendelea kutokea hasa kipindi hiki cha mvua maji yanapokuwa yamejaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuzungumzia eneo la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Msiba mkubwa uliopo kwa vijana wa Kitanzania hivi sasa pamoja na wasomi wote wanaopita vyuoni kwa kupata mkopo huu ama mikopo hii ya elimu ya vyuo vikuu ni tofauti na matarajio ambayo yaliwekwa kwenye mfuko huu. Serikali ilikuwa inalenga kuwakomboa wananchi wake maskini lakini kinachotokea hivi sasa watoto wa kimaskini wanaonufaika na mkopo wa elimu ya juu pindi wanapomaliza masomo

palepale wanakabwa wanaambiwa waanze kulipa mkopo bila kujali amepata ajira pale pale anageuka kuwa mdaiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli kama sisi tumelenga kuwakomboa Watanzania, jana umemkopesha kwa sababu ni mtoto maskini aliyeshindwa kujisomesha. Kesho baada tu ya kumaliza masomo hajapata kazi umeshambana. Kwa maana hiyo hapa Serikali badala ya kuwasaidia watu wake imegeuka sasa inafanya nao biashara. Kitu ambacho ni hatari sana kwa maisha ya Watanzania na kwa elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu changamoto ya ajira ilivyo kubwa hivi sasa. Tunasahau hapohapo, badala ya sisi kujikita kuwasaidia hawa vijana ili watoke waende wakafanye kazi hata kwa kushirikisha Sekta Binafsi, sisi tunawakaba hapohapo bila kujali changamoto wanazokutana nazo na mazingira magumu ya elimu tunayoona sisi wenyewe hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba hii bodi badala ya kujikita kwenye kuwabana watoto hawa kwa kuwadai mikopo hii warudishe pindi wanapomaliza masomo, iwape muda wa kulipa madeni yao. Pia riba zipungue, riba zimekuwa kubwa sana kwenye eneo hili.

**MWENYEKITI:** Jitambulisha wa taarifa. Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

## T A A R I F A

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba Ibara ya 178 ya Sheria ya Bodi ya Mikopo inawapa nafasi wahitimu kurejesha mikopo baada ya miaka miwili. Marekebisho hayo yalifanyika mwaka 2016 ikaondoa kipindi cha mwaka mmoja na hivi sasa marejesho yanafanyika baada ya miaka miwili na ilipitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ighondo, pokea taarifa hiyo.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, lakini tatizo ni riba kubwa zilizopo kwenye hii mikopo, tupunguze riba hii. Mwanafunzi anapoanza kulipa ule mkopo alipe lile deni alilokopa na huu mkopo usiwe na riba, ndiyo hoja kubwa ninayotaka kuisimamia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinaitwa *retention*, ule mkopo unaongezeka kadri muda unavyokwenda, ndiyo kitu ambacho mimi nataka nikiombe hapa; badala ya huyu mtu kuja kulipishwa riba alipe ule mkopo, *principle* aliochukua, ndiyo hoja kubwa ambayo naiomba Serikali ichukue hili na iliangalie kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo watoto hawa wanaomaliza vyuo wapate kazi, tushirikishe sekta binafsi. Tushirikishe sekta binafsi hawa watoto waende wafanye *practical*, wafanye mazoezi, hata Serikali inavyotangaza ajira kile kipengele cha uzoefu wa miaka 15 mtoto huyu atafaulu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka tu kumpa taarifa mzungumzaji kwamba licha ya riba bado muda wa miaka miwili ambao umetengwa ni wa karibu sana. Hapa asubuhi umetupa *testimony* ya mtoto aliyemaliza Mzumbe, ana takribani miaka sita hajapata ajira, sasa baada ya miaka miwili unanza kumwambia atoe laki moja, anazipata wapi wakati hana ajira. Kwa hiyo hilo nalo Serikali iweze kuli-*consider*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nampa hiyo taarifa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Malizia kwa sentensi moja Mheshimiwa Ramadhani kwa sababu muda umekwisha.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda pia angalau kwa uchache nizungumzie kidogo kwenye eneo la viwanda...

**MWENYEKITI:** Bahati mbaya umechelewa. (*Kicheko*)

Ahsante sana Mheshimiwa Ighondo.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Hili eneo la mikopo ya wanafunzi kwa kweli ni eneo tata. Serikali wakaliangalie tu kwenye mipango yetu hii tunakoenda. Sisi tulisoma hiyo inayoitwa bure enzi zetu, tulikuwa tunapata *boom* la bure. Sasa hawa watoto wa maskini ni jambo jema sana kwamba tunawasaidia kwa mkopo, lakini baadaye wanalipa kwa riba. Sasa ule msaada wako uko wapi? Si bora ungesema basi unamdai kama tunavyofanya mkopo wa gari, kwamba unamdai *50 percent* halafu 50 anarudisha. Sasa unasema ulimsaidia lakini bado unadai yote tena kwa riba na nini, inakuwa kama biashara vile. (*Makofi*)

Lazima tuliangalie hili suala *from a moral point of view*, inakuwa kama ina *immorality* fulani hivi. Ni kitu cha kutazama vizuri, hawa watoto wanapitia magumu kweli.

Nilikutaja Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, halafu Mheshimiwa Profesa Jumanne Kishimba ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, lakini niseme kidogo sisi Wabunge ambao tumeingia kwa mara ya kwanza tunatumia njia mbili hapa kujifunza namna shughuli

za Bunge zinavyoendesha. Ya kwanza ni hii ya kusoma kwenye Kanuni na nini na nyingine ni kuwaangalia wale wazoefu waliokuja hapa siku nyingi namna wanavyoendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima niseme kwamba ninayo masikitiko. Wapo baadhi ya wazoefu wanachangia Mpango hapa wanasimama tangu ameanza mpaka anamaliza anakosoa tu halafu hasemi tufanyeje. Nilitaka kusema hilo kwa kweli sioni kama ni jambo jema ambalo sisi tunajifunza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa maono yangu mimi Serikali ya CCM na inawezekana Serikali ya nchi nyingine yoyote duniani ingependa kuwafanyia wananchi wake kila jambo wanalotaka, kinachozuia kufanya hivyo ni uwezo. Ndiyo maana tuko hapa leo kupitia mipango kuona kupanga ni kuchagua, lipi litangulie lipi lisubiri kutokana na uwezo wetu. Kama tunataka tuongeze zaidi lazima tuseme tunapataje uwezo wa kufanya zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nishauri kidogo kwenye eneo la ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership – PPP*). Nimeangalia katika Mpango huu, ni miradi nane tu ambayo imewekwa katika Mpango wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa kwanza ni Kiwanda cha Dawa; mwingine ni Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi; Hoteli ya Nyota Nne; Uwanja wa Mwalimu Nyerere; usambazaji wa gesi asili; Reli ya *Standard Gauge* Tanga – Arusha – Musoma na Mtwara – Mbambabay; Mwingine ni hosteli ya Chuo cha Biashara Kampasi za Dar es Salaam na Dodoma; na Chuo cha Uhasibu Kampasi ya Dar es Salaam na Mbeya; na wa mwisho ni mradi wa Kiwanda cha Kutengeneza Simu. Hii ndiyo miradi katika mpango mzima wa mwaka ambayo imeingia kwenye *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na *PPP* ndilo eneo ambalo lingeweza kutusaidia kushirikisha sekta binafsi katika



kutekeleza mambo mengi ya Serikali. Kwa mfano leo hii usafiri wa Reli ya Kati kutoka Kigoma kuja Dar es Salaam, wasafiri wanaotakiwa kusafiri kila siku ya treni wanaoondoka ni asilimia 25 tu, asilimia 75 ya wasafiri wote wanabaki kwa ajili ya kukosa mabehewa. Kwa nini katika mpango huu tusingeingiza mabehewa kwenye PPP, wapo Watanzania wafanyabiashara ambao wangeweza kununua mabehewa ya treni yakafungwa. Sasa hivi injini hizi zinakokota mabehewa chini ya uwezo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwenda pale Stesheni ya Kigoma zaidi ya mara nne, mara tano. Injini inaondoka imefunga mabehewa nane yenye *capacity* ya kubeba mabehewa 30, mabehewa hakuna na mabehewa ya mizigo vilevile tatizo. Wakati mwingine yanakosekama mabehewa mpaka yanasababisha mfumuko wa bei ya saruji na bidhaa nyingine za viwandani zinazotoka Dar es Salaam kuja maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango atakapokuja hapa atueleze namna anavyoweza kuongeza wigo kwenye PPP. Naamini kabisa wapo Watanzania kama watu wanaweza wakanunua mabasi 115 wanashindwaje kununua behewa mbili, tatu au nne za treni akaingia katika utaratibu huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya afya vilevile bado tunaweza tukaingia kwenye utaratibu wa PPP. Nimeangalia sasa hivi kwenye hospitali zetu, tuna wodi za kawaida zile za msongamano na kuna wodi ambazo zimepewa *grades; grade one* na *grade two*. Wodi zile kukaa wodini siku moja acha huduma nyingine, unachajiwa kati ya shilingi 25,000 mpaka shilingi 40,000. Hiki ni kiwango cha *lodge* za kawaida za mjini ambazo mtu anaweza akakaa. Ukiwaambia wafanyabiashara wakujengee majengo hayo kwenye hospitali, watajenga tutaigia kwenye utaratibu wa PPP...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kilumbe, naona hii kengele bwana sijui ina matatizo gani. *(Kicheko)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Ina hiyana, lakini hakuna shida. Ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda. Basi unavyozungumza hapo kuna watu wa ACT huku wanakutazama kama nini, nawaambia ndio huyo Kilumbe Ng'enda. *(Makofi)*

Hili wazo la treni ni wazo zuri sana, TRC wangeweza kufanya utaratibu wakatengeneza kitu cha aina fulani hivi, wala siyo kwa mawazo ya mtu mmoja anunue behewa, tuna uwezo Watanzania wa kununua seti za treni hata kumi, kabisa kwa watu kuweka huyu 10,00, iwe 5,000, halafu ikawa ndiyo shares zao mle wakawa ndio uwekezaji wenyewe huo wa wazawa. Ni jambo la kulifikiria kabisa na inawezekana likawa zuri tu. Wizara ya Fedha liangalieni hili.

Mheshimiwa Jumanne Kishimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda. Mheshimiwa Profesa yeye huwa ni dakika kumi.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niungane na Wabunge wenzangu kwenye kuchangia Mpango huu wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili au matatu kama muda utaniruhusu. La kwanza; juzi Mheshimiwa Rais alipita kule Kahama akiwa anatokea Chato, alisimama Kahama. Haikuwa nia yangu mimi kueleza matatizo yale ya shule na afya lakini ilibidi kuyaongea ingawaje ni mambo ya Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa shule wajaribu kuja na mawazo mapya. Hivi ninavyoongea Gazeti la Nipashe

la leo wanafunzi waliochaguliwa kwenda kidato cha kwanza Mkoa wa Shinyanga ni 20,000 lakini wanafunzi 7,400 hawajulikani walipo na hawajahudhuria. Sijui sasa hata watakaokwenda *form one*, je watafika *form four*? Watakaofika labda robo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili wala siyo la Serikali kutoa pesa. Sheria ilizoweka na utapeli ulioingia shuleni, shule imehama kwenye elimu imekwenda kwenye biashara. Ukiiona orodha ya karatasi ya mwanafunzi kutoka darasa la saba kwenda *form one*, akikuletea mtoto utamwambia ngoja nile kwanza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vinavyosemwa mle ndani mwananchi wa kawaida wa kijijini hawezi. Mfanyakazi wa kawaida wa mshahara wa laki tatu, hawezi. Vitu vinavyotakiwa ni kweli vitawezekana au tutaongeza rushwa? Wanakijiji wao wamekataa lakini mfanyakazi itabidi aende kwenye rushwa au aibe ili ampeleke mtoto wake shule.

**MWENYEKITI:** Unazungumzia *joining instructions*? Ile karatasi ya...

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ya vifaa vinavyotakiwa.

**MWENYEKITI:** Orodha ya vifaa ili aweze kujiunga na *form one*.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Orodha ya vifaa hivyo haina uhusiano wowote na elimu; ni utapeli mtupu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi wa kijijini kweli anahitaji *tracksuit*; kweli? Mheshimiwa Waziri yuko hapa na bahati nzuri hizi ni ripoti za Shinyanga, tunaomba na Mheshimiwa Waziri, Uzuri Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango na Waziri wa Elimu wote ni wa Kigoma, watupe na wao ripoti zao kama kweli watu wa Kigoma wanaweza kununua viatu vyeusi. Kiatu cheusi *original* ni Sh.35,000 mpaka shilingi 40,000,

hivi vingine vyote vinapigwa *dye* na Machinga vinakuwa vyeusi, baada ya wiki tatu vinarudia kuwa vyeupe. Sasa kuna sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Waheshimiwa hawa, Mheshimiwa Waziri wa Elimu ni Profesa, Mheshimiwa Dkt. Mpango pale ni *doctor*. Kweli na kutembea kote, leo bado tunahusudu viatu kweli viwe ndiyo chanzo cha elimu cha kwenda kumkabili mtu. Wenzetu wangeliangalia sana. Nusu ya wanafunzi hawakwenda; haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la elimu naona Wabunge wanajaribu kulliongeaongea lakini linahitaji maongezi marefu sana. Ni kweli mwanakijiji unamchukua mtoto wake asubuhi saa 12 unakwenda kumkimbiza mchaka mchaka baadaye anaingia darasani, saa tatu, saa nne. Kwa nini asiende saa tano amemsaidia mzazi wake asubuhi, amefanya na kazi ili aende saa tano amekula. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama tutakataa, tutafanyaje. Huko mwisho hatuna ajira, tunakuja kuwaambia warudi nyumbani baada ya kuwa na *degree*. Wewe ulimchukua mtoto wangu anakula mihogo na viazi, unanirudishia anakula chipsi, soseji na mayai unakuja kukaa naye vipi nyumbani. Haiwezekani. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mnacheka lakini ni ukweli kabisa, *these are facts of life*. Endelea Mheshimiwa Kishimba.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unamrudisha mtu unamwambia akajitegemee, anajitegemea naye vipi? Sisi kule kijijini hata kuku akila mayai yake anachomwa mdomo na huyo ni yule anayetaga vizuri kama hatagi vizuri kesho yake anapelekwa kwenda kuuzwa. Sasa unanirudishia mtu anayekula mayai mimi nitakaa naye vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri wenzetu wa Wizara ya Elimu waje na mawazo mapya. *Academy* za

mpira ninyi mnakubali watu wafundishwe wakiwa wadogo, mnakatazaje watoto wetu kulima, kuchunga asubuhi, kufanya biashara za duka ili waende mchana; kwani watapata hasara gani? Hata kama ikitokea akawa mtoro ameshajua biashara kuna ubaya gani? Mtuambie ubaya wake nini. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ninyi wenyewe mna-*confirm*, Mheshimiwa wa Mipango kule amesema ana watu wana miaka nane hawana kazi, je, familia zao mnazihesabuje na ninyi Serikali mnataka hela yenu. Mimi nilikuja na hoja hapa kwamba na watoto wawe wanalipa. Lakini wewe unang'ang'ania mpaka riba kwa mtoto. Vipi mimi mzazi, umeniacha maskini, mtoto wangu umemharibu; hukumpa elimu, umemharibu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya Tanzania ukweli ni kwamba mimi natumia gharama kubwa kumwandaa mtumwa atakayeenda kuwa mtumwa wa mtu mwingine. Inawezekana kweli? Kwa nini unakataa mawazo yangu ya shughuli zangu tuka-*share* pamoja ili mtoto atakaposhindikana, akirudi kwangu mimi siyo mzigo, anajua hata vyakula vyangu na maisha yangu ya nyumbani; tungegombanaje na nani angekwambia kwamba kuna tatizo la ajira. Ilikuwa hakuna tatizo la ajira maana yake mtoto angeona kwamba kazi ya biashara, kazi ya kulima au kufuga inanilipa Zaidi, sitaki hata hiyo ajira, ata-*bargain* na mshahara. Sasa hivi hawana haja ya ku-*bargain* mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimnaulishe mwanangu, kila kitu, halafu mimi unipe karatasi nije kwako. Kwa kweli ni kitu ambacho kina matatizo makubwa sana. Uzuri kwa kuwa na Wabunge wengine, miaka mitano mimi nimepiga kelele lakini uzuri na Wabunge wameanza kuliona na najua mpaka mwakani wakati hela imepungua ndiyo tutalijua vizuri zaidi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili la uwekezaji. Mtazamo uliopo tunatazama tu upande mmoja. Juzi kwenye Kamati yangu ya Biashara na Viwanda nilijaribu kuwadokeza

kidogo wenzangu kwamba jamani hivi uwekezaji ninyi mnaoujua ni wa viwanda peke yake. Dunia imebadilika, leo ndege yetu inakwenda India asilimia 90 ya wasafiri ni wagonjwa, kuna ubaya gani wenzetu wa uwekezaji wakaongea na watu wa hospitali za India waone kitu gani kinachowakwaza kuja kuweka hospitali zao hapa. Tuwaruhusu, tuwape *EPZ* ileile ambayo tunaitoa kwenye viwanda, tusiwawekee tena yale masheria yetu ya hapa wenyewe wafanye bila kufuata sheria za kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itatusaidia na wagonjwa wa nchi zingine wanaokwenda India watakuja kwetu, lakini watumie sheria za kwao, tusiwawekee tena yale makorokoro yetu, mara *migration*, mara hukusoma, mara nini, hapana, itawezekana kabisa na biashara itawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengi sana, kuna maeneo ya vyo vya nje, tuwape maeneo au tuwajengee. Kama tunaweza kujenga vitu vyote vikubwa, tuwaulize wanataka nini, ili tuwajengee waweke *standards* zao, wanafunzi watoe wao nje, wa kwetu nao wakitaka *wa-apply* kama wanaenda nje, lakini wakiwa hapa hapa nyumbani. Nasi tukitaka kutibiwa kama ni hospitali, badala ya kwenda India, si tuta-*apply* tunaenda kutibiwa mle mle tu; na watu wa nje watakuja. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri wenzetu wa Uwekezaji mawazo yabadilike sana. Leo kuna biashara kubwa sana ya imani. Tuna viongozi wa dini ambao wana mvuto mkubwa sana. Kwa nini tusitenge maeneo tukawauliza, je, tukikujengea eneo la kuabudia, unaweza kuja hapa kwetu mara moja kwa mwezi? Ili kusudi wale watu wanaokufuata wewe kule wa nchi za jirani wanaweza kuja kukuona hapa mara moja kwa mwezi. Sisi tutapata biashara, hoteli zetu zitapata wateja na maeneo yote ya shughuli mbalimbali yatafaidika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilienda mbali sana mpaka nikasema, hata *group* lile la Babu wa Loliondo, kuna ubaya gani na wao wakawekewa eneo lao na yenyewe ikawa *EPZ*.

Mtu akitaka kwenda kutazamiwa hali yake, aende kihalali. Si tumeruhusu? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachohitaji sasa hivi ni kutembelewa. Hotuba ya Mheshimiwa Rais imesema inataka watu milioni tano, je, watu milioni tano tutawapata kutokea wapi ili waje watutembelee? Ni lazima wenzetu wa Uwekezaji wapanue wigo, waache kufikiria upande mmoja. Wakijitahidi hilo, litatusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kumalizia ni suala hili la *permit*. Kuna shughuli ambazo huwa hazisomewi, ni za ukoo au mtu anajua bila karatasi. Mheshimiwa Waziri wa Madini anafahamu, kulikuwa na suala la wakata *Tanzanite*. Wale watu wanaokata *Tanzanite* hawana elimu wala cheti, lakini wanafahamu kukata *Tanzanite*. Swali lililokuwa linatatiza, hawawezi kuja hapa kwa sababu *permit* yao haiwezi kupatikana maana hawana elimu. Sasa labda niulize wasomi kwa kuwa wamo humu; *definition* ya elimu ni nini, ni karatasi au ni kuelewa? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana kama mtu umemkuta anakata *Tanzanite* vizuri na anauza; na yako inakwenda kukatiwa hapo, unashindwa kumwambia aje huku kwa sababu ukimwuliza cheti, anasema sisi hii kazi haisomewi na vyo vyake havipo. Sasa kweli tukose biashara kwa ajili ya neno "cheti" au "*document*" na mtu anafahamu? Haiwezekani! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ni mzuri, naomba sana wenzetu wa Uwekezaji na Mheshimiwa Waziri wa Fedha wafikirie.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ndiyo maana Spika akambatiza jina la Profesa. Kwa sababu yeye mawazo yake huwa ni *original* na anakuja nayo vile yalivyo, sasa ukitaka yachukue, usipotaka yaache. (*Makofi*)

Ni kweli wanafunzi wanaofaulu darasa la saba (Waziri wa Elimu yupo), nichukue mfano alioutaja yeye kwamba Shinyanga 20,000, labda 7,000 hawataenda shule; moja ya sababu, nyingine sizijui, majina ya watoto wanaotangazwa wamefaulu siyo yote. Yanatajwa idadi ile ambayo vyumba vya *form one* vipo, halafu Halmashauri zinaambiwa zihangaike kujenga vyumba halafu ndiyo inatolewa orodha ya pili baada ya vyumba kuwa vimeshajengwa. Nafikiri mnanipata Waheshimiwa.

Sasa ile *gap*, kwa wananchi wa kawaida, orodha ya kwanza ikitoka, kama mtoto wake hayupo anajua aah, kafeli huyo, kwa hiyo, anatawanyika kushoto. Utakapokuja kutangaza matokeo yako ya awamu ya pili, watu hawapo; wa *u-house girl* ameshaenda, wa kufanya nini ameshaenda. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba majina ya waliofaulu yangukuwa yanatoka yote, *whether* una *capacity* ya kuwachukua au huna ili mzazi awe anajua kwamba mtoto wangu amefaulu. Vinginevyo hapa katikati ndiyo tunapowapoteza hawa, inaanza juhudi ya kuwasaka wako wapi, inakuwa taabu.

Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda nilishakutaja kama ndiye unayefuata, utafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia naishukuru Wizara ya Fedha kwa uwasilishaji mzuri wa Mpango wa Miaka Mitano inayokuja kwa Taifa letu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia Mpango huu, tuna maana kwamba ni mwelekezo wa Serikali kwa miaka mitano ijayo. Sasa ili kuutendea haki Mpango huu na yale matarajio tunayoyatarajia yaweze kupatikana vizuri, kuna mambo lazima yaboreshwe ikiwemo rasilimali watu, lazima iwepo, miundombinu iboreke na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza wenzetu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa sababu wametuwzesha na kutuelewa sisi Wannewala kwa kuwaendeleza na kuchukua majengo ambayo yalikuwa ya *NDF* ili kuwa *VETA*. Sisi Wannewala tuna kiu kubwa ya kupata ajira kwa vijana wetu, kwa hiyo, tukawakabidhi wenzetu wa Wizara ya Elimu majengo ili yatumike kama *VETA* na vijana wetu wakapate ujuzi, waweze kujijiriri wenyewe na kisha maendeleo ya watu yaweze kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo jema, lakini majengo yale yatatumia na Wilaya zaidi ya moja kwa maana ya Tandahimba, hakuna *VETA*, ni majirani zetu, watatumia pale; Masasi kwa maana ya Lulindi, hawana *VETA*, watatumia pale na Wannewala. Kwa hiyo, naiomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ituongeze au itujengee mabweni ili wanafunzi watakoenda kusoma pale wapate elimu na ujuzi unaotosheleza bila kuhangaika, mwisho wa siku wakapate wao wenyewe kujijiriri na maendeleo ya nchi yaweze kupatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili maendeleo yaweze kupatikana, lazima miundombinu iboreshwe hasa barabara. Wannewala Vijijini wana barabara yao ambayo inaunganisha Mkoa wa Lindi na Mtwara kwa maana ya Wilaya ya Lindi Vijijini na Newala; barabara ya kutoka Mkwiti – Kitangali hadi Amkeni. Barabara ile ni ya vumbi, lakini ikiboreshwa kwa kiwango cha lami, tuna uhakika kabisa kwamba mawasiliano yatakuwa rahisi, watu watafanya biashara, watakuwa wanasafiri kutoka eneo moja na kwenda eneo lingine na kujipatia fedha ambazo wataenda kuendeleza maisha yao na kuachana na hali ambayo wanayo kwa sasa.

Kwa hiyo, naiomba Wizara ambayo inasimamia ujenzi, kwa sababu tunataka kuboresha au kuleta maendeleo ya watu, basi itujengee barabara ile kwa kiwango cha lami ili nasi maendeleo yetu yaweze kupatikana kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mchangiaji ambaye amezungumzia suala la utafiti kwa vyuo vyetu vya kilimo, ni muhimu sana. Utafiti wa mazao ni muhimu sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali iongeze fedha kwenye vyuo vya utafiti ili waweze kufanya utafiti wa mara kwa mara ambapo watakuwa *up to date* na hali ya mabadiliko ya mazao yetu kwa kadri inavyojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wanamtware tunalima korosho ambazo zina magonjwa mbalimbali; ni kama binadamu, magonjwa yanabadilika kila leo. Kwa hiyo, tusipowekeza kwenye utafiti wakulima wetu wakapata kujua aina ya magonjwa ambayo yanajitokeza kwa wakati huo kupitia watafiti wale wa *TARI* Naliendele, nadhani tutakuwa hatufanyi chochote na uzalishaji wa zao la korosho utakuwa unapungua kadri ya siku zinavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niunganishe na Maafisa Ugani. Tunaomba Maafisa hawa wawepo kwenye vijiji vyetu, kwa sababu sasa hivi tunavuna lakini kiholela...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja, lakini tunaomba tupatiwe Maafisa Ugani ili wakawasimamie wakulima wetu ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwa mara nyingine naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda. Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Usonge Hamad.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa fursa ya kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano na ule wa Mwaka Mmoja wa 2021/2022. Kutokana na uhaba wa muda, nitachangia kwenye eneo la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni sekta muhimu sana. Karibu kila Mbunge aliyesimama hapa na hata Mabunge yaliyopita; nimekuwa nafuatilia kwenye runinga, hii ni mara yangu ya kwanza, Wabunge wengi walikuwa wanaonyesha hisia zao kwamba kilimo ni muhimu. Pamoja na huo umuhimu, bado kilimo kina changamoto kubwa kwamba hatujawekeza kikamilifu kwenye miradi ya kilimo. Bado hatujawa *serious* sana kwenye kilimo kama ambavyo Wabunge wengi wameonyesha hisia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wasilisho alilotoa Waziri wa Fedha na Mipango, miaka mitano iliyopita tuliwekeza vizuri sana kwenye miradi mikubwa ya maendeleo na nitaitaja hapa. Tuliwekeza vizuri sana *trillions of money* kwenye *SGR*, tulitoa *3.79 trillion*, tukawekeza kwenye barabara *8.6 trillion*, tukawekeza kwenye elimu *3.15 trillion*, tukawekeza kwenye ndege *1.24 trillion*, kwenye maji *2.03 trillion*, kwenye umeme na nishati *2.83 trillion*. Ni kitu kizuri na hii miradi imetupa heshima kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo sasa, miaka mitano iliyopita fedha iliyokwenda Wizara ya Kilimo ilikuwa ni shilingi bilioni 189.9 tu. Niseme tu, kwa mawazo yangu, nafikiria kiasi hiki kilikuwa ni kidogo sana kwa miaka mitano. Hebu tujulize, sote tunakiri kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili, ni nini kinatukwaza tusiwekeze fedha za kutosha kwenye sekta ya kilimo? Nina hakika tukijitoa kikamilifu tukawekeza kwenye kilimo, tutamkwamua mkulima, tutalikwamua Taifa hili na sote tutaingia kwenye uchumi wa kati tukiwa pamoja na wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba sasa ni wakati wa kufanya maamuzi magumu tuwekeze *trillions* kwenye kilimo na siyo *billions* kama ilivyokuwa kwenye miaka mitano iliyopita. Tuwekeze *trillions* kwenye kilimo ili tuweze kusaidia nchi yetu kwa Pamoja kwa sababu kilimo ndiyo kinachoajiri watu wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwekeza fedha za kutosha kwenye kilimo, zitatusaidia mambo mengi sana. Sitaki kuyarudia lakini machache ambayo wenzangu wameshayasema, tutasaidia vituo vya utafiti na huduma za ugani. Namshukuru sana Waziri wa Kilimo, amesimamisha Maonyesho ya Nane Nane, ameshaona kuna shida kwenye ugani, amesema fedha zielekezwe kwenye Ugani. Kwa hiyo, tutasaidia huduma za Ugani na uzalishaji mbegu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiachana na hilo, tukiwekeza fedha nyingi kwenye kilimo, hizo trilioni ambazo nashauri, zitasaidia sana kutekeleza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, tutachimba mabwawa ya kutosha, tutachimba visima mahali popote palipo na maji kwenye nchi hii, tutarekebisha ile miundombinu ya mifereji ya asili ambayo ipo nchi nzima na tumeiacha haijafanyiwa kazi sana. Tukisharekebisha hii mifereji tutakuwa na maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini kitatokea tukishakuwa na maji ya kutosha? Maji yatasambaa nchi nzima kwa ajili ya kilimo kama tulivyosambaza umeme na barabara. Tukishafikia hapo, maji yakishapatikana, tutalima kwa uhakika na kuvuna zaidi ya mara mbili kwa mwaka. Kile kitu ambacho Mheshimiwa Bashe na Wizara ya Kilimo walikuwa wanasema *block farming*, kitafanyika kwa uhakika, kwa sababu tutakuwa na maji ya kupeleka kwenye hizi *blocks* ili tuweze ku-*irrigate* na watu wazalishe mazao ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yakishapatikana, wakulima wetu hawatasita kwenda kuchukua mikopo benki. Watakuwa na uhakika wa kuzalisha na kupata kitu. Watakwenda kukopa *TIB* na Benki ya Kilimo na maisha yataanzia hapo, watu watafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda umeisha lakini niseme tu, ni vyema pia tuwezeshe hizi benki; *TIB* na Benki ya Kilimo, wapewe mitaji ya kutosha na waelekezwe kuwa na *window* maalum ya kuwasaidia wakulima wadogo wadogo, siyo wakulima wakubwa tu. Kwa hiyo, tukifanya hivyo, tutakuwa tumewasaidia wakulima na watazalisha vya kutosha. Wakishazalisha vya kutosha, tutaanzisha viwanda na tutafanya mambo mengi ambayo yataleta maendeleo kwa Taifa letu, tutamkwamua mkulima kutoka kwenye umasikini na tutakuwa tunakwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa. Nakushukuru sana.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Prof. Patrick Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini. *(Makofi)*

Nilishakutaja Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, utafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii kuhudhuria kwenye Bunge lako Tukufu salama usalimini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, sina budi pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri wa Fedha kwa uandaaji mzuri wa mapendekezo haya ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi pia kipekee kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa mno aliyofanya kwa ajili ya

kulisimamia Taifa hili la Tanzania kusonga mbele kimaendeleo. Ingawa wapo watu wachache ambao ndiyo wanaomrejsha nyuma Mheshimiwa Rais, lakini bado anaendelea kufanya kazi kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wasilisho la Waziri wa Fedha, uchambuzi na ushauri wangu utajikita katika maeneo makuu matatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza nitajikita zaidi kuhusiana na kupanda bei kwa vifaa vya ujenzi. Sasa hivi tumeshuhudia upandaji bei wa holela. Tokea kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu 2020, bei ya *cement* imepanda mno. Kwenye hili halijaathiri tu sekta binafsi, lakini hata sekta ya umma pia imeathiriwa mno. Sasa hivi tumeshuhudia *cement* inauzwa kwa shilingi 17,000/= mpaka shilingi 20,000/=. Kwa kweli Watanzania wanaumia sana. Haiumizi tu kwa huku *Mainland*, lakini hata kwa upande wa Zanzibar pia wanaumia. Wapo wafanyabiashara ambao wanachukua *cement* kutoka Bara kupeleka Zanzibar; kwa bei hii ya shilingi 17,000/= ikifika Zanzibar ni bei kubwa mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika kuja kufanya majumuisho atupe majibu, amechukua hatua gani, au atachukua hatua gani kwa ajili ya kudhibiti upandaji holela wa bei ya *cement*? Siyo *cement* tu, nondo nazo zimepanda sana; *gypsum powder* nayo pia imepanda sana; misumari na bati, halikadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana atakapokuja Mheshimiwa Waziri atupe majibu na mikakati ambayo ipo kwa ajili ya kudhibiti huu upandaji holela wa hii *cement* ambayo imemuathiri sana Mtanzania katika pato lake la kawaida. Siyo kuathiri tu katika sekta binafsi, hata sekta ya umma, kwa maana ya Serikali. Sasa hivi Serikali inapoendesha miradi yake ya kimaendeleo, hununua *cement* kwa bei ghali sana, inasababisha kukwamisha utendaji mzuri wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie eneo la pili ambalo ni muhimu sana kwa sasa hivi katika nchi yetu ambayo tayari tunaendelea kwenye uchumi wa kati. Bado hatujajipanga na hatuna mpango mkakati wa kuhakikisha kwamba Serikali inakusanya mapato kupitia *digital economy*. Kwa sasa hivi, nadhani sote ni mashuhuda, Waheshimiwa Wabunge tunatumia mitandao ya kijamii. Wapo wafanyabiashara wengi sasa hivi hawanunui bidhaa zao kuingiza madukani, wananunua bidhaa ile kuweka kwenye stoo na wakauza biashara yao kupitia mitandao ya kijamii. Wanatumia *WhatsApp, Instagram, Facebook* na mitandao tofauti tofauti. Hata hivyo, bado sijaona wazi kabisa Serikali kusimamia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wafanyabiashara wanawasiliana na mteja moja kwa moja kwa maana kwamba *seller* na *customer* wanashirikishwa kwa pamoja wanawasiliana wapi nikuletee mzigo, nikikutumia mzigo Dodoma utatoa pesa ya usafiri shilingi 1,000, lakini Serikali bado hajjatambua hizi *technic* ambazo sasa hivi zinatumiwa na wafanyabiashara. Hii inasababisha Serikali kupoteza gharama kubwa sana kwa ajili ya kuwachaji hawa wafanyabiashara. Hivyo, naiomba sana Wizara hii pamoja na wataalam wetu wa Serikali kuhakikisha sasa wanaweka mipango madhubuti na mikakati ili mradi fedha za Serikali zisipotee kupitia uchumi huu wa *digital economy*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sasa hivi tuna wasanii, tuna watu mashuhuri kwenye nchi hii ya Tanzania na wanatumia mitandao ya kijamii, kwa mfano, tunao wasanii wakubwa wanapata fedha kupitia *you tube*; msanii analipwa pale ambapo ana watazamaji wengi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Usonge.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Usonge Hamad tunakushukuru sana. Kwa vile umemaliza na suala la wasanii, kabla ya Sophia, nimuite Hamis Mwinjuma kwanza ili aunganishe. Mwana FA.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Umenipiga *ambush* kusema ukweli. Cha kwanza kuongea kwenye Bunge lako tukufu ni kumshukuru Mwenyezi Mungu, pili, kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi na kipekee kabisa Rais wangu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambaye aliongoza vikao vyote vya uteuzi vilivyohakikisha jina langu linarudi. Tatu, niwashukuru wananchi wenzangu wa Muheza kwa kunipa imani kubwa. Nne, niishukuru familia yangu na nichukue fursa hii sasa kuchangia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 mpaka 2025/2026. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la mchango ni kuisaidia Serikali kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato. Niseme kwamba nimeusoma Mpango na naona kwamba kuna maeneo mengi ambayo tunaweza kama Wabunge tukachangia na tukaisaidia Serikali kufanya hilo ili iweze kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ufanisi kadri inavyokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwa sababu ya muda sitaweza kuongea mambo mengi, lakini niseme kwamba eneo ambalo nataka kulichangia ni hasa la walionitumia, wananchi wa Muheza. Pamoja na kwamba nchi hii inaonekana kwamba asilimia 65 ya wananchi wa nchi hii wanapata riziki zao kwa kutumia kilimo, wananchi wa Muheza ni takriban asilimia 90 ama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Muheza kama ambavyo najua wananchi wengine wengi wa nchi hii wanataka kuchangia mapato ya Serikali zaidi ya wanavyofanya sasa hivi. Mazingira yanawapa wakati mgumu. Ningependa kuchukua nafasi hii kuiomba Serikali ijue kwamba haiwezi kukwepa moja kwa moja kwenye mazingira kuyafanya rafiki ili kuwezesha kuingiza fedha zaidi



baadaye. Ndivyo biashara zinavyofanywa, unawekeza ili upate zaidi huko mbeleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilihudhuria Mkutano wa wadau wa mkonge na Waziri Mkuu na moja ya vitu ambavyo vilinishangaza lakini kwa wema, ni suala kwamba wakulima wadogo wanazalisha zaidi ya wakulima wakubwa, kwamba katika *top four* ya wazalishaji wa zao la mkonge nchini wakulima wadogo ni namba moja, wakifuatiwa na Mboni wakifuatiwa na na *METL* na wengineo wanafuata. Hii inaonesha kwamba mahali ambapo tunafanya kosa labda ni kutotoa macho kwenye kuhakikisha wakulima wadogo wanawezeshwa na kupewa nafasi ya kuzalisha zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Rais Magufuli ya kufungua Bunge la 12 tarehe 13 Novemba, 2020, katika ukurasa wa 27 na 28 Rais anasema kwamba moja ya vitu ambavyo vinatu-*cost* ni kwamba, naomba ninukuu: "Takwimu zinaonesha kuwa kila mwaka nchi yetu inapoteza wastani wa kati ya asilimia 30 – 40 ya mavuno yake kwa sababu mbalimbali ikiwemo kukosekana kwa miundombinu ya kuhifadhi" mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais pia kwenye ukurasa wa 27 ameweka wazi kwamba lengo la Serikali ni kukifanya kilimo kuwa cha kibiashara, sasa kuna miradi mbalimbali ambayo ilisitishwa, mathalani Mpango wa *Marketing Infrastructure Value Addition and Rural Finance - MIVARF* kwamba baada ya awamu ya kwanza Serikali haikusaini kuendelea na awamu ya pili. Sijui sababu zake, lakini nafikiri moja ya vitu ambavyo Serikali ingeweza kufanya ni *ku- take over* kwenye mpango huu, badala ya kuwaacha wale wa-*Finland* watuendeshee, Serikali ingeendeleza kwa sababu ni Mpango ambao ulikuwa unaonekana una manufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *post-harvest centres* ambazo zilikuwa zinatumiwa kama masoko zilikuwa zinawekwa mahali kuhakikisha soko la wafanyabiashara wa

mbogamboga, kwa mfano maeneo kama Lushoto, linakuwa la uhakika. Miundombinu ya kufikisha kwenye soko lile wale watu wa Finland walikuwa wanahakikisha wanatengeneza. Kwa hivyo, tunaweza kuua ndege wawili kwa jiwe moja. Kwanza tukahakikisha miundombinu ya wafanyabiashara, wakulima kufikisha kwenye soko inapatikana na pia soko la wazi la wafanyabiashara wakulima hawa wa mboga mboga liko wazi. Kwa mfano kulikuwa na barabara ya kutoka Mktoni kwenda Kwai kule Lushoto au Chanjamjawiri mpaka Pujini kule Pemba hizi zote zilitengenezwa kwa ajili ya Mpango huu. Kwa hiyo tungeweza kuhakikisha kwamba wana soko na miundombinu inatengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vitu ambavyo vinaniumiza moyo ni kwamba hii asilimia 30 mpaka 40 ambayo Mheshimiwa Rais alisema inapotea ni ya wakulima wadogo. Wakulima wa ndizi kule kwetu Amani kwa mfano, ukienda wakati wamvua unaona jinsi ambavyo ndizi zimeoza barabarani kwa sababu zinashindwa kufikishwa sokoni. Kwa hiyo, naomba Serikali iwekeze kwenye kuhakikisha kwamba tunawafaidisha, tunawanufaisha wakulima wadogo na wanaweza kupata masoko...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. HAMIS M. MWINJUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, Mwana Fa. Ahsante sana.

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kupata nafasi ya kuchangia Mpango huu wa Tatu tunaouenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mpango unaandaliwa kulikuwa kuna malengo hasa waliyafikia. Kwanza kulikuwa na mambo kama manne kwa sababu ya muda nitayataja, viwango vya juu vya maendeleo ya viwanda lakini pia ushindani, maisha bora na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uweze kutimiza haya malengo kulikuwa kuna viashiria, kwa mfano, walisema kuwekeza kimkakati katika viwanda vya nguo za pamba pamoja na mazao ya mbogamboga. Leo hii katika nchi hii ya Tanzania na hasa nikizungumzia Nyanda za Juu Kusini, wanalima mazao ya mboga mboga, wanalima mazao ya biashara lakini hatuna soko la uhakika. Ndugu zangu hapa wamezungumzia Maafisa Ugani. Leo hii ukienda Mkoa wa Mbeya, utakuta wakulima wanalima kutokana na wanavyosikia kwenye mikeka au kwenye vikao vya chini wanavyokaa na wala sio kwa utaalum. Leo wanakwambia zao la chai ni zao ambalo linauzika duniani na hatujawahi kusikia chai imeshuka katika soko la dunia, lakini hakuna Afisa Kilimo anayekwenda kuwasaidia wakulima wa chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo chai inauzwa Sh.200 kwa kilo wilaya ya Rungwe, lakini ukienda Njombe chai inauzwa Sh.500 kwa kilo. Ukienda Lushoto, chai ni Sh.500 kwa kilo. Ni nchi moja, Serikali moja, bei tofauti. Tumelilalamikia hilo na tunaendelea kuuliza kwa nini tuna Bodi ya Chai inayofanana bei zinaenda tofauti, uchumi unakua hauendi sawa, watu wa Mbeya wanapata kidogo, watu wa Lushoto wanapata zaidi. Tunaomba Serikali na hasa Wizara ya Kilimo isimamie suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii kuna mazao ya *vanilla*. Mkulima anaamua kulima *vanilla* kwa sababu jirani yake kalima *vanilla*. Anaambiwa kilo moja ni 400,000 sasa tunataka Maafisa Kilimo waende wawaambie wananchi kama ni kweli hiyo bei iko kwenye soko badala ya watu kuambiana na kuwa na vikundi vya kuambiana zao hili linalipa, lakini mwisho wa siku akilima *vanilla* kwa miaka miwili anakuta soko Sh.50,000 na ametumia gharama kubwa. Tunaomba Wizara ya Kilimo isimamie suala hilo lisaidie

wananchi wasifanye kilimo cha makundi au kusikia kwenye redio mbao, ifuate mfumo wa Serikali kwa kupitia Maafisa wetu wa Kilimo kwenye halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia biashara ya ushindani, leo hii tuna Bandari ya Dar es Salaam, ni bandari ambayo Mungu ametupa wala hatujaitengeneza, ipo. Leo Bandari ya Dar es Salaam kama tusipofanya kwa umakini kama wananchi wa Tanzania Beira inachukua wateja wetu wote wanapeleka Bandari ya Beira, watapeleka Bandari ya Afrika Kusini. Hivyo tunaomba viongozi wetu ambao wamesomea mambo ya *marketing* wajitahidi kusimamia biashara yetu ili Bandari yetu ya Dar es Salaam iendelee kupata wateja na wateja wasitukimbie kwa sababu ya vile viwango vinavyowekwa. Mtu akienda Beira anapewa labda siku 21 ndipo anaanza kulipia mzigo wake. Ukija kwetu mnawapa siku 14. Ni lazima tuwe wajanja na kufikiria kwamba wanaotuzunguka Mombasa na wengine hawapendi maendeleo ya Tanzania, hivyo basi viongozi wajifikirie kujiongeza, wahakikishe wale wateja ambao walikuwa wanapitia bandari yetu, hatuwapotezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda, huwezi kuzungumzia viwanda ukaacha kilimo. Leo hii tunahitaji kupata malighafi kutoka kwenye kilimo ili viwanda vyetu viweze kupata malighafi hapa hapa nchini. Naomba sana tuhakikishe kwamba kilimo hasa mbolea na pembejeo zinafika kwa wakati kwa wakulima. Nilizungumza hata hotuba iliyopita, bila utafiti hatuwezi kufanikiwa, tuwekeze kwenye utafiti. Nilisema *last time* kwamba tuna Chuo cha Uyole ambao wao ni wenzetu wamesomea mambo hayo, tuna *SUA* na asubuhi umezungumza hawa watu wa *SUA* wajikite kwenye utafiti ili kusaidia watu wetu na kilimo chetu tupate mazao ya kutosha ili yaweze kusaidia kwenye viwanda na tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utalii; leo hii tuna majirani zetu wa Kenya, sisi tuna vitu vingi sana vya utalii lakini kuvitangaza tumeweka bajeti ndogo sana. Leo hii miko mingi sana ina vivutio lakini Kaskazini ndiyo inaonekana ina

vivutio vingi kwa sababu Serikali imewekeza huko zaidi. Kuna vivutio vingine ni vidogo. Ukienda sehemu za Njombe unakutana na bustani ya Mungu, unakutana na maua mazuri, tujitahidi kueleza watalii wetu kwamba hata huko pia wanaweza wakaja na uchumi ukaongezeka. Tuna daraja la Mungu sisi kwetu Rungwe, je, watu wetu wanafikaje? Ukienda kwenye daraja la Mungu miundombinu kufikia ni kilometa tano kutoka barabara kuu lakini mpaka ufike barabara ilijengwa na Mjerumani mpaka leo hakufikiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwango vya kutoza watalii. Nimerudia mwanzo nimesema viongozi wetu na wataalam waende hata kwa upelelezi wajue Kenya wanafanyaje na nchi zingine wanafanyaje na sisi tuone kama tunapunguza au tunaongeza kwa faida ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango ulisema uchumi utakua mpaka asilimia 10, ule ulikuwa ni Mpango, lakini mpaka sasa bado hatujafikia, tunahitaji kukaa na kujipima ni wapi tumekosea, ni wapi tuongeze nguvu ili tuweze kuhakikisha tunasonga mbele kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi sana ambayo sisi kama Taifa tunafikiri tukisimamia tunaweza tukasonga mbele. Tunazungumzia maisha bora, ili Mtanzania wa kawaida asilalamike kusema mnasema uchumi umekua, mfuko wangu hauna pesa, ni lazima mzunguko wa fedha uachiliwe kwa wananchi. Unapomlipa mkandarasi kwa wakati, mamantilie atawauzia wale wafanyakazi kwenye barabara, mamantilie yeye akishauza chakula atalipa ada ya mtoto, pesa zitakuwa mfukoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kulipa madeni kwenye Halmashauri zetu, tunahitaji kuwekeza zaidi kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia utawala bora msipokuwa na amani, nakumbuka kuna Waziri mmoja alijibu hapa akasema utawala bora hapa pana amani. Sote tunafahamu unapozungumzia amani lazima uzungumzie na

haki. Tulikuwa na uchaguzi uliopita, uchaguzi uligubikwa na mambo yasiyokwenda sawa kuanzia kwenye wakati wa kujiandikisha, wakati wa kutangazwa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia, naona kengele kama vile.

Unasikia, imeshaita tayari. *(Kicheko)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. Sasa anafuata Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami ya kuchangia kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye vitu vitatu na vyote viko kwenye eneo la kilimo. Nitatumia lugha mchanganyiko. Eneo la kwanza ni *effective utilization of labour force*, *post-harvest loss* na *productivity* kwenye *agriculture*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye *effective utilization of labor force*; ukiangalia Tanzania *majority age group* ni vijana ambao ndiyo tunawategemea waweze kuzalisha. Hawa vijana kama ambavyo nimechangia mchana wakati mzungumzaji alipokuwa anachangia pale walio wengi ni wale waliomaliza kidato cha nne, wengine darasa la saba na wengine wametoka vyuo vikuu. Hawa vijana kama nilivyokuwa nimegusia mwanzoni wanaposikia shughuli za kilimo, ufugaji, iwe ni kulima ni kama vile hiyo kazi ni ya watu fulani ambao sio wao wenyewe. Kwanza wanaumia, hawako tayari kwenda kufanya hizo kazi, kwa

hiyo kama Taifa hatuja-*harness* vizuri ile nguvu ya wale vijana katika kuzalisha mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia China, Wachina wanafanya kazi kama nyuki, angalia Vietnam, Vietnam wanafanya kazi kama nyuki, njoo Tanzania. Saa tatu kamili za asubuhi, mtu ameshatoka shambani yuko nyumbani amekula kishoka. Saa nne kamili za asubuhi tayari ameshakunywa aina ya maji, ameshaanza kuchangamka mpaka saa sita anazungumza Kiingereza. Matokeo yake kama Taifa hatujanufaika vizuri na matumizi ya nguvu za vijana katika kuzalisha ili tuweze kupata mafanikio tunayotaka kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya haya, *vision* na *mission* tuliyonayo kama Taifa huko tunakoelekea kwa spidi, sisi tunaelekea huku, wananchi ambao ni wazalishaji tumewaacha huku. Hivyo kama Taifa nina ushauri sasa, kwenye eneo hili la matumizi sahihi ya nguvu kazi za vijana kwenye kujenga Taifa nashauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kwanza, vileo vipigwe marufuku kuuzwa na kunywewa mida ya kazi. Ni rahisi sana, kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alisimama akakataza viroba na vikapotea, vivyo hivyo katazo linaweza likatolewa wananchi wakabaki wanakunywa muda wa *weekend*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili, nashauri turejeshe mfumo wa kufundisha vijana wetu uzalishaji wakiwa shuleni, nenda sekondari, ukienda sekondari mwanafunzi anasoma kuanzia *form one* hadi kidato cha sita hajawahi ku-*practise* ufugaji wala kilimo. Naishauri Serikali kwenye Mpango huu unaokuja wa miaka mitano turejeshe haya mashamba darasa kwenye shule zetu. Hawa ambao wameshamaliza muda wao umepita tuwaache, lakini hawa ambao wako kwenye shule zetu tuwafundishe kulima na tuwafundishe ufugaji. Wale watakaobahatika kuendelea na Vyuho Vikuu, wataendelea. Wale ambao hawatabahatika waweze kuona hizi shughuli za kilimo kama sehemu ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihamie upande wa kuongeza uzalishaji (*increasing productivity*). Tanzania tumebahatika kuwa na mito, mabonde na ardhi nzuri yenye rutuba. Eneo linalolimwa ni dogo, mkuu wa kaya ambaye mara nyingi ni baba, unakuta kwenye kaya zetu ukienda vijijini hata hapa Dodoma mtu amelima nusu eka, amelima eka moja, ana vimbuzi viwili nyumbani, akiongeza na ng'ombe watatu amemaliza, watu wameridhika. Hii kasi tuliyonayo sisi kama Serikali kwamba watu tufanye kazi *people are relaxing*, hawana haraka, ameridhika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, kupitia mifumo iliyopo ya kuhudumia na kusimamia maendeleo tutoe maelekezo. Tutoe *target* kwa kila mkoa, wilaya na kijiji, ili familia zote za vijijini ziweze kuzalisha. Badala ya kulima eka moja au mbili ziweze kuwa eka nyingi ili nguvu ya Serikali inayoenda kuwekezwa kwenye kilimo iweze kuonekana ndani ya kipindi cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la *post harvest loss* sijaweza kulizungumzia, ila niseme tu kwamba naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara. Tumalize hapohapo Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Nianze kutoa mchango wangu katika Mpango huu wa mwaka mmoja na miaka mitano na nataka kwenda kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukiangalia kilimo cha umwagiliaji katika nchi yetu tunalima hekari 461,376. Kilimo cha uhakika duniani kote lazima utumie umwagiliaji na ukimwagilia maana yake una maji ya uhakika na unaweza kunyeshea na mazao yakaiva kwa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hali halisi kwa sasa Tanzania mvua zinanyesha na hapa Dodoma unaona



mchana kutwa mvua imekuwa ikinyesha, lakini hakuna namna yoyote tunayofanya, kama nchi kuweza kuzuia maji haya. Nashauri katika Mpango huu, Serikali ije na mpango mzuri iweke hela kwenye kilimo, wananchi waweze kutengenezewa mabwawa ili haya maji ambayo yanatoka katika mbingu yanapokuja ardhini yaweze kutiririka kwenye mabwawa, yahifadhiwe na badaye wakulima wetu waweze kunyeshea mashamba na Tanzania tutaokoka kwa kuwa na mashamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mvua hizihizi ndiyo zinazoenda kuharibu barabara. Tumekuwa tukilalamika hapa tangu hotuba ya Rais kwamba *TARURA* iongezewe fedha, lakini tungekuwa na namna ya kuzuia haya maji yaende kwenye mabwawa badala ya barabarani, ni wazi ni rahisi sana kuweza kutumia maji haya ambayo yapo katika nchi yetu kufanya kilimo cha umwagilia. Maji haya yanaharibu barabara. Yanapoharibu barabara maana yake ni kwamba Serikali hiihii pia tunaanza kuilaumu itafute pesa za kutengeneza barabara, kumbe tungeweza kuwa na mpango mzuri wa kuhifadhi maji yanayotiririka, ili maji haya yakaweza kunyeshea mashamba na wakati huohuo tutakuwa tumezuia maji haya yasiende kwenye barabara kuleta uharibifu. Kwa hiyo, nadhani Waziri Mpango na Serikali yake waone namna gani kusaidia kuweka fedha ya kutosha katika uwekezaji kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia bajeti zote zilizopita hazikuonesha wazi kabisa kwamba tumewekeza kwenye kilimo. Kwa mfano leo, *AMCOS* na mashirika madogo madogo ya wakulima yamekuwa yanakopeshwa ili kulima lakini wakati huo wanawekewa *insurance* ya pembejeo hizo, lakini wakati huo wanaenda kudaiwa wakati ambapo Serikali huku hatujawawezesha bado kwa kuwawekea namna nzuri ya kupata mavuno kwenye mashamba yao. Ni lazima tuhakikishe kwamba tunapowakopesha wakulima, wakati huo tumeshawawekea mazingira mazuri ya wao kuzalisha, vinginevyo tutakuwa tuna madeni na tunawadai hawa wenye *AMCOS* lakini hawataweza kulipa. Nadhani masuala haya yanapaswa kuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, pembejeo. Leo hii Tanzania kama nchi, pembejeo zetu zote tunatoa nje. Kwa mfano, mbegu zetu nyingine zinatoka Kenya, Uganda lakini ombi langu kwa nini tusianzishe mashamba ya mbegu katika nchi yetu ili mbegu zisitoke nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati nachangia kwenye Hotuba ya Rais, mbegu zinatoka nje kwa gharama kubwa, ikija hapa kwetu tunauziwa shilingi 13,000 mpaka shilingi 15,000 kwa mfuko. Ni wazi kabisa kwamba mwananchi wa kijijini kule kwa kupanda eka nyingi anahitaji kuwa na *investment* ya kutosha. Tukiwa na mashamba ya mbegu hapa nchini ni wazi kwamba mbegu zitakuwa za bei nafuu na zitaongeza ubora katika uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu ya barabara katika nchi zote ndiyo inayosaidia uchumi wa nchi kupanda. Katika Mpango huu, naomba muangalie barabara kubwa zinazoleta uchumi katika nchi hii. Kwa mfano, kuna barabara ambayo kila siku tumekuwa tukiisema hapa, hii ya Karatu - Mbulu - Dongobesh - Haydom - Simiyu - Bariadi.

Kwa hiyo, barabara kama hizi zikifunguliwa na zikaonekana kwenye Mpango, kwa sababu, ukiangalia kwenye Ilani ya Chama ipo, kwenye Hotuba ya Rais ipo, lakini namna ya kuweka mpango sasa hii barabara ianze kujengwa ndiyo inakuwa kigugumizi, kwa hiyo, kupanga ni kuchagua. Ukipanua hili eneo la Tanzania kama nchi ukawekeza hela kujenga zile barabara za upande ule, kwa hiyo, unapozunguka nchi hii mazao yanatoka kijijini kwenda viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nikuambie ukweli viwanda vyetu vipo, lakini ukimuuliza Waziri wa Viwanda atakuambia hakuna malighafi, lakini nenda kijijini kwa mfano Haydom utakuta alizeti ipo. Itafikaje kiwandani, haiwezekani kwa sababu barabara za kule ni mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika ni kidogo sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Regina Qwaray, atafuatiwa na Mheshimiwa George Nathan Malima.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza Waziri wa Fedha kwa taarifa yake nzuri aliyoianda. Pia niipongeze Kamati ya Bajeti kwa kuandaa vizuri taarifa yao. Kwa namna ya pekee pia, niipongeze Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa inayofanya kuhakikisha Tanzania inazidi kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite katika sekta ya kilimo. Kilimo ni msingi wa uchumi wa viwanda na uti wa mgongo wa Taifa letu. Wananchi wengi wa Tanzania tunategemea kilimo ili kujikwamua kiuchumi, hasa wananchi wa vijijini wanategemea kilimo kujipatia mahitaji yao. Mwananchi wa kijijini anategemea kilimo kusomesha mtoto, kupata mahitaji yake ya msingi ikiwemo afya, yaani kilimo ndiyo kila kitu kwake. Pamoja na hayo yote bado wanakumbana na changamoto nyingi ikiwemo soko kwa maana kwamba baada ya mavuno, wananchi hawana soko la uhakika. Wanavuna lakini mwisho wa siku mazao yao hayapati soko kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kilimo wanacholima kwanza kinakuwa hakina tija. Wanatumia vitendea kazi vilivyopitwa na muda. Akina mama wengi wa kijijini wanajihusisha sana na kilimo lakini hawana vitendea kazi vinavyowarahisishia kufanya kilimo kile kuwa chepesi zaidi. Hivyo inakuwa vigumu sana kupata tija au kupata manufaa kupitia kilimo. Wamama hao leo wanahangaika kutumia jembe la mkono katika kilimo, hawawezi kulima mashamba makubwa hivyo, wameishia kulima mashamba madogo madogo ambayo sasa mazao wanayoyapata ndio hayohayo wanatumia katika chakula na katika mahitaji mengine, mwisho wa siku wanaendelea kudhoofika kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo bado naendelea kushauri Serikali kuona ni namna gani watainua sekta hii ya kilimo ili wananchi wetu wa vijijini waweze kujikwamua kiuchumi. Kwanza nishauri Serikali iwekeze katika utafiti wa mbegu tunazozitumia. Mbegu zetu nyingi tunazotumia zinatoka nje ya nchi, asilimia kubwa mbegu za mahindi na mbogamboga hazizalishwi hapa nchini hivyo, husababisha wananchi kutumia gharama kubwa kupata mbegu na kutumia mbegu ambazo sio bora katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali ifundishe wakulima wetu kuhifadhi na kusindika mazao ili waweze kuuza bidhaa badala ya malighafi. Pia nishauri pia Serikali kujenga mabwawa ya kuvunia maji ili kuboresha *scheme* za umwagiliaji. Mfano, katika Wilaya ya Babati kuna Vijiji vya Shauri Moyo, Masware, Kisangaji, Bonde la Kiru, Madunga, Narkash, vyote vinategemea kilimo cha umwagiliaji, lakini hawana uwezo mkubwa au teknolojia ya kutosha kuvunia maji ili waweze kuendesha kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wengi hawana elimu ya kutosha. Hawaelewi ardhi yao wanayoitumia ni mazao gani hasa yanastawi, hivyo wanastawisha mazao ambayo wakati mwingine hayaendani na maeneo yao. Maafisa Ugani katika maeneo yetu bado ni wachache sana. Niishauri Serikali kuongeza Maafisa Ugani katika kila kijiji ili waweze kuwaelimisha wananchi wajue ni mazao gani yanastahili kustawishwa katika maeneo yao, lakini pia waweze kutoa shamba darasa. Yale mafunzo ya shamba darasa yanasaidia wananchi kuona kwa vitendo ili waweze kuzalisha mazao yale yanayoendana na maeneo yao na pia yaweze kuwaletea tija. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia vyuo vya kilimo viboreshwe. Vyuo vyetu vya kilimo haviendi kulingana na ukuaji wa teknolojia. Bado tunatumia mbinu zile za zamani katika kuwapa mafunzo wale wataalam wa kilimo ambao wana kazi ya kwenda kuwaelimisha wakulima hawa, ili waweze kuzalisha mazao kwa kiwango kikubwa. Mfano,

Chuo cha Sokoine nashauri Serikali ione ni kwa namna gani kiendelee kubaki na kutoa taaluma inayohusiana na kilimo, uvuvi badala ya kujikita katika kutoa fani ya ualimu. Kama inavyotambulika ni Chuo cha Kilimo, kibaki katika kutoa fani ya kilimo badala ya kujishughulisha na fani nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika Mkoa wetu wa Manyara, tunaomba Chuo Kikuu cha Sokoine kuanzisha shamba darasa katika mkoa wetu, ili wananchi wa mkoa ule waweze kufaidika na mafunzo ya kilimo na mwisho waweze kulima kilimo chenye tija na kufaidika na kilimo hatimaye kuleta maendeleo na mapinduzi katika viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Regina Qwaray. Nilishakutaja Mheshimiwa George Nathan Malima, Mbunge wa Mpwapwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Tarimo. Mheshimiwa Malima hayupo?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Sawa, basi Mheshimiwa Priscus Tarimo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Kajjage.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Niendeleo kuwashukuru wapiga kura wangu wa Moshi Mjini kwa namna wanavyoendelea kuniunga mkono na kunitia moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajaribu kwenda kwa harakaharaka kutokana na muda, lakini nianzie kwenye kilimo. Kwenye kilimo mpango ulioletwa ni mzuri lakini unahitaji kujaziwa mambo mengi ambayo mengi wameyataja Wabunge wenzangu lakini na mimi niongezee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema tunaweka nguvu kwenye kilimo na tunaendelea kutegemea kilimo cha maji

ya mvua, tutakuwa tunapoteza muda. Wakati tatizo la mabadiliko ya tabianchi linaendelea kuwa kubwa, tukitegemea kilimo bila kuwa na mpango madhubuti wa umwagiliaji tutakuwa tunapoteza muda. Bwawa la Nyumba ya Mungu lililoko kwenye Mkoa wa Kilimanjaro lilijengwa miaka ya 67, lina faida kubwa pamoja na kuzalisha umeme, kuna samaki lakini mabwawa kama haya yanaweza kutengenezwa ili kusaidia umwagiliaji ili kilimo chetu kiwe chenye tija. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona mpango wa kilimo cha *large scale*. *Block farming* kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wadogo ni kizuri lakini kama tunataka kilimo kilete tija ni vizuri tuwe na sera pia ambazo zitasaidia wakulima wakubwa waweze kuwekeza katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna eneo ambalo nadhani Wizara inabidi ilifanyie kazi zaidi. Nadhani suala hili Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo alishaliongelea siku za nyuma kwamba ni lazima Sera ya Viwanda iwe na mwingiliano wa karibu na Sera ya Kilimo. Kwa mfano, sasa hivi tuna matatizo ya mafuta ya kula lakini tunaona tumefeli kwenye alizeti kwa maana ya kwamba *demand* yetu imekuwa kubwa kuliko *supply*. Hata hivyo, Kigoma kuna mawese huoni kinachofanyika ambacho kitaleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tunaagiza sukari lakini mwenzetu wa Kilombero amesema wanatupa sijui tani za miwa 40 kila msimu. Juzi tu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alikuwa na kikao na wakulima wa ngano kwa maana ya kwamba tunaagiza ngano nyingi. Kwenye haya mazao ambayo *demand* yake ndani tayari ni kubwa kwa nini kusiwe na mpango wa muda mfupi na wa muda mrefu mpaka miaka 20 kuhakikisha tunakidhi soko la ndani la mazao haya ikiwa ni pamoja na kuweka viwanda vyake? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi ambayo inaenda kukamilika. Nimejaribu kuangalia sijaona mpango ulionyooka wa ku-*support SGR* kwa mfano. Ningefurahi sana kama ningeaona tayari kuna juhudi za kuongea na nchi kama Congo

kuhakikisha kwamba watatumia *SGR* kwa ajili ya kusafirishia mizigo yao itakapokamilika. Hii ikiwa ni pamoja na kuangalia namna ya kuunganisha Bandari ya Dar-Es-Salaam kwenye viwango vyake, kuna mtu amesema hapa na kuitangaza ili kwenye hii miradi ambayo inaenda kuiva karibuni tuone ni namna gani itaingiza fedha ili kusaidia mipango hiyo, sijaliona. Mimi nilitegemea sasa hivi kuwe kuna *economic diplomacy* ya kuangalia nchi kama za Rwanda, Burundi, Congo, tunatafuta njia gani watapitisha mizigo yao yote hapa kwetu, hiyo ni pamoja na *ATCL*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye utalii nako bado kuna matatizo. Kwanza niseme tu wale wafanyabiashara wa utalii na Mkoa wa Kilimanjaro ni mmoja wa maeneo hayo, wana kilio kutokana na janga hili la *corona*. Biashara zao zimekwenda chini sana, wanaomba Serikali iwaangalie japo hata kwenye tozo ili kuwapunguzia makali. Hata hivyo, kuwepo kwa *ATCL* nilitegemea kuwepo kabisa na mkakati wa kuunganisha na baadhi ya mashirika ya kimataifa, ili i-*promote* utalii kwa ndani ili sasa tuanze kupata fedha kutika kwenye mashirika haya ya kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mikopo hasa kuwainua wafanyabiashara wadogo, nilishasema kwenye kuchangia hoja mwanzo kwamba tuangalie uwezekano wa kumkopesha mtu mmoja-mmoja. Pia hapa kwenye umri tuliojiwekea hasa kwa vijana, sina shida sana na akina mama, tumesema vijana ni miaka 18 mpaka 35, lakini vijana wa Kitanzania wenye miaka mpaka 45 wana nguvu ya kuweza kufanya kazi na kuzalisha. Tujaribu kuangalia sheria zetu kwa nini vijana sasa miaka 36 mpaka 45 hawakopesheki kwenye fedha hizi ili kuchangia kwenye pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TARURA*, huwezi kusema kilimo bila kuwa na miundobinu iliyo sawa. *TARURA* wamepewa jukumu, najikita kwenye kuishauri Serikali itafute namna bora ya kuipatia *TARURA* chanzo cha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa ninyi nitakaowataja hapa mwishoni kwa sababu mmekuwa wa mwisho kabisa na mmekuwa na subira sana nitawapeni dakika kumi-kumi endapo muda wangu utatosha.

Kabla ya hapo niwajulishe Waheshimiwa Wabunge kwamba kwenye *tablets* zenu kuna mabadiliko ya ratiba ya Mkutano huu ambapo mabadiliko hayo yanatupeleka hadi keshokutwa, Jumamosi. Kwa hiyo, naomba muangalie kuona mabadiliko hayo na *time table* yenyewe imeambatanishwa pia kwenye *tablets*.

Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza, naomba nianze kupongeza Serikali kwa kuleta Mpango huu mzuri, pamoja na mipango mingine yote iliyotangulia tuliona kwamba ina nia ya kuhakikisha tunafikia Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025 sanjari na kukuza malengo endelevu ya *SDGs*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu umekuwa na nguzo muhimu tatu, ikiwa ni utawala bora, maendeleo ya watu pamoja na kukuza uchumi. Kukuza uchumi ni kuwekeza katika sekta za kiuchumi na kiuzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa muda mrefu imeendelea kuingia katika mikataba na makubaliano mbalimbali aidha kupitia wahisani, mikopo, uwekezaji ambalo ni jambo jema sana, lakini tumeona mara nyingi Mheshimiwa Rais amekuwa akihoji, ndugu zangu hivi kweli huu uwekezaji una tija? Hivi hii miradi ina tija? Tija ni nini basi? Tija ni uwiano kati ya kitu unachowekeza na kile kinachopatikana, lakini kikionyesha mabadiliko chanya katika mtu mmoja mmoja, katika taasisi na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tija ni nini ili kama mwekezaji anaweka mradi wake au analeta msaada wake au anaweka kampuni yake, mwisho wa siku anapoondoka



aache ajira endelevu, aache ujuzi, akuze ujuzi kwa wale ambao wanahusika na pia kubwa kabisa waache teknolojia pamoja na ubunifu. Yaani mradi unapokwisha asiondoke yeye na vitu vyake akaacha vitu vitupu. Kwa mfano katika kuwekeza 100% kwa maana ya *consultancy* anaanzisha mradi yeye 100% mgeni anakuwepo pale pengine *engineer* wetu au mtaalam wetu anashuhudia tu msumari unavyopondwa pondwa kwenye shirika hilo au kwenye kampuni au mradi au mashine inavyofungwa, lakini ule ujuzi hashiriki moja kwa moja, anapondoka anaondoka na ujuzi wake mwekezaji. Kwa hiyo ifikie sehemu, nashauri Serikali hii miradi safari hii, tunaona watu wengi wanalalamikia miradi ya maji, miradi mbalimbali ambayo tumeingia lakini kama nilivyofafanua nini maana ya tija. Je miradi hii inaacha tija kweli? Kwa nini? Sasa ifikie sehemu tutumie chombo kile kinaitwa chombo cha kukuza tija na ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani lilitwa Shirika la Tija la Taifa, chombo hiki kipo na kipo vizuri chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu chombo hiki sasa kipewe meno kipewe uwezo ili kuondoa haya malalamiko yote ambayo yako kwenye miradi ambayo ina mambo mengi ambayo ni baadhi lakini kwa kweli ni mingi, miradi ambayo imekuwa ina-*fail*. Chombo hiki kabla miradi au mikataba hajaanza kutekelezwa, chombo kikaangalie kikapime hii miradi itakuwa na tija kama nilivyoeleza maana ya tija ili baadaye kusiwepo na malalamiko. Huu ni wakati wa kukipa chombo hiki meno na uwezo maana tunacho, tunacho kwenye Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia viwanda tulivyopata ni vingi sana kwenye nchi sasa hivi. Kweli ni vingi na ni vizuri, ni jambo jema, lakini chombo hiki bado kina uwezo wa kwenda kutathmini vile viwanda, kufanya *analysis* na kutoa ushauri ili mwisho wa siku viwanda visiwe vya kupotea, viwe vina-*sustain* vinakaa muda mrefu yaani vinaendeleza kuwa na tija, maana yake havikufanyiwa huu upekuzi mwanzo ndiyo maana tunaona kuna malalamiko mengi, kwenye viwanda hatujui itakuwaje baadaye na miradi imeshaonyesha jinsi ilivyokuwa kwenye Mipango iliyopita. Kwa hiyo, nashauri chombo hiki kitumike ili kilete tija katika miradi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitoe mfano, wenzetu China wakati wanaandaa *Olympic* 2008 walikuwa wametoa nafasi kwa wawekezaji, lile ni jambo kubwa lilihitaji watu wawekeze kwa wingi, lakini walikuwa wakali, wakasema unakuja kuwekeza ndiyo, lakini kuanzia mwanzo wa mchakato wa kutaka kuwekeza, kama ni kujenga uwanja wewe mwekezaji utafanya kazi kwa asilimia 70 na sisi wazawa *consultancy* mzawa atafanya 70 ili pale wanapomaliza watapata faida ya 70% yes lakini 30% kutoka anapowekeza anajenga kiwanda au anajenga uwanja ile pesa inabaki ndani inazunguka kwa sababu yule mwekezaji wa ndani (*consultancy*) alikuwepo toka mwanzoni. Kwa hiyo inabidi kuangalia mfano wa wenzetu, wameendelea lakini wako makini sana na mali yao na mzunguko wa pesa yao ndani mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwenye suala la afya, na-*declare interest*, suala zima la kada ya *physiotherapy*. Naipongeza Serikali sana imefanya bidii nyingi lakini taaluma hii ambayo ni matibabu kwa njia mbalimbali ikiwemo mazoezi tiba, wataalam ni wachache, wenye shahada hawazidi 100 kwenye nchi nzima, lakini pia chuo ambacho kinatoa shahada hii ya *physiotherapy* Kiswahili chake matibabu ya njia mbalimbali ambayo pia ni mazoezi tiba, ni KCMC peke yake. Niipongeze Wizara ya Afya sasa ina mpango wa kuanzisha hii kozi kwenye Chuo cha Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado haitoshi, naomba niishauri Serikali ifanye uanzishaji wa kozi hii kwenye Chuo cha *UDOM* na Bugando. Hawa watu wanahitajika sana kwa sababu tunafungua hospitali nyingi za mikoa kwa bidii na pia hospitali za wilaya, pamoja na vituo vya afya. Pia nashauri kwa sasa kwenye vituo vya afya na hospitali za wilaya, hivi vitengo viwekwe, havipo, tufikirie viwekwe na wataalam waongezeke, wapelekwe kule kwa sababu ni idara muhimu sana, lakini ina watu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia pawepo na wazo la kuongeza Shahada ya Uzamili na Uzamivu

ikiwezekana ya kada hii ya *physiotherapy* hatuna kwenye nchi yetu. Ili upate Shahada ya Uzamivu lazima uende nje ya nchi. Kwa hiyo nilikuwa nashauri hili jambo litekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Dkt. Alice Kaijage kwa mchango wako huo. Mheshimiwa Martha Gwau atafuatiwa na Mheshimiwa Nashon Bidyanguze.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mpaka kufikia siku ya leo. Pia naomba niishukuru familia yangu kwa *support* waliyonipa kipindi chote. Naomba nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kwa kurudisha jina langu na kuniwezesha kuwa hapa lakini mwisho, naomba niwashukuru wapiga kura wangu akinamama wa Mkoa wa Singida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi kuchukua nafasi hii kuchangia Mpango huu wa Miaka Mitano tunayoiendea. Kwanza naomba nimpungeze Waziri kwa hotuba nzuri lakini maelezo mazuri yanayohusiana na Mpango huu ambao naamini yamejikita kwenye kusaidia wananchi na hasa wale wenye kipato kidogo. Mchango wangu kwa siku ya leo nitauelekeza kwenye kilimo ambapo najua wachangiaji wengi wameshachangia, lakini kwa sababu ni suala ambalo linagusa mtu wa chini, kwa hiyo tunalongelea mara kwa mara na tunaamini kwamba yule mtu wa chini ndiyo mlengwa hasa ambaye anapata shida na ndiyo mwenye kipato cha chini. Kuna usemi wa *three knows* wanasema; *no pharmacy, no food, no future*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwa mimi ninayetoka Mkoa wa Singida naomba nijikite kwenye zao kubwa la alizeti. Hili zao, wewe mwenyewe ni shahidi kipindi cha nyuma kama miezi mitatu iliyopita tumepata uhaba wa mafuta. Pia tuna mashamba ya kulima, tuna watu wenye

nguvu za kulima ili hii alizeti itosheleze sisi kwa mwaka mzima na hata kupata ziada ambayo itasababisha sisi tukasafirisha kwenda kuuza. Kwa hiyo naomba pamoja na Mpango mzuri wa Wizara ya Kilimo, hili zao la alizeti tulipandishe hadhi liwe kama zao la korosho na mazao mengine ya kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Tukipandisha hadhi hili zao tutakuwa na *guaranteed market* lakini pia tutakuwa na *guaranteed price* kama yalivyo mazao mengine kama korosho, lakini pia litatusaidia sisi Watanzania na watu walioko nje ya Tanzania. Kwa kulipandisha hadhi tuhakikishe kwamba mbegu bora zinapatikana ambazo tukikamua mafuta ya alizeti tutapata mengi ukilinganisha na sasa hivi mbegu zilizopo mafuta yanayotoka ni 40% tu. Tukipata mbegu bora tukapata bei bora ya mbegu ambayo mkulima wa chini anaweza ku-*afford* kununua, itasaidia hili zao listawi lakini pia tuuze kwa Mkoa wetu wa Singida lakini hata na mikoa mingine ya jirani waweze kulilima na kupata faida kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni utafiti ambao utasaidia, siyo tu kwa Mkoa wa Singida najua Mkoa wa Singida zao linastawi vizuri, lakini utafiti ukifanyika ina maana hata na mikoa mingine itaweza kulima hili zao la alizeti. Mwisho wa siku hatutapata hii aibu ya kuagiza mafuta nje ambapo tunatumia pesa nyingi sana kuagiza na wakati hizo *resources* tungeziweka kwa wakulima wetu, tungewa-*empower* wananchi wetu, wakalilima na wakapata masoko, huu uhaba wa mafuta hautakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni zao la vitunguu ambalo linapatikana Mkoa wa Singida. Nalo hilo tulipandishe hadhi, tukipandisha hadhi litatusaidia tatalima Singida na mikoa mingine watalima pia. Kwa hiyo kwa upande wa kilimo nilitaka nijikite kwa hilo. Tuna *SIDO* wanaweza wakatusaidia kutoa elimu kwa wakulima wetu kwa viwanda vyetu vidogo vidogo ambavyo vikitaka kusindika mafuta na vitataka kufanya shughuli nzima za uzalishaji

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine naomba niongelee suala la...

**SPIKA:** Samahani Martha lipandishwe hadhi kwa kufanyaje?

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Kuwa zao la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine naomba niongelee suala la usafiri. Tunajua uwekezaji ndiyo kila kitu kwa sasa hivi na ndiyo unasaidia pato la Taifa na ajira kwa vijana wetu. Usafiri wa anga ni kitu muhimu sana ambacho mwekezaji anakiangalia, awe wa ndani awe wa nje. Kutoka Dar es Salaam mpaka Singida ni masaa 12 kwa gari, sasa tukifungua viwanja vya ndege, tukapata ndege, mwekezaji atatumia saa 1.30 kufika Singida kuona fursa zilizopo ambazo ataweza kuwekeza. Sio tu mwekezaji wa nje lakini hata mwekezaji wa ndani, mtu wa Mwanza atakuja Singida mara moja, ataona fursa, ataondoka, nami wa Singida nitaenda Mtwara, nitaona fursa naondoka, kwasababu ya usafiri ambao ni ndege itakuwa ni rahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipongeze kwa kweli Shirika la Ndege, mikoa mingi imepata ziara hizo na viwanja. Tunaiomba Serikali kwa mikoa ambayo ya kimkakati kama Singida itusaidie uwanja wa ndege ili tuweze kupata fursa watu wote waone mazao yetu, tuna uchimbaji wa madini, tuna zao la alizeti, tuna mambo mengi ambayo yanaendelea Singida, tukipata kiwanja cha ndege na ndege itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho la kumaliza, ni suala la usafiri wa treni. Tuna treni yetu ya Singida ambayo ilikuwa inasaidia wakulima wetu kusafirisha mazao kwa bei rahisi kutoka sehemu moja mpaka nyingine. Kwa hiyo, hiyo ilikuwa inampa fursa mwananchi wa Singida kujua soko liko wapi. Kama liko Mwanza, atapeleka mazao yake akauze kule, kwa sababu ulikuwa ni usafiri *affordable* lakini pia na bei kidogo ni nzuri. Kwa hiyo naomba Serikali iangalie hili la

kufufua treni ya Singida ili itusaidie kwenye suala zima la kusafirisha mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nataka niwakaribishe wote Mkoa wa Singida, tuna uzinduzi wa kitabu cha uwekezaji kwa mkoa, tarehe 23 Januari mje mjionee fursa mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge mnaweza kupenda kuwekeza na niwakaribishe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nikushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Martha umesema tarehe 23 Januari.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Samahani ni tarehe 23 Februari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, kungea kwa mara ya kwanza ni shughuli. Mheshimiwa Nashon Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Mpango kwa taarifa nzuri aliyoleta mbele yetu na naomba nichangie eneo la kilimo na uvuvi kama muda utanitoshia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii niwashukuru Wanajimbo la Kigoma Kusini kwa kunichagua, lakini pia nikishukuru Chama Cha Mapinduzi kuweza kurudisha jina langu ili niweze kupeperusha bendera ya kutetea Jimbo la Kigoma Kusini ambapo nilishinda kwa kishindo na pia Mheshimiwa Rais alipata kura nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niwashukuru familia, hawa watu kama wasingeweza kunipa *support* nisingeweza kufika hapa nilipo; mke wangu pamoja na watoto lakini zaidi sana ndugu yangu mmoja ambaye anaitwa Gervas;

Mkurugenzi wa *World Worth*. Huyu mtu alilifika kwenye mkutano wa kampeni wakati mimi nazindua tarehe 11 Oktoba, 20. Aliwaambia wananchi, mkimchagua huyu bwana Bidyanguze mimi nitamchangia milioni 50 kuongezea kwenye Mfuko wa Jimbo wa Serikali. Jambo la ajabu sana, kwa hiyo nataka nikwambie kuanzia sasa tayari katika Mfuko wa Jimbo ule ambao nilifadhiliwa na mwanaume yule tayari nilishapeleka milioni 12 mifuko ya cement 600 ya thamani ya milioni 12. Huyu mtu lazima nimpongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nichangie Mpango huu kwenye eneo la kilimo. Kilimo ni kweli ndiyo uti wa mgongo, lakini kwa bahati mbaya sana naomba nishauri Serikali, bado haijaweka miundombinu mizuri yaani ile ambayo inatamanisha wananchi waweze kupenda kilimo. Serikali bado inasaidia tu wale ambao wameitikia kilimo, mimi najjuliza wako vijana wengi wanaingia shule za sekondari wanamaliza vyuo vikuu, wote hawa plan yao ni kuajiriwa. Naamini Serikali haina uwezo wa kuajiri wote hao, sasa tufanyeje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Serikali ije na mpango wa kushawishi wananchi, hawa vijana ambao ni kundi kubwa, waweze kupenda kilimo. Kilimo wanakikimbia, si tunao majimboni kule, wapo ambao wamesoma wamemaliza vyuo vikuu lakini hawana kazi, lakini ukiwaambia twende tujajiri kwenye kilimo hawana habari na hicho kitu. Sasa nadhani katika eneo hili la kilimo, yuko mchangiaji mmoja amezungumza vizuri na sikumbuki vizuri, hivi tathmini ya wanafunzi ya wanaokwenda kujifunza kilimo kusoma masomo ya kilimo hivi ni wangapi? Naona kama ni wachache sana, kwa sababu gani? Kilimo wanakikimbia na wale ambao wanalima wanakwenda kuchoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani Wizara ya Kilimo ije na mpango ambao utatengeneza ushawishi ili watu waweze kulima. Kilimo kimetafsiriwa kwamba ni kwenda na jembe la mkono kwenda kulima, mtu aliyesoma hawezi kwenda kulima kwa kilimo hicho. Kwa hiyo tunatakiwa Serikali ije na mpango wa kusaidia kutoa mashamba maana

mashamba yenyewe kuyapata ni kazi. Mashamba yapatikane kwa njia nyepesi kama vile ambavyo Serikali inahamasisha uwekezaji tuhamasishe uwekezaji ndani ya kilimo kwa watu wetu hawa vijana, tukishafanya hivyo, watu watakipenda kilimo, lakini mwisho wa siku lazima kilimo kile Serikali iweke utaratibu wa kupata masoko kwa ajili ya mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mkulima kwa kiasi fulani, niliwahi kulima maeneo ya Tanga kule, lakini tuliwahi kupata mahindi mengi wakati fulani nadhani ilikuwa elfu mbili kumi na ngapi sijui, lakini Serikali kwa sababu ya kuhitaji kutunza chakula ndani ya nchi ilikataza watu kusafirisha mazao nje ya nchi. Hata hivyo, yenyewe Serikali haikuwa tayari kuyanunua. Sasa wewe fikiria, mtu amekwishalima na amekwishavuna, asafirishe akauze, apate fedha anazuiliwa na Serikali ni jambo jema, lakini basi yanunue hayo mazao. Kwa hiyo nafikiri kwenye eneo la kilimo tukilifanyia kazi ni sehemu nzuri sana ya kuajiri watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ufugaji pia; ufugaji ni kama kilimo. Sisi Kigoma tunalo Ziwa Tanganyika lina samaki wengi sana lakini elimu haipo ya uvuaji wa samaki, ni eneo moja ambalo kama Serikali ingejikita kufundisha na kutoa nyenzo kwa ajili ya watu waweze kuvua, nadhani vijana wetu hawa ambao wako katika shule na wanaingia kwenye shule na vyuo vikuu wangeweza kujikita baada ya kutoka kule, kuja kuingia kwenye habari ya uvuaji wa samaki. Habari hii ni ajira kubwa sana na ingeleta tija kubwa sana na fedha nyingi kwenye kuongeza kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nafikiri hili nalo lazima tuliangalie sana, kuliko kufikiria tu kwamba lazima mtu asome awe nani. Nasema hivi, watu wengi sasa hivi wanafikiria kila mtu awe Mbunge, wanafikiri kwamba kwenye Ubunge kidogo kuna nafuu, lakini Jimbo la Kigoma Kusini, Jimbo la Mwibara na mengine, hivi wote kama watafikiria kuja huku ni kwa nini? Ni kwa sababu inaonekana kidogo Mbunge akirudi kutoka Bungeni, anakuja amevaa vizuri,



anaonekana anafaa. Kwa hiyo, nadhani Serikali iwekeze katika kilimo na uvuvi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuchangia hayo. Ahsante *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nashon Bidyanguze. Mheshimiwa Ng'wasi Kamani atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Mshua.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Mwaka Mmoja. Nianze kwa kumpongeza Waziri Dkt. Mpango kwa Mpango huu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kama mwakilishi wa vijana nina machache tu ya kushauri juu ya namna gani tunaweza tukashughulikia au kutatua tatizo la ajira. Wote ni mashahidi kwamba kila Mbunge anayesimama ni dhahiri anakerwa na tatizo la ukosefu au upungufu wa ajira kwa vijana. Nina ushauri wa namna mbili tu na ndiyo zitakuwa *points* zangu za msingi kwa jioni ya leo. Kwanza, ni namna gani tunaweza kutumia Mifuko ya Hifadhi za Jamii kutatua changamoto ya ajira; na pili, namna gani vijana tuafikia uchumi wa kweli wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la namna gani tunaweza kutumia Mifuko ya Hifadhi za Jamii kutatua changamoto ya ajira, nianze kwa kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira kwa kuleta katika Bunge hili Tukufu Sheria ya Mifuko ya Hifadhi za Jamii, mwaka 2018 na Bunge hili Tukufu likapitisha sheria hiyo ambapo mpaka sasa mifuko yetu tunaendelea nayo vizuri. Ni-*declare* kwamba niko katika Kamati ya Katiba na Sheria ambayo inasimamia mifuko hii. Kwa hiyo, nafahamu namna mifuko hii inafanya kazi na mpaka sasa imefikia wapi. Napenda tu kusema kwamba

tusiamini yale tunayosikia kwamba mifuko hii haiko vizuri. Mifuko hii inaendelea vizuri na tunaamini itakwenda kufanya vizuri zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018 ilipotungwa Sheria hii ya mabadiliko ya Mifuko ya Hifadhi za Jamii, kifungu cha 91(1) cha Sheria ya *NSSF* kinaruhusu mfuko huu kupokea michango kutoka kwa watu walioko kwenye *informal sectors* au ajira zisizo rasmi. Watu hawa wanatoa michango ya shilingi 20,000/= tu kwa mwezi ambayo ni sawa na shilingi 650/= kwa siku. Baada ya kupokea michango hii, mtu akishafikisha miaka miwili, anakuwa na uwezo wa kupokea fao ambalo ni aidha atapata vifaa, mashine au mtaji wa kuanzisha kiwanda kidogo. Hii inafanyika kupitia *SIDO* na Benki shirikishi za mfuko huu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kama ifuatavyo. Changamoto ya kwanza tunayokutana nayo sisi kama vijana hasa wale ambao tunatoka vyuoni, kwanza anayetaka kuajiriwa katika mfumo ulio rasmi, anapata changamoto ya kukosa uzoefu (*experience*). Pia yule anayetaka kwenda kujajiri, hana mtaji na hakopesheki katika benki na taasisi nyingine za fedha kwa sababu hana *collateral* au dhamana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tukiamua kupeleka utaratibu huu kwenda vyuoni moja kwa moja, tukahamasisha vijana walioko katika vyuo na vyuo vikuu kuweza kupata mchango wa Sh.20,000/= kila mwezi, ambapo kijana huyu atachanga kwa muda wa miaka miwili, mitatu au minne kutegemea na kipindi chake anachokaa chuoni. Akitoka hapo, kijana huyu kupitia benki hizi shirikishi chini ya Mfuko wa *NSSF* na *SIDO* anakuwa anaweza kukopesheka aidha mashine, kifaa cha kazi au anaweza kukopesheka kwa mtaji kwa ajili ya kuanzisha viwanda vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Wizara husika ikikaa na kuangalia mpango huu, itakuwa tumepata mwarobaini wa tatizo la ajira kwa vijana wanaotoka katika vyuo na vyuo vikuu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, napenda kusema kwamba tutakuwa ndiyo tumeondoa tatizo la ajira kwa upande wao, lakini tutakuwa tumeiongezea nguvu mifuko hii ambayo kwa namna moja au nyingine naweza nikasema ni *National Security*. Kwa sababu fedha hizi ndizo zinazotumiwa na Serikali yetu kuwekeza katika miundombinu na katika huduma mbalimbali za jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, vijana hawa wakienda kujiajiri wenyewe...

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, VIJANA, KAZI, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Mheshimiwa Ng'wasi ukae chini halafu uzime *microphone*. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, VIJANA, KAZI, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nampongeza sanasana Mbunge huyu kijana kwa mchango wake na umahiri mkubwa wa kiushauri anaoutoa sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa kwamba kwa hesabu na taarifa niliyonayo kama Waziri wa Sekta kwa sasa, Mfuko wa *NSSF* ambao unashughulika na *private sector*, asilimia 100 ya makusanyo, ni asilimia 40 tu ndiyo inayotosha kulipa aina zote za mafao na kubakiwa na asilimia 60 ya makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa asilimia ile 60 ya makusanyo, mimi kama Waziri wa Sekta, kwa kushirikiana na vijana wazalendo kama huyu anayechangia hapa, tukatengeneza kwa pamoja programu nzuri, nadhani ushauri huu unaweza kuwa ni muafaka kabisa wa kutafuta mwarobaini kwa ajili ya kuwahudumia vijana wetu na kutatua tatizo la ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwa taarifa hii kwa kweli ningefurahi kumpa Ubalazi au Champion wa kuwasaidia vijana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea na nitafurahi sana kuwa Balazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, tumesikia hapa kwamba kuna changamoto kubwa sana katika mikopo ya elimu ya juu. Mpango huu kama ukifanikiwa, utasaidia vijana hawa wanaotoka vyuoni moja kwa moja kuingia katika mpango wa kujijiri na kuajiri wengine kuweza kuanza mara moja kurejesha mikopo yao ya elimu ya juu na kuepuka suala zima la riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 inaahidi kwamba kuna ajira milioni nane ndani ya miaka hii mitano zinatakiwa kuzalishwa. Kwa mpango huu, kama ukifanikiwa, maana yake suala hili la ajira milioni nane linakwenda kuwa rahisi na linakwenda kufanikiwa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *point* yangu ya pili inakwenda sambamba na hii, ni namna gani vijana tutafikia uchumi wa kweli wa viwanda? Tunapozungumzia uchumi wa viwanda hasa kwetu sisi vijana ambao ndiyo kwanza tunaanza maisha, hatuzungumzia viwanda vya *billions of money* au *millions of money, a hundred of millions*, hapana; tunazungumzia viwanda vidogo vidogo ambavyo kila mtu atakuwa na uwezo wa kukianzisha kwenye chumba chake au kwenye nyumba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi vitawezekana tu kwetu sisi vijana kama tukitoa bajeti ya kutosha kwenda kwenye *SIDO* na *TIRDO*. Taasisi hizi ndizo pekee ambazo zina uwezo wa kutusaidia sisi kupata mashine zenye *efficiency* sawa lakini kwa gharama ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mfano wa mfanyabiashara aliyetaka mtambo wa kutengeneza *ethanol* kwa kutumia zao la mihogo. Mtambo huu huu Brazil na China ulikuwa ni shilingi milioni 850, lakini mtambo huu huu, *model* ile ile baada ya kuwa *studied* na TIRDO wametoea mapendekezo ya kuweza kuutengeneza kwa shilingi milioni 150. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni nini? Mitambo ambayo tunaweza kuipata katika nchi jirani kwa gharama kubwa, tunaweza tukaitengeneza sisi wenyewe katika nchi yetu kwa gharama ya chini ambayo itatusaidia vijana kuweza kushiriki moja kwa moja katika uchumi wa viwanda na kukuza pato la Taifa. Naomba katika Mpango huu mawazo haya tuyaangalie namna tunavyoyaweka ili sisi kama vijana tupate kunufaika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado deni la msingi linabaki kwa Wizara ya Elimu. Vijana tukitoka vyaoni, hata tukitengenezewa mazingira mazuri kiasi gani, kama elimu tuliyopata katika shule tulizosoma haitusaidii au haitu-*equip* kuweza kuwa na uelewa wa kutosha wa kijamii, maana yake mambo haya yote ni bure. Mama yangu Mheshimiwa Ndalichako nakuamini, naomba sana mpango mfumo wa elimu uangaliwe kwa kushirikisha wadau wakiwemo vijana, nini hasa kinaweza kubadilishwa katika mfumo wetu wa elimu ili vijana watoke shuleni wakiwa na uwezo wa kuishi katika jamii zetu (*real societies*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, naunga mkono hoja, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ng'wasi. Umejithahidi sana, maana yake wenyewe wanaita *maiden speech*. Kwa hiyo, *it was a good start*. (*Makofi/Kicheko*)

Mfuko wa Elimu ya Juu inabidi uangalie mambo yao na *of course* Wizara ya Elimu pia. Unamkopesha mtoto wa maskini kwenda kusoma kozi ambayo hata akimaliza hiyo kozi, kama anavyosema Mheshimiwa Kishimba, atapata

hicho cheti, lakini hana cha kufanya kutokana na kozi hiyo. Ulichofanya ni nini sasa? Kwa nini ulimkopesha *in the first place*? Kwa nini umempotezea miaka yake mitatu halafu haina *utility* yoyote? Zaidi anatoka kule na deni asilimia 15 na riba ya asilimia sita na migogoro mingine na *frustration* ya kuanzia anapomaliza shule tu. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia kwa kweli. (*Makofi*)

Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Asha Mshua.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanah-wataala aliyenipa uwezo na afya njema leo hii nikaweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani zangu za dhati ziende kwa Chama changu cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuridhia kwamba mimi Asha ambaye najulikana zaidi kama Mshua kuwa Mbunge wa Jimbo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mjini Zanzibar kwa imani walionionyesha. Niwahakikishie mbele yako kwamba sitawaangusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa aliyofanya iliyopelekea kupata ushindi wa kishindo wa uchaguzi uliopita. Hiyo ni kuonyesha kwamba utekelezaji ulikuwa wa kuridhisha katika awamu aliyohudumu. Ni matumaini yangu pia huko mbele tunakokwenda mambo yatakuwa mazuri zaidi kwa sababu yale mambo yetu muhimu; *Standard Gauge, Stiegler's Gorge* na mengineyo yote yatakuwa *in full operation*. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. John Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nachukua nafasi hii adhimu sana kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kuwa Rais wa Zanzibar na kuweza kuhudumu kwa *style* yake

ya umahiri, umakini na uhodari na kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unapaa na neema tele kwa Wazanzibar. Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia habari ya Mpango. Nimeusoma na nimeuelewa na watu wengi wameuchangia. Kwa kweli Mpango umepangika, hongera sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na timu nzima mlioandaa Mpango huu. Kwa ujumla wake mipango ya humu inaleta matumaini kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia sekta ya afya na hasa Mpango wa Bima kwa Watanzania wote. Taarifa ya Serikali ilionesha kwamba asilimia 33 tu ya Watanzania wanashiriki fursa za Bima ya Afya. Hadi kufikia 2019, Watanzania walionufaika na huduma hiyo ilikuwa 13,029,636 sawa na asilimia 25 ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iharakishe mchakato wa kuhakikisha kwamba Mfuko wa Bima kwa Watanzania wote unakuwa tayari na mchakato huo wa sheria ukamilike mapema iwezekanavyo. Hii itasaidia kuwa na mfuko mmoja wa Bima ya Afya ili kuwezesha Watanzania wengi kufaidika na huduma hiyo kwani wakiwa na afya njema, watachangia katika shughuli za maendeleo kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya pili ambayo nataka kuizungumzia ni hii ya Hifadhi ya Jamii. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria. Nimejengewa uelewa juu ya Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii inayochangia uchumi kwa kiasi kikubwa. Mifuko hii inachangia uchumi wa viwanda na nachukua nafasi hii kuipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa utaratibu wa Mifuko yetu *NSSF, PSSF* na *WSF*. Nakupongeza sana Mheshimiwa Jenista, wewe na Kamanda wako Waziri Mkuu Mheshimiwa Majaliwa, mmejipanga kweli kweli kuchangia maendeleo na ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu, tuongeze ubunifu wa maeneo ya uwekezaji kama vile viwanda vya kilimo vyenye uhakika wa soko, pamoja na

kupanua huduma zake kwa Watanzania walio kwenye sekta isiyo rasmi kama vile wakulima, vikundi mbalimbali vya kijamii ambapo huko ndiko kuna Watanzania wengi Zaidi. Tukifanikiwa kuchangia mapato basi mifuko yetu hii itazidi kunona na Watanzania wetu watanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo, ahsante sana, nyote nawapongeza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwa kuwa nina vidakika hapa, Mheshimiwa Kuchauka malizia hizo dakika zilizobaki. Mheshimiwa Mbunge wa Liwale.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii niwe mchangiaji wa mwisho kwenye hii hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa watu wengi wameshachangia mambo mengi sana, mimi nataka nianze tu na hii sekta ya kilimo. Ni sekta ambayo imechangiwa karibu na Wabunge wote. Yale mambo ambayo nitayazungumza, siwezi kurudia yale ambayo wenzangu tayari ameshayazungumza. Nataka tu nigusie sehemu moja inayohusu mambo ya masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tuna tatizo la utafiti, pembejeo na mambo mengine, lakini soko ni tatizo kubwa zaidi. Kwa sababu wakulima wengi hata wale wadogo wadogo wanaojitahidi kulima, wakihangaika. Nitoe mfano tu, hapa juzi tumesikia kwamba kuna wakulima wa miwa wa Morogoro wamekosa soko, miwa imeungua moto. Leo kuna wakulima Shinyanga wanasema mchele unakosa soko lakini ukienda Mtwara unakuta mchele kilo moja ni Sh.3,000/= mpaka Sh.4,000/=. Tatizo bado Serikali haijajikita kuhakikisha wakulima wetu wanapata uhakika wa kuwa na masoko ya kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanachangia hapa wanasema wasomi wetu hawako tayari kwenda kwenye kilimo. Jamani, ni msomi gani atakubali kwenda



kwenye kilimo akalime heka 10 au 20 za korosho asikie kwamba korosho zimekosa soko? Huyo mkulima ili aweze kujiandaa lazima ataandika andiko, atakwenda benki, atakopa fedha, atafungua shamba la kulima miwa, akihakikishiwa kwamba Kilombero watachukua miwa, inafika mwisho wa msimu, wanakwambia Kilombero wametoshaka na miwa, haina soko. Huyo msomi ambaye amechukua fedha kwenye mabenki, amekosa soko, anakwenda kuzilipa vipi pesa alizokopa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mkulima gani ambaye tangu amezaliwa amemkuta baba yake analima kwa jembe la mkono, shangazi yake analima kwa jembe la mkono, hajatoka; halafu yeye aseme mimi msomi nimetoka *SUA* naweza kulima kwa jembe hili la mkono litanitoa, litamtoa wapi? Kwa hiyo, tusianze kuwalaumu sana wasomi wetu, lakini lazima tuangalie Serikali imejikita vipi kwenye hili suala la kilimo? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko Waziri mmoja hapa hapa, sikumbuki vizuri, 2015 alisema jembe la mkono linakwenda Makumbusho. Lile jembe mpaka leo halijafika Makumbusho. Lazima tuwe wakweli, bado tuna tatizo kwenye sekta hii ya kilimo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo vilevile tuiunganishe na sekta ya miundombinu. Wako wakulima vijijini mazao yao yanaharibika kwa sababu ya miundombinu mibaya kulifikia soko. Leo Serikali, sera yetu inajikita kujenga barabara tunasema tunaunganisha mkoa na mkoa, tunajenga *trunk road*, tunakwenda *regional road*, lakini tunasahau ziko barabara zinazotakiwa zihudumie wananchi wetu kupelekea mazao kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano tu Wilaya yangu Liwale, sisi ni wakulima wa korosho wazuri sana, lakini kwa sababu hatuna barabara; kutoka Nachingwea kwenda Liwale ni kilomita 124; Nachingwea korosho wanauza 3,000, Liwale wanauza 2,000 kwa sababu hakuna mfanyabishara yuko tayari kukanyaga pale Liwale kufuata korosho. Mnunuzi

akinunua korosho kwa bei ya 3,000 akileta mpaka hata Dar es Salaam itakuwa imefika bei zaidi aliyochukua Mtwara au Lindi. Kwa hiyo, bado kuna tatizo la miundombinu. Kwa hiyo ili kilimo chetu kiweze kwenda sambamba na mpango huu lazima kwanza tufanye mageuzi ya kilimo kwamba tulime kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuhakikishe miundombinu rafiki ya kufikisha mazao haya kwenye viwanda, lakini yapo mazao mengine haya mazao ya msimu, kwa mfano kama nyanya, leo hata ukimwambia mtu afungue kiwanda cha kulima nyanya ambazo zinalimwa miezi miwili, miezi mitatu nyanya hakuna, kile kiwanda anakipeleka wapi, hicho kiwanda anafanya kazi peke yake, maana akishawajiri watu wanachakata hizo nyanya kwa miezi miwili au mitatu, kiwanda kimefungwa kwa sababu nyanya hakuna. Kwa hiyo ni lazima twende na kilimo cha umwagiliaji. Kama kweli tunajenga kiwanda cha matunda, ni lazima tuhakikishe yule mwenye kiwanda anapata matunda muda wote na anapataje matunda muda wote, ni pale tu tutakapoanza kilimo cha umwagiliaji, lakini hiki kilimo cha kutegemea mvua, hakitatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazungumzia mananasi hapa kwa Mheshimiwa Rais mstaafu, kuna mananasi mengi tu, ukienda msimu Chalinze mananasi ni mengi mpaka yanaoza, lakini leo ukifungua kiwanda cha mananasi pale, kitafanya kazi miezi mingapi, miezi miwili au mitatu mananasi yamekwisha, inabidi kiwanda kifungwe na wale uliowaajiri inabidi uwape likizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuwa na viwanda vya kudumu, ni lazima tuwe na uhakika kwamba tunakuwa na kilimo cha umwagiliaji, kilimo ambacho kitamhakikishia mwenye kiwanda cha matunda kile anapata matunda muda wote. Hili ni jambo ambalo nimeona nilizungumzie kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile bado naendelea huko huko kwenye kilimo; tunapokwenda kuzungumzia kilimo

cha umwagiliaji, bado ukienda katika skimu za umwagiliaji leo, bado tunatumia mito yaani hatuwezi kuweka skimu za umwagiliaji hapa Dodoma, hakuna mto, ni mpaka uwe pembeni ya mto ndiyo wanatengeneza kile kilimo cha umwagiliaji. Wakati mwingine yanapotokea mafuriko kama haya, ile mifereji yenyewe imevunjika, imeharibika, hakuna kilimo cha umwagiliaji.

Naiomba Serikali tafadhali tafadhali, kama kweli tunataka tuisaidie nchi hii, tuwasaidie hawa vijana wa nchi hii, lazima tufanye maamuzi ya kufanya mageuzi ya kilimo, siyo hiki kilimo cha kutegemea mvua wala hiki sio kilimo cha msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mwingine, nimefanya kazi kwa Bakharesa miaka zaidi ya 20, wakati ule ngano ilikuwa inauzwa kilo moja Sh.200 nje, ngano ya Tanzania Sh.370. Bakharesa aliamua kwenda kulima ngano Basutu, kilichomkuta alilima mwaka mmoja tu akaacha. Watakuja *OSHA* hapo, watakuja *TFDA*, watakuja sijui Ardhi, watakuja watu wa madini, yaani wanakuja kibao. Ile ngano amelima, amevuna, ngano akiagiza India *by then* ilikuwa 240, ngano alilima Basutu ilifika 400, akaamua kuacha mpaka leo ngano ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli mpaka leo Bakharesa mimi wakati naondoka mwaka 2014 anasindika tani 1,500 *per day*, lakini yote hii anaagiza kutoka nje, *100 percent* anaagiza kutoka nje. Sasa ni lazima kwanza tujenge mazingira, unajua tatizo lingine linakuja kubwa ni kwamba akionekana mtu anataka kufanya biashara, basi yule anaonekana sijui ameiba hela mahali, sijui anataka kufanyaje, atafuatwa milolongo hapo, itaonekana kama vile hafai, kwanza anaonekana mtu ana hela, hata yule anayekwenda labda anapeleka andiko lake, tayari anaanza kwanza kusachiwa, yaani zile pesa watu wanaanza kugawana kabla hazijafika huko shamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ulikuwa ni huo tu. Ahsante sana.

**MWENYEKTI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka. Mheshimiwa kuchauka anaongea kama, lakini anaongea vitu vya msingi sana. Hayo ndiyo matatizo ya nchi yetu, sisi kama Wabunge lazima tuyaelewe na sababu Waheshimiwa Mawaziri wa Serikali ni Wabunge wenzetu yaani *environment*, tunasema nia tu, lakini ile *environment* watu wako *suspicion* nayo kama wanavyosema, yaani mtu akionekana ana hela tayari kikosi kazi na vingine. (*Makofi/Kicheko*)

Mwisho wa siku tunataka nini, kwani sisi tunatakaje na Rais keshasema hapa anataka mabilionea, lakini hapa chini shida, yaani tuna *environment* fulani hivi, kwanza *environment* ya kuhisi mtu yoyote mwenye pesa mwizi, hatufikiri kabisa kama kuna njia halali ambazo Mtanzania anaweza akatajirika, hapana, ila hapa hapa nchini anaweza, sitaki kuongea lugha za kibaguzi, kama Mhindi hivi au nini, hata akiwa na hela za dunia nzima wala hawashuki, wanaona ni sawasawa tu, lakini wewe Mgogo wa Dodoma uwe na hela umetoa wapi? Haiwezekani! Kwa hiyo vitu vingine na *attitudinal*, ni lazima tu-*change* hasa sisi viongozi, ni lazima tubadilike, tukubali kwamba haya mambo ni *possible*.

Michango hii kwenye Mpango kwa kweli inatusaidia sana, maana ndiyo tunapanga jinsi ya kwenda na ole wake huyo mtu mwenye vipesa awe Waziri, mama yangu wee kaiba, kaiba. Sasa kama Waziri lofa, sasa wewe mwananchi wa kawaida utakuwaje? Maana kama yeye tumemkabidhi nchi nzima afikiri, atupeleke mahali, halafu kumbe yeye mwenyewe hawezi hata kujipeleka popote yeye na familia yake, atatupeleka sisi mahali popote huyo mtu? Kwa hiyo, tuache roho ya korosho Watanzania, tukubali haya mambo na tutasogea kwa maana hiyo. (*Kicheko*)

Katibu.

**NDG. RAMADHANI ABDALLAH ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Mipango imemaliza kazi yake kwa muda huu.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge tumeendelea vizuri na mjadala wetu na kesho tutahitimisha. Kwa kweli umekuwa ni mjadala wa aina yake, mjadala mzuri wenye kujenga, tumechambua, tumechangia mwelekeo na kwa mtazamo huu, naamini tutaenda kimataifa, tunakoelekea ni kwema na kwenye mwanga mkubwa Zaidi. Niwashukuru wote.

Kwa leo majina yote tuliyokuwa nayo, wote wamepata nafasi kabisa hakuna aliyebaki hata mmoja. Kwa hiyo wale wachache ambao bado hawajapata nafasi kabisa tutakuwa na fursa kiasi fulani kesho. Pia tutampa nafasi Mheshimiwa Waziri wa Mipango kabla ya kuhitimisha na Mawaziri wengine kufuatana na utaratibu wa *Chief Whip* utakavyokuwa ili sasa tuweze kuhitimisha.

Kesho kutwa tutakuwa na Muswada ule mmoja ambayo umekuja kwa hati ya dharura ambao na wenyewe tutaushughulikia na kumaliza mapema tu siku ya Jumamosi, hata kama mtu anataka kusafiri siku hiyo wala asiwe na haraka, *by* mchana hivi ama kabla ya hapo tutakuwa tumeshamaliza, kwani Muswada ule ni mfupi sana, hauna maneno mengi. Kwa hiyo, tushirikiane siku mbili hizi zilizobaki ili tuhitimishe kazi yetu vizuri.

Kabla ya kuahirisha, kuna funguo wameokota watumishi wetu, itakuwa meza kuu hapa, kama ni ya kwako basi uje uichukue.

Kwa hatua hiyo basi, naomba sasa niahirishe Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.49 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 12 Februari, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*